# MADA: UHAKIKI WA FANI KATIKA NGANO TANO ZA KISWAHILI

**NA**

**JENIPHER OKECH OYOYO**

**C50/66660/2010**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KITIVO CHA SANAA IDARA YA ISIMU NA LUGHA KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2013**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

………………………………. Tarehe ……………………………

Jenipher Okech Oyoyo

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

………………………………. Tarehe ……………………………

Prof .Kineene Wamutiso

(Msimamizi)

………………………………. Tarehe ……………………………

Dkt. R. Timammy

(Msimamizi)

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia mamangu mpendwa Eunice A. Okech pamoja na marehemu babangu Nathaniel Okech kwa kunilea na kunipeleka shule japo kulikuwa na milima na mabonde lakini walijikaza kisabuni. Mungu awarehemu.

Pia naitabarukia mume wangu mpenzi Bwana Oyoyo pamoja na wanangu Annet, Janesophy, Sharon, Kenneth, Jacob na Esther kwa uvumilivu mwingi waliokuwa nao kipindi chote nilichokuwa masomoni. Mliyakosa mapenzi ya mama kwa wanaye lakini mlizidi kunipa moyo. Mwenyezi Mungu awabariki na awape moyo wa shime nanyi mtende vizuri kuliko mimi maishani mwenu.

## SHUKRANI

Kwanza namshukuru Maulana kwa kunineemesha na kunipa siha njema maishani na kuniwezesha kufikia kiwango hiki cha elimu. Pia namshukuru kwa kunipa rasilimali ya kuweza kukilipia kisomo hiki cha shahada ya uzamili kwani wengi walitamani lakini hawakuweza. Kazi hii haingetimia bila ya kudra za Mwenyezi Mungu pamoja na misaada ya kitaaaluma kutoka kwa watu wa aina mbalimbali ambao sitaweza kuwataja wote.

Nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Isimu na Lugha kwa ushauri wao walionipa wakati wote nilipokuwa chuoni; waliniwezesha kuimarika kiusomi. Nyote mliotufunza mlitufaa pakubwa. Siwezi kuwasahau wahadhiri kama. Dkt. Iribe, Prof. Habwe, Dkt. Zaja, Dkt. Mweri, Prof. Wamutiso, Bw. Mung'ania, Dkt. Swaleh.

Shukrani nyingi zaidi ziwaendee wasimamizi wangu Prof. Kineene na Dkt. Timammy. Bila ya ushauri na maelekezo yao na kunirekebisha hatua kwa hatua singeweza kuimaliza kazi hii na kufika tamati. Usaidizi wa Dkt. Timammy ni wa kipekee na hauna mfano; ana roho ya ubinadamu kwani alijitolea kuhakikisha kuwa kazi hii haikupitwa na muda uliowekwa. Mungu akupe maisha marefu ili uweze kuwasaidia wengine.

Sitasahau kuwashukuru wanafunzi wenzangu: Dorin, Grace, Ruth, Omar, Rachel, Obure, Chisia na Joyce. Mawaidha yenu yalinitia shime. Nawashukuru nyote kwa msaada wa vitabu pia. Kwa ndugu zangu Emmanuel, Nelson, Julius, Walter na dada zangu Christine na Dorine, nawashukuru kwa sala zenu na usaidizi wa kifedha uliofanikisha kumaliza kazi hii.

Mwisho namshukuru Shaida Kibibi kwa kuichapisha tasnifu hii. Mungu ambariki kila mmoja aliyeifanikisha kazi hii kwa hali au kwa mali.

# IKISIRI

Tasnifu hii imeshughulikia fani katika ngano teule za Kiswahili kwa kutumia nadharia ya umuundo. Tasnifu hii ina sura sita.

Katika sura ya kwanza, tumeangalia tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu za kuchagua mada ya utafiti na kuorodhesha nadharia tete za utafiti huu. Katika sura hii pia tumeshughulikia yaliyoandikwa kuhusu mada, upeo wa utafiti, msingi wa kinadharia na njia za utafiti. Tulitumia mbinu ya maktabani kukusanya data tuliyohitaji na kuichanganua.

Katika sura ya pili, tumetoa maelezo kuhusu fani na vipengele vyake kama; msuko wahusika, usimulizi, muundo na tamathali za usemi.

Sura ya tatu, imeangazia tathmini ya msuko, wahusika na usimulizi katka ngano tatu za kibunifu kutoka jamii ya Waswahili.

Katika sura ya nne, vile vile tumechanganua msuko, wahusika na mbinu ya usimulizi zilizotumika katika ngano kutoka jamii ya Waswahili vile vile.

Sura ya tano, imeshughulikia matumizi ya lugha na tamathali mbalimbali za usemi kama zinavyojitokeza katika ngano tulizochambua.

Sura ya sita imezungumzia hitimisho tathmini na mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

# YALIYOMO

**UNGAMO** ........ **i**
**TABARUKU** ........ **ii**
**SHUKRANI** ........ **iii**
**IKISIRI** ........ **iv**
**YALIYOMO** ........ **v**

**SURA YA KWANZA** ........ **1**
1.0 UTANGULIZI ........ 1
1.1 TATIZO LA UTAFITI ........ 1
1.2 MALENGO YA UTAFITI ........ 1
1.3 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII ........ 2
1.4 UPEO NA MIPAKA ........ 2
1.5 NADHARIA TETE ........ 3
1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII ........ 4
1.7 MSINGI WA KINADHARIA ........ 8
1.8 MBINU ZA UTAFITI ........ 9
1.9 HITIMISHO ........ 10

**SURA YA PILI** ........ **11**
**MISINGI YA UHAKIKI WA FANI** ........ **11**
2.0 UTANGULIZI ........ 11
2.1 DHANA YA FANI ........ 11
2.2 MUUNDO ........ 12
2.2.1 MUUNDO WA NDANI ........ 13
2.3 MSUKO ........ 13
2.3.1 AINA ZA MSUKO ........ 13
2.4 WAHUSIKA ........ 14
2.4.1 MHUSIKA BAPA ........ 15
2.4.2 MHUSIKA DUARA ........ 15

2.5 MATUMIZI YA LUGHA ........ 15
2.5.1 MAANA NA MATUMIZI ........ 15
2.5.2 SEMI ........ 17
2.6 TAMATHALI ZA USEMI ........ 17
2.6.1 TASHBIHI ........ 18
2.6.2 CHUKU ........ 19
2.6.3 TASHIHISI ........ 19
2.6.4 DHIHAKA/KINAYA ........ 19
2.6.5 NIDAA ........ 19
2.6.6 TAKRIRI ........ 19
2.6.7 USAMBAMBA ........ 20
2.6.8 TANAKALI ZA SAUTI ........ 20
2.7 TASWIRA ........ 21
2.8 VILIWAZO ........ 21
2.9 USIMULIZI ........ 21
2.10 FASILI YA NGANO ........ 23
2.11 HITIMISHO ........ 25

**SURA YA TATU ........ 26**
3.0 UTANGULIZI ........ 26
3.1 TATHMINI YA NGANO YA BINTI MATLAI ........ 26
3.1.1 MSUKO ........ 26
3.1.2 UCHAMBUZI WA WAHUSIKA KATIKA NGANO YA BINTI MATLAI SHAMSI ........ 28
3.1.2 USIMULIZI KATIKA NGANO YA BINTI MATLAI SHAMSI ........ 30
3.2 KISA CHA CHECHE NA SUNGURA ........ 31
3.2.1 TATHMINI YA MSUKO WA NGANO. ........ 31
3.2.2 USAWIRI WA WAHUSIKA ........ 32
3.3 KISA CHA SUNGURA NA SIMBA ........ 34
3.3.1 TATHMINI YA MSUKO WA NGANO ........ 34
3.3.2 USAWIRI WA WAHUSIKA ........ 36

3.3.3 USIMULIZI WA NGANO YA SUNGURA NA SIMBA ................................ 37
3.4 HITIMISHO ........................................................................................ 39

**SURA YA NNE ........................................................................................ 40**
4.0 UENDELEZI WA UCHANGANUZI WA NGANO ............................................ 40
4.1 UTANGULIZI ........................................................................................ 40
4.2 KISA CHA NDOVU NA BINADAMU ............................................................ 40
4.2.1 TATHMINI YA MSUKO WA NGANO ........................................................ 40
4.2.2 USAWIRI WA WAHUSIKA. ..................................................................... 43
4.2.3 USIMULIZI KATIKA NGANO YA NDOVU NA BINADAMU ................... 44
4.3 MIGANI YA FUMO LIYONGO ................................................................... 46
4.3.1 TATHMINI YA MSUKO WA NGANO ........................................................ 46
4.3.2 USAWIRI WA WAHUSIKA ...................................................................... 49
4.3.3 USIMULIZI KATIKA MIGHANI YA FUMO LIYONGO ............................ 51
4.4 HITIMISHO ........................................................................................ 52

**SURA YA TANO ........................................................................................ 53**
**UKIUSHI WA KISEMANTIKI KATIKA NGANO TANO ZA KISWAHILI ......... 53**
5.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 53
5.1 SEMI ........................................................................................ 53
5.2 TAMATHALI ZA USEMI ........................................................................ 55
5.2.1 TASHBIHI ........................................................................................ 56
5.2.2 CHUKU ........................................................................................ 57
5.2.3 TASHIHISI ........................................................................................ 58
5.2.4 DHIHAKA/KINAYA ............................................................................. 59
5.2.5 TAKRIRI ........................................................................................ 59
5.2.6 USAMBAMBA ..................................................................................... 61
5.2.7 TANAKALI ZA SAUTI ........................................................................ 61
5.3 MBINU NYINGINE ZA LUGHA ................................................................ 62
5.3.1 NIDAA ........................................................................................ 62
5.3.2 TASWIRA ........................................................................................ 63

5.3.3 VILIWAZO ........................................................................................ 64
5.3.4 USIMULIZI ........................................................................................ 65
5.4 HITIMISHO ........................................................................................ 66

**SURA YA SITA ........................................................................................ 67**
6.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 67
6.1 MUHTASARI WA MATOKEO ........................................................................................ 67
6.2 KUHUSU NADHARIA TETE ........................................................................................ 68
6.3 MAPENDEKEZO YA UTAFITI ........................................................................................ 69

**MAREJELEO ........................................................................................ 70**

**VIAMBATISHO ........................................................................................ 74**
KISA CHA BINTI MATLAI SHAMSI ........................................................................................ 74
KISA CHA CHECHE NA SUNGURA (JAMII YA WASWAHILI) ........................................................................................ 82
SUNGURA NA SIMBA (JAMII YA WASWAHILI) ........................................................................................ 84
NDOVU NA BINADAMU ........................................................................................ 87
MIGANI YA FUMO LIYONGO ........................................................................................ 90

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Utafiti huu unahusu uhakiki wa fani katika ngano tano zilizoteuliwa kutoka jamii ya Waswahili. Katika sura hii maswala tunayozingatia ni madhumuni ya utafiti, upeo na mipaka na nadharia tete. Vilevile, tunachambua yaliyoandikwa kuhusu mada hii, msingi wa kinadharia na njia ya utafiti. Maswala hayo ni muhimu na yanatupa mwongozo thabiti katika utafiti wetu. Ngano tunazochambua tumeziteua katika kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi (2003) ya Wamitila.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Tatizo la utafiti huu ni kubainisha iwapo mtunzi wa ngano tulizoteua amefaulu katika kuvileta pamoja vipengele vya fani ili kizipa ngano hizo umbo kamili. Uhakiki wa fani ni dhana ya kijumla inayotumiwa kueleza mkabala wa kuhakiki kazi ya kifasihi ambao huchunguza kazi hiyo kwa kuangalia uhusiano kati ya sehemu mbalimbali zinazounda kazi hiyo. Aidha vipengele vya fani vina uamili mkubwa katika kuwasilisha ujumbe uliodhamiriwa na mtunzi kwa hadhira yake. Mbali na hayo, matumizi mazuri ya vipengele vya fani huufanya muundo wa kazi ya fasihi kuvutia hadhira lengwa. Kwa upande mwingine, kutomakinika kwa mtunzi katika matumizi ya fani huifanya kazi ya kifasihi kutokuwa na umbo zuri. Matokeo yake ni kuwa kazi ya kisanii hukosa mshikamano na mwingiliano unaotarajiwa. Matini ya aina hiyo huwa haina uwezo wa kuvutia hadhira.

## 1.2 MALENGO YA UTAFITI

Malengo ya utafiti huu ni kuhakiki fani katika ngano teule za Kiswahili .Katika harakati hizi ,_tunadhamiria kutekeleza yafuatayo:

i. Kubainisha na kuchanganua vipengele mbalimbali vya fani vinavyoingiliana na kukamilishana katika ujenzi wa umbo la ngano.
ii. Kutathmini mchango wa vipengele vya fani katika kuwasilisha maana katika ngano zilizoteuliwa .

iii. Kutathmini kufana au kutofana kwa msanii katika muundo wa ngano teule za Kiswahili.

## 1.3 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Tumechagua mada hii kwa sababu mbalimbali. Kwanza, ngano ni kipengele cha fasihi simulizi kilicho kikongwe na ambacho hakijafanyiwa utafiti wa kina, ikilinganishwa na vijitanzu vingine vya fasihi simulizi kama ushairi, methali, drama na vitendawili. Pili, wazee na kina nyanya waliokuwa wakiwatambia watoto na vijana hapo kale siku hizi wametingwa na shughuli za kujijenga kiuchumi kwa muda mrefu na hawapati muda wa kutosha nyakati za jioni ambao ndio uliokuwa wakati mwafaka wa kutoleana hadithi na vitendawili. Tatu, ngano ni kipengele cha fasihi simulizi ambacho hutahiniwa na baraza la mitihani ya kitaifa katika karatasi ya tatu ya Kiswahili nchini Kenya.

Ngano tulizoteua na kuhakiki zimo kwenye kitabu kilichoidhinishwa na idara ya elimu nchini Kenya kufundishiwa wanafunzi wa shule za upili na vyuo. Kwa hivyo, tunaamini kuwa mada hii itatoa mchango wetu wa kiusomi katika ngano za Kiswahili na kuwatia shauku wanafunzi kufurahia fasihi simulizi hasa ngano za Kiswahili. Vile vile, katika uchunguzi wetu, hatujapata ithibati yoyote ya kuonyesha kuwa kuna utafiti wowote uliokwisha kufanywa kuhusu ngano za Waswahili kwa kutumia nadharia ya umuundo.Kwa hivyo, utafiti wetu utaliziba pengo hili.

## 1.4 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu unahusu matumizi ya fani katika ngano za Kiswahili. Ili kufanikisha uhakiki huu, tumetumia nadharia ya umuundo, ambayo husisitiza kuwa uhakiki wa kifasihi ufanywe bila ya urejelezi wa nje. Kunga wanazozitumia wasanii katika uwasilishaji wa ujumbe ndio lengo letu.

Kwa kuwa dhana ya fani ni pana na ina vipengele vingi, tumechagua kuhakiki baadhi yavyo ambavyo ni msuko, wahusika , usimulizi na matumizi ya lugha.

Tunajadili namna vipengele hivi vya kifani vinavyotumiwa, uamili wake wa kiumbaji na mchango wake katika muundo au umbo la kazi nzima. Lengo letu kuu ni kushughulikia fani na iwapo tunaangalia maudhui kwa undani tunakuwa tumekiuka mpaka wa nadharia ya umuundo, japo ni vigumu sana kutenganisha fani na maudhui kwa sababu fani ndiyo husitiri maudhui.

Vile vile tasnifu hiii, imejaribu kuonyesha mifano mitano ya ngano za Kiswahili zilizoteuliwa kutoka kitabu cha <u>kichocheo cha Fasihi simulizi na Andishi</u> cha Wamitila (2003).

<u>Ngano tunazozichambua ni:</u>

1) <u>Kisa cha Binti Matlai Shamsi-Ngano za Mazimwi.</u>
2) <u>Kisa cha cheche na Sungura-Hekaya</u>
3) <u>Migani ya Fumo Liyongo</u>
4) <u>Sungura na simba-hurafa</u>
5) <u>Ndovu na binadamu-Ngano ya kimafumbo</u>

Sababu za kuhakiki ngano za kitabuni ni kuwa, muda tuliopewa kufanya utafiti ulikuwa mchache na pia tulikuwa na uhaba wa fedha za kuendea nyanjani kukusanya data. Sababu ya pili ni kuwa , ngano za kitabuni zimehaririwa na wataalam wa lugha na hivyo imetutatulia tatizo la uhariri.

## 1.5 NADHARIA TETE

Utafiti huu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo:

i. Vipengele vya fani katika ngano za Kiswahili vimeingiliana na kuhusiana katika ujenzi wa umbo au muundo wa ngano zenyewe.
ii. Vipengele mbalimbali vya fani katika ngano teule za Kiswahili vimechangia pakubwa katika kuwasilisha maana za ngano zenyewe.
iii. Watunzi wa ngano za Kiswahili tulizoteua wamefaulu katika usanifu wa muundo.

### 1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII

Njogu na Chimerah (1999), wamezungumzia fani katika ngano kwa mapana na kueleza kuwa haiwezekani kutenganisha fasihi simulizi na vipengele mahususi vya fani kama vile methali, jazanda, tashbihi, chuku, tanakali za sauti na kadhalika. Mjadala wao kuhusu tamathali hizi za semi umekuwa wa manufaa kwetu kwa sababu tumechunguza matumizi ya lugha katika ngano tano tulizoteua. Uchambuzi wao wa fani umetuwekea mhimili mzuri wa kuchambua fani katika tasnifu yetu. Pia wameelezea kuhusu masimulizi na wahusika.

Wafula na Njogu (2007:54) wameeleza kuhusu nadharia ya umuundo wakiwanukuu Leech na Short (1981) wanaeleza kwamba, "Fasihi ni umbo lenye viungo viwili, maudhui na fani na kwamba viungo hivi vyaweza kutenganishwa. Hapa muundo unafananishwa na mtindo ukimaanisha lugha inayotumika katika maandishi au mazungumzo ya kifasihi". Kauli ya Short ni kwamba wazo kwanza huota katika fikra za mwana sanaa au msemaji yeyote wa kifasihi. Wadhifa wa mwana sanaa ni kuainisha na kutumia lugha inavyofaa kuelezea wazo.

Wanaeleza pia kuwa umuundo huleta pamoja vipengele mbalimbali vya lugha na kuvipa umbo moja lisiloweza kugawika kwani viungo hivyo haviwezi kutenganishwa na kujisimamia kisha vikaleta maana. Kazi hii imetufaidi sana kwani imetuelekeza vizuri kuhusu nadharia tutakayotumia inavyobainisha lugha katika vitengo viwili yaani lugha dhahiri na lugha dhahania na jinsi ambavyo matawi mbalimbali ya lugha hayawezi kufasiriwa nje ya mipaka ya muundo yaani lugha ni mfumo wa muundo unaojitosheleza na unaojieleza.

Wamitila (2004) amechangia katika maelezo ya nadharia ya umuundo akieleza kuwa "wakiki wakimuundo unajishughulisha na kuangalia sehemu mbalimbali za kazi ya kifasihi au viwango mbalimbali na kuonyesha jinsi ninavyounda muundo mzima. Viwango hivi ni vipengele vya fani.

Steere (1889) alikusanya simulizi mbali mbali kutoka kwa jamii ya Waswahili wa Zanzibar na kuzihariri. Hadithi hizi zilikuwa maarufu sana. Lengo la Steere lilikuwa kuwahamasisha watu wengine waliojua kusoma na kuandika kuweza kupata picha ya uandishi wa hadathi.

Kwa kiasi fulani tunaafikiana na Steere katika kazi ya kushughukia masimulizi ya Waswahili lakini tunatofautina katika malengo. Yeye alishughulikia waliojua kusoma na kuandika tu na kulisahau tabaka la wasio wasomi. Malengo ya fasihi simulizi kwa jumla ni mengi, miongoni mwao yakiwa kufunza maadili kwa jamii, kuburudisha, kuonya, kuendeleza tamaduni za jamii na kadhalika. Hata hivyo, kazi yake imetupa muelekeo mzuri kwani ngano tulizohakiki zilikusanywa na kuhaririwa na Wamitila kutoka kwa jamii ya Waswahili.

Katika mwaka (1970) Steere alizitafiti ngano mbalimbali kama hadithi ya Liyongo, Kisa cha sultani Darai na nyingine nyingi na kuzitafsiri kutoka lugha ya Kiswahili hadi kingereza. Kazi yake pia imetufanikisha katika utafiti wetu kwani hadithi ya Liyongo tumeihakiki.

Ngole na Henero (2006), wamefanya utafiti wa ngano katika Jamii ya Wasukuma nchini Tanzania. Kazi yao imetusaidia katika matumizi ya mbinu za lugha japo walifafanua zaidi matumizi ya methali.

Wamitila (2003) amejadili vipengele mbalimbali vya fani. Vipengele hivyo anavyoshughulikia ni msuko, usimulizi, wahusika, tamathali za usemi miongoni mwa nyingine. Pia ametuwezesha kupata ngano alizohariri tayari. Kazi yake imeufanikisha uhakiki wetu kwa kiwango kikubwa kwani lugha ya kitamathali alizotumia imetupa mwongozo.

Mghanga (1984) katika tasnifu yake ya uzamili alichambua ngano tano za Kidawida zilizoandikwa na Mbele. Katika ngano hizi, Mghanga alishughulikia maudhui kwa kutumia nadharia ya Kimarxisti. Kazi hii ni muhimu kwa utafiti wetu kwa sababu

inaangazia maudhui ambao ndio msingi wa fasihi yoyote ile. Fasihi haiwezi kuwa fasihi bila ya mwandishi, msimulizi au msanii kutumia lugha kwa njia ambayo itamwezesha kuwasiliana na wasomaji ama wasikilizaji wake kwa njia ya kuwavutia na ambayo itawafanya wasome ama wasikilize ujumbe wake.Lugha ndio malighafi ya kuumba sanaa ya fasihi na matumizi ya lugha ama mtindo una uhusiano wa kidaelektiki na maudhui.

Njue (1989) katika tasnifu yake ya uzamili amechambua ngano za Waswahili huku akishughulikia ujumbe pamoja na funzo kwa jamii iliyozizusha. Pia amezungumzia wahusika, ploti ya ngano na umuhimu wa fasihi kwa jumla. Uhakiki wake uliohusisha baadhi ya vipengele vya fani kama wahusika na ploti umetufaa, tofauti ni kuwa amezama zaidi katika ujumbe na funzo ambavyo ni vipengele vya maudhui.

Timammy (1990) katika tasnifu yake ya uzamili amehakiki fani katika hadithi za jamii ya Waswahili. Amechanganua matumizi ya lugha na tamathali mbalimbali za usemi. Kazi hii ni muhimu kwa utafiti wetu kwa sababu imeangazia kipengle cha mtindo ambacho ni lugha tofauti na kazi yetu ni kuwa utafiti wetu umetumia nadharia ya umuundo.

M'Ngaruthi (2008) anajadili kuhusu vipengele mbali mbali vya fani, isitoshe, amezungumzia kuhusu mtindo na maudhui, ploti, wahusika, usimulizi, mandhari, dhamira , vichekesho na aina mbalimbali za ngano. Ingawa kazi yake imejikita katika mawanda mapana, mchango huu
umetuongoza katika kuchanganua vipengele mbalimbali vya fani katika ngano teule za Kiswahili.

Nandwa na Bukenya (1983) walizungumzia fasihi ya kiafrika kama nyanja tasa kwa sababu haijafanyiwa utafiti wa kuridhisha ambao unaweza kuikuza na kuleta uelewa zaidi kuihusu .

Ngure (2007) katika kitabu chake kilichoidhinishwa na idara ya elimu kwa ajili ya kuwaandaa wanafunzi wa kidato cha nne kwa mtihani amejadili tanzu zote za fasihi simulizi. Katika kazi hii amechunguza maswala katika fasihi simulizi hasa ngano kwa uwazi. Amejadili sifa za ngano na umuhimu wake kwa jamii, wahusika, ploti , mandhari na maudhui. Pia ameshughulikia sifa za muundo wa ngano. Vile vile amechambua mtindo wa usimulizi, ploti, wahusika na mbinu nyingine za kisanaa. Maoni yake juu ya mbinu hizi za kisanaa yametusaidia katika utafiti wetu.

Finnegan (1970) anaelezea kuhusu Fasihi simulizi ya kiafrika. Anaeleza kuwa “Fasihi hii inatungwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia yam domo na vitendo bila kutumia maandishi”. Anaendelea kusema kuwa hizi ni hadithi za jadi, nyimbo, mashairi, vitendawili, methali n.k. pia anasema kuwa nyenzo za sayansi na teknolojia hazihusishwi katika kubuni, kutongoa na kuifadhi sanaa hii. Kazi yake imetufaa katika utafiti wetu kwani tumepata fasili mbalimbali za Fasihi simulizi.

Naye Matteru (1987) ameainisha tanzu za Fasihi simulizi katika viwango vitatu, navyo ni Nathari, ushairi na semi. Tumefanikiwa katika nathari ambapo tumepata kipera chake kama ngano. Ametaja aina mbali mbali za ngano kama hekaya istihara, kharafa na kuainisha ngano za kubuni na kihistoria. Sisi vile vile tumechambua ngano za kubuni na kihistoria. Kwa hivyo kazi yake imetupa mwelekeo katika kazi yetu.

Mbughuni,(1982) alifanya utafiti kuhusu methali za Kiswahili akizungumzia maadili yapatikanayo katika methali, maana ya methali zenyewe huku akieleza kuwa methali huwa na sehemu mbili, sehemu ya kwanza ikiwa ni swali na sehemu ya pili ikiwa ni jibu la swali.Vile vile alizungumzia mtazamo wa wanawake katika jamii ya Waswahili akifanya utafiti wa Fasihi Simulizi nchini Tanzania.Kazi yake imechangaia katika utafiti wetu kwani baadhi ya methali alizotumia zinapatikana katika ngano za Kiswahili tulizohakiki.Mtazamo wa jamii ya Waswahili kuhusu wanawake barani Afrika ni sawa.

## 1.7 MSINGI WA KINADHARIA

Uhakiki huu umejikita katika nadharia ya umuundo. Nadharia hii imetufaa sana katika kuchanganua vipengele mbalimbali vya fani katika ngano zilizoteuliwa ili kubainisha jinsi vipengele hivyo vinaungana na kuunda umbo la kazi nzima. Nadharia hii iliibuka nchini Czechoslovakia na inahusishwa na wanaisimu wa shule ya Prague kati ya miaka ya 1928-1946, ambao walihusika na Urasimu wa Kirusi kabla ya kuanguka kwake. Earlich(1969) anaeleza kuwa kuzuka kwa shule ya isimu ya Prague (SIP) kulihusishwa sana na urasimu na hasa kikundi kimoja cha wanaisimu wa Moscow.

Miongoni mwa waasisi wa nadharia ya umuundo ni Roman Jakobson, Jan Mukarovsky, N.S. Trubetzkoy, Boris Tomaserky na Ren Wellek. Culler, J. (1975:4-5) anaeleza kuwa wasomi waliathiriwa na mawazo ya Ferdinand de Saussure kuhusu dhana za kiisimu za 'Langue' na 'Parole'. Saussure alibaini kuwa Parole ni lugha ya kimatumizi ilhali 'Langue' ni mfumo lugha ulio na jumla ya taratibu za lugha ambazo msemaji wa lugha hizo anazifahamu.Kulingana na Saussure 'Langage' huundwa kwa "Langue na Parole"

Kwa kurejelea dhana hizi, wanaumuundo walielezea kuwa fasihi inaweza kuangaliwa kama mfumo wenye kanuni zake ambazo kila msanii anahitaji kuelewa na pia aelewe jinsi ambavyo mfumo huo unavyoweza kutumiwa katika mawasiliano na hata kimuundo. Walisisitiza kuwa ili kuelewa mfumo wa kazi ya kifasihi, lazima mhakiki achunguze matumizi ya lugha katika maandishi au mazungumzo, vipashio vyake na mahusiano ya vipashio hivyo. Kwa mantiki hii, wanaumuundo walielekea kuashiria kuwa fasihi ni mfumo unaojisimamia kama 'Langue' kwa kuwa na kanuni zake. Hivyo kazi ya kifasihi inafaa kuangaliwa kwa mujibu wa kanuni za utunzi zinaoitawala. Kwa mfano katika uhakiki wa ngano za Kiswahili, unastahili kuchunguza lugha ilivyotumika pamoja na kaida zinazotawala utunzi wa hadithi na kutathmini ikiwa mtunzi anatekeleza kaida hizo.

Pia, wanaumuundo walitumia dhana ya ukinzani uwiliuwili iliobuniwa na Saussure.Walieleza kuwa dhana hii inaweza kutumiwa kuelezea maana ya maneno kutokana na vinyume vya maneno hayo. Ukinzani uwiliuwili katika fasihi unaweza

kutumiwa katika vipengele zaidi kama vile kutofautisha sifa za wahusika. Aidha wanaumuundo walitumia dhana za Saussure za kiashiria na kiashiriwa.Saussure aliona ulimwengu wa lugha kuwa unajengwa kwa viashiria na viashiriwa na kuwa viashiriwa hubainishwa na viashiria. Wanaumuundo walionelea kuw vipengele mbalimbali vya fani ndivyo viashiria.Maana inayotokana na vipengele hivi ndivyo viashiriwa. Wanaumuundo walijihusisha na uhakiki wa mashairi na tungo nyingine za kifasihi. Walichunguza upatanifu wa kisauti, vina, mizani, wizani, toni na arudhi kwa jumla. Pia walisisitiza umbo la msuko, hadithi na usawiri wa wahusika. Pia wanaumuundo walisisitiza hali ya juu ya ubunifu katika matumizi ya lugha. Walipendekeza mbinu za ukiushi katika matumizi ya lugha kama vile tamathali za usemi.

Wanaumuundo walisisitiza uhuru na upekee wa kazi ya kifasihi.Waliamini kuwa kazi ya kisanaa haifai kuwa na urejelewa wa nje.Walipinga hatua ya kuhusisha fasihi na miktadha ya kijamii, kihistoria, kisiasa na kifilosofia. Nadharia ya umuundo inatufaa katika utafiti huu kwa kuwa inatilia mkazo muungano na muingiliano wa vipengele mbali mbali vya kifani katika ujenzi wa umbo moja la kazi ya kifasihi. Hivyo inaafiki malengo yetu katika utafiti huu.

Wasomi mbalimbali kama Massamba (1999) wamezungumzia nadharia ya umuundo kwa kina na kuelezea chimbuko lake na wasisi wake.

Wafula na Njogu (2007) wamezungumzia matumizi ya lugha yanavyojitokeza katika nadharia ya umuundo na matawi ya lugha .

## 1.8 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu tumeufanyia maktabani ambapo tumedurusu matini kadhaa zenye manufaa kwa utafiti wetu. Kama vile vitabu,tasnifu zilizojadili vipengele vya fani na pia majarida na makala mbalimbali yaliyo na mada zinazorejelea ngano kwa jumla. Pia tulisoma ngano tulizoteua na kuzichanganua kimuundo.Tulitilia mkazo muundo, wahusika, ploti na mbinu za lugha.Pia tulisoma kuhusu nadharia ya umuundo kubainisha sifa zake kutoka maktaban.

### 1.9 HITIMISHO

Katika sura hii tumejadili juu ya tatizo la utafiti,malengo ya utafiti na sababu za kuchagua mada. Pia tumeshughulikia upeo na mipaka ya utafiti,yalioandikwa kuhusu somo na msingi wa kinadharia ambayo ni umuundo na mwisho tukajadili njia tulizotumia katika utafiti wetu ambapo tulijikita sana maktabani.Sura inayofuata inahusu misingi ya uhakiki wa fani.

# SURA YA PILI

# MISINGI YA UHAKIKI WA FANI

## 2.0 UTANGULIZI

Sura ya kwanza inahusu mambo ya kiutangulizi ya utafiti huu.Sura hii ya pili inahusu ufafanuzi wa misingi ya uhakiki wa fani. Mwanzo kabisa tunafafanua dhana ya fani na kueleza vipengele vyake mbalimbali.Kwa kuwa vipengele vya fani ni vingi na vipana mno, tunajadili tu vipengele ambavyo tumevitumia katika uhakiki wa ngano tulizoteua.

## 2.1 DHANA YA FANI

Wataalamu na wahakiki wa fasihi wanakubaliana kuwa fani ni jumla ya viambajengo vya kazi ya kifasihi vinavyotumiwa na msanii katika kupitisha ujumbe wake kwa hadhira. Wataalamu hawa ni pamoja na Mbatiah (2001),Wamitila (2003), Njogu na Chimerah (1999).

Wamitila (2003:41) anaeleza kuwa fani hutumiwa kueleza muundo au mpangilio wa kazi fulani ya kifasihi au hata sehemu zake. Fani hueleza mbinu na mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo au maudhui.

Naye Mbatiah (2001) anasema kwamba dhana ya fani ina maana mbili. Kwanza ni jumla ya vipengele vya kimtindo na kisanaa katika kazi ya kifasihi vinavyojenga kiunzi cha kubebea ujumbe au maana mahususi. Pili ni kategoria ya fasihi, yaani utanzu kama ushairi, drama na riwaya. Kwa uchunguzi wetu tunaona ya kwamba wataalamu hawa wawili wanaelekea kukubaliana katika kijelezi cha kwanza kuwa fani ni vipengele vya kimtindo na kisanaa vinavyojenga kiunzi cha kubebea ujumbe na maana mahususi. Kijelezi hiki kina maana kuwa fani ni zile mbinu ambazo msanii anatumia ili kuufikisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa.Kimsingi, kazi za kifasihi huwa zimegawika katika sehemu mbili kuu. Maudhui na fani. Maudhui ni maswala mbalimbali yanayozungumziwa na mtunzi katika kazi ya kifasihi.Maudhui pia hujulikana kama yaliyomo. Kwa upande mwingine fani huwa ni vipengele vya kisanii vitumiwavyo kuyawasilisha maudhui. Mbali na kuyawasilisha maudhui, fani pia huwa na uamilifu wa

kuupa utungo wa kifasihi umbo mahususi. Umbo lenyewe linaweza kuwa la ndani au la nje. Kuhusu ngano tunazochambua, umbo la ndani hujengwa kwa matumizi ya lugha, wahusika, usimulizi n.k.

Katika uhakiki wetu hatutajishugulisha na umbo la nje kwani hushughulikiwa zaidi katika tungo za kishairi ambapo umbo la nje hujengwa kwa vipengele kama vile beti, mishororo, vina, mizani n.k.Wataalamu wa nadharia ya umuundo wanasisitiza na kutilia mkazo uhakiki wa kifani katika kufasiria matini na kupimia kufana au kutofana kwa mtunzi katika kazi yake ya usanii.

**2.2 MUUNDO**

Muundo ni umbo la kitu. Muundo unaeleza jinsi kitu fulani kilivyoundwa kwa kukitazama na hata kukigusa. Muundo pia hurejelea jumla ya uhusiano unaokuwako kati ya visehemu mbalimbali vinavyounda kitu kamili au cha kijumla. Katika utafiti wetu tunaangalia muundo kama vile vijisehemu vidogovidogo ambavyo huunda kazi nzima ya kifasihi.

Mbatiah (2001 :59) anaeleza kuwa 'Muundo ni uhusiano wa elementi za kazi za kifasihi katika mpangilio dhabiti unaozishikamanisha elementi hizo'.

Maelezo haya yanaoana na yale ya Wamitila (2003 :153) ambaye anasema kuwa "dhana hii ya muundo hutumiwa kueleza sifa za nje zinazoipa kazi ya fasihi sura za kutambulikana.Hata hivyo si lazima elementi za kimuundo ziweze kuonekana kijuujuu. Baadhi ya elementi huwa za kindani".

Kutokana na sababu hii, sharti hadhira isome kazi inayohusika ili kubaini na kuelewa elementi hizo. Hali hii husababisha kuwepo kwa aina mbili kuu za miundo katika kazi za kifasihi. Muundo wa ndani na muundo wa nje.

### 2.2.1 MUUNDO WA NDANI

Muundo wa ndani ni aina ya muundo wa kazi ya kifasihi ambao hauonekani kwa macho. Hujumuisha vipengele ambavyo sharti hadhira isome kazi ya kifasihi ili iweze kuvibaini. Kimsingi muundo wa ndani hujengwa kutokana na muingiliano baina ya vipengele mbalimbali vya kifani kama vile usimulizi, msuko, wahusika, matumizi ya lugha, wakati n.k. Kwa hivyo muundo wa ndani ni dhana inayoingiliana  sana na msuko, yaani mfuatano wa matukio na mahusiano yake kiwakati na kiusababishi. Muundo wa nje sitaushughulikia kwa sababu ambazo nilitoa mbeleni.

## 2.3 MSUKO

Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa msuko ni mtiririko au mfululizo wa matukio yanayojenga hadithi na namna matukio hayo yanavyosababishana. Njogu na mwenzake wanaendelea kueleza kuwa msuko unaweza kuelezwa kama mtiririko wa vitendo na namna vitendo hivyo vinavyozuana.

Kwa ujumla msuko hurejelea mpangilio wa matukio  yanayopatikana katika ngano na huhusisha matendo ya mhusika mkuu na jinsi yanavyoathiri wahusika wengine katika kazi ya kifasihi.Kwa kawaida msuko hueleza jinsi ambavyo matukio. Wamitilah (2003 :32) anasema kuwa:*‘muundo wa hadithi ni muhimu. Muundo huu ndio tunaouita msuko’*.

Hapa tunaangalia jinsi matukio ya ngano yalivyopangika kuanzia mwanzo kwenye kitangulizi. Kwenye sehemu ya kitangulizi, panazuka mvutano wa usimulizi  ambao unaendeleza mgogoro kati ya wahusika walioko, kuwepo kwa taharuki, harakati zao hadi kilele cha usimulizi au upeo na hatimaye mwisho wake.

### 2.3.1 AINA ZA MSUKO

Kimsingi kuna aina mbili za msuko. Msuko sahili na msuko changamano. Msuko sahili ni aina ya msuko ambao ni wa moja kwa moja. Hoja hii ina maana kuwa msuko sahili huwa na matukio yanayotiririka kuanzia mwanzo hadi mwisho. Matukio hufuatana kiwakati na kiusababishi.Msuko sahili hauna urejelezi wa nyuma. Aghalabu msuko wa

aina hii hupatikana katika tungo fupi kama ngano na mashairi. Tendi fupi za Kiswahili pia huwa na msuko wa aina hii.Kulingana na Wamitila (Khj) msuko sahili pia hujulikana kama msuko msago. Kwa upande mwingine, msuko changamano ni aina ya msuko ambao huenda mbele na nyuma. Hoja hii ina maana kuwa msuko wa aina hii hutumia mbinu rejeshi kwa wingi. Kutokana na hali hii huwapa wasomaji hamu ya kuendelea kusoma zaidi na zaidi ili wapate kufuatilia hadithi husika na kupata maana.Kulingana na Ngara (1985) msuko changamano hujulikana kama msuko wa kioo. Msuko wa aina hii huwa na kipengele cha wakati na vipengele kama wahusika na usimulizi ambapo lazima kuwepo na mahusiano ya vipengele hivi na matukio ambayo yanatendwa katika nyakati tofautitofauti. Nyakati hizi zinapowasilishwa katika hadithi lazima ziwe katika wakati uliopita, uliopo na hata ujao, na huu muundo ndio unaoleta urejeshi katika hadithi.

## 2.4 WAHUSIKA

Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya kifasihi; matendo ya viumbe hawa hufanana na yale ya binadamu. Wataalamu kama Mbatiah (2001), Wamitila (2003), Wamutiso (2005) , Ngure (2007) na M'Ngaruthi (2008) wanadai kuwa wahusika ni watu, wanyama, ndege, wadudu miti, mashetani, majini n. k wanaotumiwa na watunzi katika utendaji na upitishaji wa ujumbe . Kutokana na matendo na mazungumzo yao wanatudokezea kuhusu ujumbe wa kazi inayohusika.

Kulingana na maelezo ya wataalamu hawa, ni dhahiri kuwa kila mhusika akiwa ameshikilia jukumu lolote lile, ana umuhimu mkubwa sana katika kazi ya sanaa. Kila mhusika hupenyezwa katika nafasi yake maaalum ili kutimiza majukumu maaalum ya msanii hata kama anapewa nafasi ndogo sana, hataonekana kama kajitokeza kisadfa. Wahusika wengine hushirikishwa kwa kupewa nafasi ya kutenda, kusema, kujiwasilisha na kujitambulisha kwa hadhira . Wahusika hawa huingiliana kwa njia nyingi na katika mahusiano yao tunapata mwanga na kuweza kuelewa jamii kama mfumo wa maumbo uliokamilika. Ni muhimu kuangalia wahusika kama viwakilishi vya binadamu katika jamii halisi kwani kila mhusika huwa na sifa nzuri au mbaya zinazopatikana katika binadamu wa kawaida.

Msanii anapowasawiri wanyama, wadudu, ndege na vitu visivyo na uhai vitende kama binadamu halisi huwa na malengo mbalimbali. Kwanza hutumia mafumbo kwa wasikilizaji anapotaka kujikinga kutokana na athari za mazingira yasiyofaa kama ya kisiasa au uongozi mbaya . Athari za wahusika huonekana kutokana na matendo ya wahusika vivuli. Wamitila (2003) amewaainisha wahusika katika makundi kumi na sita ambapo Forster (1927) anawaainisha katika makundi mawili makuu , ambao ni wahusika bapa na wahusika duara .

### 2.4.1 MHUSIKA BAPA

Kulingana na Wamtila (2003) mhusika bapa ni aina ya mhusika ambaye habadiliki tangu mwanzo hadi mwisho. Mhusika wa aina hii huwa na sifa na matendo yale yale kuanzia mwanzo hadi mwisho. Ikiwa ana sifa mbaya, sifa hizo huendelea hadi mwisho wa kazi au usimulizi.Ikiwa ana sifa nzuri, basi sifa hizo pia huendelea hadi tamati.

Kuna aina mbili za wahusika bapa,bapa sugu na bapa kielezo. Wahusika bapa vielezo huwa hawabadiliki, vile vile hupewa majina ambayo yanaafikiana na matendo yao na tabia zao. Majina ya wahusika hawa huwa kama kielezo cha kifupisho cha wasifu wao. Mhusika bapa kielezo huwa na sifa au tabia nzuri ambazo huchukuliwa kuwa kielezo au kitu cha kuigwa.

### 2.4.2 MHUSIKA DUARA

Mhusika duara ni kinyume cha mhusika bapa. Mhusika duara hubadilikabadilika kitabia kila mara. Kutokana na kubadilika kwake, mhusika duara huonekana kuwa na sifa zinazokaribiana na zile za binadamu wa kawaida, kubadilika kwake pia huwa ni njia ya kuonyesha uhalisia wa kijamii.

## 2.5 MATUMIZI YA LUGHA

### 2.5.1 MAANA NA MATUMIZI

Kimani na Chimerah (1999: 6-8) kwa mujibu wa mhakiki wa kirusi, Roman Jacobson, “fasihi ni matumizi ya nguvu dhidi ya lugha ya kawaida kimakusudi” katika kauli hii, Jakobson ana maana kwamba fasihi huichukua lugha ya kawaida alafu ikaifinyanga,

ikaiunda huku na huku hadi ikaifanya ipendeze. Hivi ni kusema kwamba, kile kinachosemwa kifasihi huwa kimeinuliwa kwa matumizi ya lugha hivi kwamba mdundo wake si wakaida. Yaani fasihi ni matumizi ya lugha kwa ufasaha.

Lugha iliyotumika katika kazi ya fasihi inapendeza, inavutia na kutulazamisha tuitafakari maradufu. Maana hii ya fasihi ndiyo iliyotolewa na wanamuundo wakirusi kama Victor Shklovsky na Boris Tomashvsky. Pia kwa mujibu wa wanamuundo, kitu kinachotofautisha lugha ya fasihi na lugha nyingine ni uwezo wa fasihi wakulemaza lugha ya kawaida. Kwasababu ya nguvu za mbinu za kifasihi, lugha ya kawaida inavutwa vutwa, inafinyangwa na inapondwa pondwa. Lugha ya fasihi ni lugha iliyofanywa ngeni. Kwasababu ya ugeni wake, ulimwengu wa kawaida nao unakuwa mgeni, usiokuwa wa kawaida na uliokengeushwa. Hii inadhibitishwa na mbinu mbali mbali ambazo zimetumiwa katika ngano tulizo hakiki ambazo zimekubaliana na urasimu kwa kuipa lugha ya fasihi upekee.

Kirumbi (1975:10) anasema kuwa ,"Tusemapo fasihi hujengwa na maneno , lazima maneno hayo yawe ni maneno zaidi ya maneno mengine,fasihi si kuwa na maneno ya kisanaa, bali ni kutumia maneno ya kila siku kisanaa." Kirumbi anathibitisha kuwa lugha itumiwayo katika fasihi imerembeshwa ili kuleta mvuto kwa hadhira.

Naye wamitila (2003)anakubaliana na mawazo hayo na kusisitiza kuwa lugha ndiyo nyenzo inayotofautisha fasihi na sanaa nyingine kama uchoraji, ufinyanzi, ususi na nyinginezo.Tukiangalia fasili zote hizo, jambo kuu ni ule uamilifu wa lugha kama chombo cha kupashia habari.

Katika uhakiki wa kazi ya kifasihi, mhakiki hawezi kukwepa suala la lugha kwa maana hiyo ndiyo nyenzo kuu ya fasihi. Katika tasnifu hii tunabainisha sifa za lugha ya ngano pamoja na dhima yake na jinsi inanvyojipambanua na lugha ya kawaida. Vilevile ni vyema msanii aielewe hadhira yake ndiposa achague ni kiwango kipi cha msamiati atakachotumia.

Msanii anaweza kuwa na mawazo mazuri ya kupasha hadhira yake lakini atumie lugha ngumu yenye msamiati mzito kiasi kwamba hadhira lengwa isielewe. Jambo hili husababisha kutofanikiwa kwa msanii katika malengo yake kwani jukumu kuu la lugha ni kuwasilisha fikra za msanii. Tunaangalia kiwango cha lugha cha tamathali za usemi katika uhakiki wetu ili kuona jinsi ambavyo lugha ni muhimu katika kazi ya kifasihi.

### 2.5.2 SEMI

Misemo ni matumizi ya maneno ya kawaida kinjozi kwa njia isiyokuwa ya kawaida. Misemo huhitaji mtu kufikiria kwanza ndiposa afichue maana ya maneno husika. Misemo mingi hubuniwa  na jamii. Misemo katika jamii moja hutofautiana na jamii nyingine. Hii ni kwa sababu  baadhi ya misemo hutungwa kutokana na mazingira pamoja na itikadi za jamii. Misemo hutumika  kwa lengo la kusitiri maana na pia kumfanya msomaji kutafakari ujumbe uliopo.

Wamitila K. (2003) anakubaliana na kauli hii kwa kueleza kuwa semi ni neno lenye upana ambalo hutumiwa kuelezea matamko fulani yanayoelezea ukweli fulani. Aidha, semi ni kauli za maneno kadha yenye maana iliyofichika.

## 2.6 TAMATHALI ZA USEMI

Tamathali za usemi hujulikana pia kama lugha ya kitamathali. Tamathali za usemi ni mojawapo wa dhana kongwe zaidi katika fasihi za ulimwengu. Dhana hii imetumika katika uhakiki wa fasihi tangu enzi za nadharia ya balagha ya zamani. Dhana hii imeelezwa na kuainishwa na wataalamu mbalimbali wa fasihi katika makamusi na pia vitabu vya kinadharia. Japo wataalamu wengi wa fasihi ya Kiswahili wameishughulikia dhana hii, uainishaji wake ambao ni wa wazi zaidi umefanywa na Kuhenga (1977), Wamitila (2008), Mbatiah (2001) na Holman na Harmon (1986). Wataalamu hawa wanakubaliana kuwa tamathali za usemi ni dhana ya kifasihi ambayo hutumiwa kuelezea aina ya ukiushi wa kimaksudi katika matumizi ya lugha ya kawaida au iliyozoeleka.

Wanaelezea kuwa ukiushi huu unaweza kuwa katika viwango vya maana (semantiki) na mpangilio wa maneno (sintaksia) ili kuleta maana mpya au msisitizo. Kwa hivyo, tamathali ya usemi ni fungu la maneno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine.

Tamathali ya usemi huwa ni mbinu ya kupimia usemi wa mtunzi. Ubunifu lazima ujitokeze katika matumizi ya tamathali mbalimbali za usemi. Pia tamathali za usemi huvutia wasomaji na kuwapa hamu ya kutaka kusoma zaidi. Huwafanya wasomaji kutafakari kuhusu wanayoyasoma na kulinganisha na mazingira na mandhari yao. Ni vyema tufahamu ya kwamba, tamathali za usemi nyingi huwa na mpaka mdogo sana kati yazo. Msomaji anastahili kuwa na uelewa wa kina ili aweze kupata ujumbe ulionuiwa na mtunzi.

Tamathali za usemi ni nyingi mno. Zile zinazochukua nafasi muhimu katika kazi za kifasihi na hasa ngano ni pamoja na sitiari, tashbihi, kinaya, chuku, tafsida, tabaini, maswali ya balagha, nidaa, usambamba, tashihisi na taashira. Kwa kuwa tamathali hizi ni nyingi, hututaweza kuzijadili zote. Tumejadili tu zile ambazo zinatufaa katika utafiti huu.

### 2.6.1 TASHBIHI

Tashbihi ni mbinu ya mlinganisho wa vitu viwili au zaidi vyenye hulka tofauti kama vile sitiari. Hata hivyo tofauti na sitiari, tashbihi hutumia viungo vya ulinganishaji.

Msokile (1992) anafafanua kuwa aina hii ya tamathali hutumia ulinganisho wa mambo ama vitu kwa kutumia viunganishi ‘ja’, ‘mithili ya’, ‘mfano wa’, ‘sawa na’ na ‘kama’. Mtunzi hutumia ulinganishi huu kusisitiza sifa fulani na pia kujenga picha ya aina fulani akilini ambayo athari yake ni ya kudumu zaidi.

### 2.6.2 CHUKU

Chuku pia hujulikana kama udamisi. Ni mbinu inayotumika kueleza hali ya kukikuza kitu, mtu au hali kupita kiasi. Matumizi ya mbinu hii hudhamiriwa kusisitiza sifa hiyo ya ukubwa au udogo. Kauli zinazotumika katika mbinu hii huwa ni za kutiliwa chumvi ili kusisitiza na pia kuchekesha. Kwa kutumia chuku, sifa za kawaida za kitu kinachohusika hukiukwa. Kitu hicho huweza kudunishwa au kukuzwa. Katika Kiswahili chuku hujulikana kama "kutia chumvi".

### 2.6.3 TASHIHISI

Wales (2001:349) anafasili tashihisi kuwa; 'Ni tamathali ya usemi ambapo kitu kisicho na uhai, mnyama, kisicho binadamu au chenye sifa za kidhahania kinapewa sifa za binadamu.' Tamathali hii hutumiwa kuleta mvuto wa kisanaa na athari fulani za kihisia.

### 2.6.4 DHIHAKA/KINAYA

Wamitila (2003) kuihusu tamathali hii, anasema kwamba msemaji au mwandishi hutumia usemi unaoficha hisia zake kumhusu mtu au kuihusu hali fulani. Kimsingi, pana kinaya fulani katika maneno yaliyotumiwa. Sababu kuu ya kutumia dhihaka ni kumcheka na kumkera mtu.

### 2.6.5 NIDAA

Hii ni mbinu ambayo hutumika kuonyesha hisia fulani kama vile mshangao, furaha, hasira au kukataa jambo fulani. Alama ya mshangao hutumiwa kuleta hisia iliyokusudiwa.

### 2.6.6 TAKRIRI

Takriri ni mojawapo wa tamathali za usemi ambayo inahusu urudiaji katika lugha. Ingawa urudiaji ni wa aina nyingi sana, baadhi ya urudiaji umepewa majina mengine kama vile usambamba.

Msokile (1992:61) anaeleza kuwa; “Takriri ni urudiaji wa silabi, maneno, mistari au vifungu vinavyolingana katika kazi ya sanaa”. Lengo kuu la msimulizi kurudiarudia maneno au vipengele hivyo ni kulitilia mkazo jambo linaloelezwa.

### 2.6.7 USAMBAMBA

Usambamba ni aina maalum ya urudiaji katika matumizi ya lugha ambapo hupatikana katika kiwango cha kirai, kishazi au sentensi. Kuna aina mbalimbali za usambamba. Miongoni mwa aina hizi ni usambamba wa kimuundo na usambamba wa kisintaksia. Usambamba wa kimuundo ni aina ya urudiaji ambao hujengeka katika urudiaji wa muundo ulio sawa. Urudiaji wa aina hii hupatikana sana katika nyimbo za ngano na katika ushairi wa Kiswahili ambapo muundo sawa wa baadhi ya mishororo hurudiwa katika beti mbalimbali.

Kwa upande mwingine usambamba wa kisintaksia ni aina ya urudiaji katika matumizi ya lugha ambao unahusu uruduaji wa vipengele au vipashio vya kisintaksia katika mfuatano. Vipengee virudiwavyo viwe virai au vishazi, hupatikana katika sehemu ile ile ya sentensi vikiwa vimeandamana. Mifano mingi tumeitoa katika sehemu ya takriri. Mfano mmoja zaidi ni katika kisa cha ‘sungura na cheche’. Sungura anapokasirika na kuondoka akihisi njaa kali baada ya kitoweo chote cha kanga na mayai kuliwa na cheche. Akiondoka na kwenda zake anasema;

*Twende kwetu, twende kwetu tukatafute chakula.*

Hii ni takriri ya kifungu – maneno yanayofuatana ili kusisitiza kuonyesha hisia za hasira alizokuwa nazo sungura baada ya kukikosa chakula.

### 2.6.8 TANAKALI ZA SAUTI

Tanakali ni neno ambalo huiga sauti fulani, jinsi kitu kiangukavyo au kilivyo. Msingi mkuu wa matumizi ya mbinu hii ni kumwezesha msomaji kupata taswira kamili na hisia za mlio wa kitu kinachozungumziwa.

Wamitila (2003) anathibitisha kauli hii kwa kusema kuwa tanakali sauti hutumiwa kurejelea sauti ambayo inaigiza jinsi kitu fulani kiangukavyo, kiliavyo, kilivyo n.k.
Katika uhakiki, wataalamu wanatofautisha kati ya tanakali sauti inayotuletea hisia za mlio wa kitu fulani na tanakali sauti inayotukumbusha maneno yanayohusiana na neno fulani maalum.

## 2.7 TASWIRA

Taswira ni picha ambazo humjia msikilizaji akilini anapoisoma kazi fulani ya kifasihi. Picha hizi hujengwa kwa maelezo fulani. Aidha hujengwa kwa matumizi ya tamathali za usemi kama tashibiha na sitiari. Sababu moja ya kutumia taswira ni kumfanya msomaji aelewe vile mtu au kitu kinavyoonekana na pia kutoa msisitizo fulani.

## 2.8 VILIWAZO

Wamitila (2003) anasema kiliwazo ni sehemu ya hadithi ambayo huwa imekusudiwa kuituliza hadhira kidogo hasa kwenye hadithi zinazozungumzia masuala ya kusikitisha au ya kitanzia. Kiliwazo kinaweza kuwa kifungu kilichojaa ucheshi kilichokusudiwa kuiondoa kwa muda ile hali ya kusikitisha. Nyimbo hutumiwa kama viliwazo.

## 2.9 USIMULIZI

Wamitila (2003) anaeleza kuwa usimulizi ni uelezi wa matukio katika hadithi. Mawazo ya Wamitila ni kama kazi zote za fasihi lazima ziwe na matukio na hayo matukio yanaweza kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia nyingi za usimulizi. Msimulizi hana budi kuchagua mtindo fulani ambao ni wa kufaa zaidi kuwasilisha mawazo yake yatakayomwathiri msikilizaji kwa njia moja au nyingine. Usimulizi unaweza kuwa wa kufululiza matukio moja kwa moja bila ya kutatiza, au unaweza kuwa usimulizi wa kirejeshi na ule wa kiutomaji ambapo msimulizi hukatiza mtiririko au hurejelea mambo yaliyopita (kirejeshi) au aweze kukatiza mtiririko wa hadithi na kuweka vifungu kama vile barua.

Hii aghalabu hutokea katika kazi ya kidrama (kiutomaji). Katika usimulizi wa nafsi ya kwanza, msimulizi anaweza kuwa mshiriki wa matukio au matendo ya hadithi au ashuhudie matendo hayo bila kushiriki. Msimulizi ambaye hashiriki na yuko nje ya hadithi anaweza kueleza hisia na fikra za wengine na matukio yote ya hadithini.

Katika usimulizi nafsi ya kwanza kuna mhusika ambaye anashiriki katika hadithi. Yeye huwa anajielezea tu tajriba zake lakini hana uwezo wa kueleza za mtu mwingine. Msimulizi huyu huweza kujenga uhusiano wa karibu mno kati yake na msomaji. Sisi kama wasikilizaji tunaona anachoona, kusikia anachosikia na kuhisi anachohisi. Anaposimulia, yeye hutumia viwakilishi "mimi" na "ni" vya nafsi ya kwanza. Kwa mfano; katika ngano ya 'cheche na sungura', sungura anasema: 'Mimi sina mke wala sina mama wala mtoto, afadhali tukae pahali pamoja mimi na wewe. Sungura akamwambia cheche 'Mchome kanga huyu na mayai nayo yachome. Mimi nimechoka tik, nitalala kidogo.

Usimulizi wa nafsi ya pili huhusisha viwakilishi vya nafsi ya pili "wewe" na "u". Kulingana na Wamitila (2003) ni kuwa aina hii ya usimulizi ni nadra sana kupatikana katika Kiswahili hata katika lugha nyingine. Mifano michache inaweza kupatikana katika *Dunia yao* na *Dharau ya Ini* ya Wamitila. Matumizi ya nafsi ya pili yanaweza kuwarejelea wahusika wanaopatikana katika ulimwengu huo, au kurejelea ulimwengu wa wasikilizaji ambapo kuna kuvunjwa kwa mpaka uliopo kati ya ulimwengu wa kibunifu na ulimwengu halisi. Mfano "ulishtuka umepaa angani na kutoka kwenye jingo ulimokuwa, ukapaa hadi ukawa mbali sana na dunia, huko juu kabisa…" (Wamitila, *Dharau ya Ini*, uk. 110). Usimulizi wa nafsi ya tatu huwa na matumizi ya 'a' na 'yeye' katika viwakilishi vya nafsi. Ni mtindo ambao hupendelewa sana na wasomi. Hadithi huelezea matukio yanayohusu mtu mwingine. Msimulizi huwa nje ya hadithi akisimulia juu ya mhusika fulani.

Wellek na Warren (1949:105) wanasema kuwa katika tenzi, mtunzi husimulia kisa kama msimulizi wa nafsi ya tatu. Wakati mwingine huwapa nafsi wahusika wake kuzungumza moja kwa moja. Kuna waandishi ambao huchagua kusimulia kisa pasipo kushiriki moja

kwa moja, huwaacha wahusika peke yao na kumruhusu msomaji kuwahakiki bila kumwelewa msimulizi. Usimulizi mwingine humruhusu msikilizaji kumwelewa msimulizi na mitazamo yake kuhusu mambo yanayoikabili jamii.Usimulizi wa matukio huweza kuwa wa nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu. Katika ngano, usimulizi ni muhimu sana kwani huwasilisha ufafanuzi zaidi wa sifa za mandhari, wahusika wake, majukumu yao na matukio yakiwa katika mbinu ya mfululizo au kukatizwa kwa visa. Pia kipengele cha toni hudhihirika katika usimulizi msanii atakaowasilisha.Katika ngano teule za Kiswahili tulizohakiki mtunzi ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu na amefaulu sana katika matumizi ya mbinu hii.

## 2.10 FASILI YA NGANO

Wataalam mbali mbali wametoa maelezo kuhusu maana ya ngano.Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981) "ngano ni hadithi fupi ambazo wazee huwasimulia aghalabu watoto".

Naye Wamitila(2003:40) anaeleza kuwa "ngano ni hadithi za kimapokeo ambazo huwatumia wahusika wa aina mbali mbali wakiwemo wanyama,miti au watu Kusimulia tukio au kisa Fulani chenye mafunzo.Anaendelea kueleza kuwa neno 'ngano' hutumiwa katika jamii zetu kwa maana pana sana kiasi kwamba aina nyingine ya simulizi au hadithi zinaweza kujumlishwa kwenye kundi pana la ngano. Nao Njogu na Chimerah (1999:143) wanaeleza kuwa ngano ni hadithi zinazotoa mifano kadha wa kadha ya maisha ya binadamu na matatizo anayo kumbana nayo ulimwenguni.

M'Ngaruthi (2008) naye anasema kuwa "hadithi ni kisa au matukio halisi au zilizobuniwa .Hadithi hizi za kimapokeo hujulikana kama ngano''.Anaendelea kueleza kuwa,hata hivyo baadhi ya ngano hizi zimebadilika kiasi kwamba zinaposimulima na wasimulizi tofauti husikika kama ngano tofauti.Baadhi ya wasimulizi wataondoa au kuongeza mambo fulani katika hadithi wasimuliapo ama kwa kutaka kuongeza chumvi au kutokana na usahaulifu wa baadhi ya sehemu za hadithi asilia.Bila shaka hii ndiyo huchangia kwa urefu au ufupi wa vitanzu vya hadithi.

Ngure (2007) anasema kuwa :

> *Kuna tamaduni tatu za fasihi kutoka Afrika.*
> *Kwanza ni ule utamaduni wa fasihi simulizi au fasihi ya kutoka kinywani hadi sikioni ambayo huwa inapitishwa kutoka kizazi hadi kingine. Utamaduni huu hujumuisha nyimbo,mashairi,drama,methali, mafumbo,misemo na ndiyo turathi iliyo kongwe na tajiri kuliko zote.Mbali na hayo imejaa uhai na uchangamano hutegemea wakati,mahali na muktadha*

Hapa Ngure anamaanisha kuwa,ngano inavipengelen mbali mbali katika kusitawishwa kwake. Kipengele mojawapo kikiwa ni usimulizi ambao unaonekana kuwa na madaliko kulingana na wakati,kile ambacho Ngure anaita muktadha.Muktadha ikimaaanisha kuwa ngano husimuliwa mahali maalum na wakati maalum. Watoto,vijana na watu wazima katika jamii ya jadi na hata ya sasa walifunzwa utamaduni wao pamoja na uhalisi wa maisha yao kwa njia ya masimulizi katika elimu na nidhamu hii.Jamii nzima ilihusika katika kuwafunza na kuwaelekeza vijana wake.Mambo haya yalitekelezwa kupitia kwa hadithi,nyimbo,methali,vitendawili na tanzu nyingine za fisihi simulizi.

Vile vile inahalisi kuzingatia aina mbali mbali za hadithi za kimapokeo.Hadithi hizi zimegawanywa katika makundi mawili .Kundi la kwanza ni la zile hadithi ambazo hujengwa katika misingi ya ubunifu au kuwaza na kufikiria kisa fulani.Ubunifu huu ni wa kijamii kama tutakavyona hapo baadaye,yaani kisa fulani kinatungwa na kupokezwana.Hizi huitwa hadithi (za mapokeo) za kibunifu.Mifano ni hekaya,hurafa,istiara,mbazi nakadhalika.

Kundi la pili la hadithi ni zile zenye misingi yake katika matukio ya kihistoria,yawe ya kikweli yaliyotendeka au la.Hadithi hizi husimulia mtu aliyeishi,historia ya jamii au kusimulia matukio fulani ya kihalisi.Hizi hujulikana kama hadithi (za mapokeo) za kihistoria mifano yake ni tarihi,kumbuku na kadhalika. Kulingana na utafiti wetu tutajishughulisha zaidi na kundi la kwanza la hadithi, yaani hadithi za mapokeo za kibunifu.

## 2.11 HITIMISHO

Sura hii imehusu uelezaji wa misingi ya kuhakiki fani. Tumejadili dhana ya fani na kuonyesha vipengele vyake muhimu. Pia tumejadili vipengele vya fani ambavyo tunavishughulikia katika sura zinazofuata. Vipengele vyenyewe ni msuko, muundo, wahusika, tamathali za usemi na fasili ya ngano kutoka kwa wataalamu mbali mbali.

# SURA YA TATU

## 3.0 UTANGULIZI

Kufikia hapa tunashughulikia miundo ya ngano mbili za kibunifu, huku msisitizo wetu ukiwa katika msuko,masimulizi na wahusika.Kwa kuchunguza uumbaji wa vipengele hivi, tumejaribu kubainisha kufaulu kwa mtunzi katika kuunda msuko wa ngano na jinsi anavyowasawiri wahusika wake huku akitumia mbinu mbalimbali.Mwelekeo wa uhakiki ndio tunaoendeleza katika sura hii,ambapo tutashughulikia ngano tatu zilizosalia kutoka katika jamii ya Waswahili nchini Kenya katika sura ya nne.

## 3.1 TATHMINI YA NGANO YA BINTI MATLAI

### 3.1.1 MSUKO

Kuhusiana na msuko wa ngano hii ni kwamba matukio yote ya kimsingi yanachangia katika muwala na mtiririko wa ploti na usimulizi kwa jumla. Mfuatano huu hutegemea uhusiano kisababishi. Hizi ni sifa maalumu sana katika utimilifu wa kifasihi wa ngano yoyote ile.

Msuko wa kisa cha Binti Matlai Shamsi ni sahili. Matukio katika kisa hiki yamepangwa katika uhusiano wa kiusababishi. Una urejelezi mwingi wa matukio katika usimulizi. Msimulizi ametumia mbinu ya mgogoro katika viwango viwili. Kwanza nafasi ya mhusika ambaye ni mfalme (baba wa vijana hao) na pili mgogoro wa kiitikadi kati ya nguli kitinda mimba na ndugu zake. Tunachunguza zaidi mgogoro huu wa pili, japo ule wa kwanza ndio uliokuza huu wa pili kwani tamaa ya baba yao ya kumtaka yule ndege ilimletea mgogoro wa kinafsi. Mtoto wa suria anakuwa na mgogoro na ndugu zake kwa sababu ya maswala ya kijamii na kaida ya kijadi kama vile mtoto wa suria hana haki ya kupendwa na kupendelewa kama matendo ya wale ndugu sita kumhusu kitinda mimba huyu yanavyojitokeza. Mgogoro huo unakuzwa na wivu wanaokuwa nao kuwa baba yao anampenda mtoto wa suria kuliko wao ambao ni watoto halali kulingana na mila na itikadi za jamii nyingi za Kiafrika.

Mgogoro huu unajenga taharuki pale ambapo wanataka kumuua mtoto wa suria na wanapompokonya mali na watumwa na kumwacha aende asikokujua. Msikilizaji anashikwa na shauku ya kutaka kujua kutatokea nini hatimaye. Je, kitinda mimba atafia mwituni? Je, atapata wapi chakula? Je, ataweza kuikumbuka njia ya kurudi kwao? Haya ni maswali ambayo yanamhamasisha msikilizaji ili aendelee kusikiliza apate majibu yake. Matumizi mengine ya taharuki ni pale ambapo majitu yanamshika akitaka kumtwaa yule ndege wa ajabu katika tundu.Majitu yanapoamka na kumkuta nyumbani mwao yanamshika na kutaka kumuua. Yanapobishana kuwa yamuue au kumpeleka kwa sultani, tunaingiwa na hamu ya kuendelea kusikiliza ili kujua itakavyokuwa. Mbinu ya taharuki imetumiwa vizuri na imeoana vizuri na matukio tena pale anapoenda kumfanyia dawa na hirizi babake binti Matlai Shamsi. Anafanikiwa kumtorosha binti huyo baada ya kumdanganya mfalme kuwa dawa ya binti yake inafanyiwa bahairini. Mfalme anapogundua kuwa merikebu ya kitinda mimba (mganga kwa wakati huo) haiko baharini anashikwa na hofu na kutoa merikebu zake zimtafute binti yake dunia nzima. Watu wanakuwa na hamu ya kutaka kujua kama binti huyo alipatikana au la. Mbinu ya taharuki imetumika tangu mwanzo hadi mwisho. Msikilizaji hahisi kuwa amelazimishwa.

Sadfa inatokea pale mwishoni ambapo kijana mkubwa anataka kumwoa binti Matlai Shamsi na kitinda mimba wa suria waliyedhania wamemua na kumtupa mtoni anaingia nyumbani kwao, badala ya binti Matlai kuozwa kwa kijana mkubwa, mambo yanapinduka kinyume na arusi kubwa inafanyiwa kitinda mimba na sherehe ya kufana inafanywa. Mtunzi anaweka matukio kiwakati na kilele cha masimulizi kinafikia pale anapofanyiwa sherehe kwa kina binti Matlai Shamsi na mfalme. Msimulizi amejenga matukio katika misingi ya uhalisia wa maisha na kusawiri jinsi wivu na tamaa huleta maafa. Ni kupitia kwa msuko huu ndipo tunapata sifa za wahusika wa ngano hii na mtazamo wao.

### 3.1.2 UCHAMBUZI WA WAHUSIKA KATIKA NGANO YA BINTI MATLAI SHAMSI

Katika sehemu hii, tunachunguza wahusika wanaopatikana katika ngano hii, wana sifa za aina gani, na ni wahusika wepi ambao ni muhimu katika muundo wa ngano na michango yao katika ukuzaji wa usimulizi. Inatubidi kugusia maudhui na ujumbe kwa kiwango fulani kwani ni vigumu kuwazungumzia wahusika na kuweka kando ujumbe walio nao kwa jamii wanayotoka.Lengo kuu la msimulizi wa kisa hiki ni kuonyesha sifa na tabia anazopaswa kuwa nazo binadamu aliyekamilika. Wahusika katika ngano hii wameainishwa katika makundi mawili: wema na wabaya. Wale ambao ni wema huwa ni vielezo ambavyo vinafaa kuigwa na wanadamu.

Mhusika mkuu (nguli) katika ngano na ambaye yumo katika kundi la wahusika wema ni yule ndugu wa saba ambaye ni kitinda mimba wa mfalme. Kupitia mhusika huyu, msimulizi anaashiria msimamo ambao watu wanapaswa kuwa nao katika maswala kama kumcha Mungu, mapenzi kwa wazazi, uvumilivu na bidii, katika kutimiza malengo wanayonuia.

Ndugu wa saba anasawiriwa kama mhusika asiyelipiza uovu kwa uovu, mwenye kuwajali ndugu zake, anayempenda baba yake na anajitolea mhanga kuhakikisha kuwa amemtimizia babake mahitaji ya moyo wake kwa kumletea yule ndege mwenye miguu ya lulu na mabawa ya dhahabu. Ni mwenye bidii, anapitia majaribio mazito lakini anaendelea mbele bila kusita. Sifa nzuri zinapatikana kwa huyu kijana wa saba. Baada ya kumpata yule ndege, binti Matlai Shamsi na ule upanga wa radi, badala ya kuwaachilia mbali wale ndugu zake sita waliomnyang’anya mali yake yote na kutaka kumuua, bado anamwambia yule zimwi ambaye alikuwa rafiki yake kuwa ‘nitakwenda kwa ndugu zangu, nipate kuenda nao pamoja kwa baba’.Hii inaonyesha moyo wa msamaha aliokuwa nao kwa ndugu zake anapowambia ‘basi twendeni sote kwa baba kwa shauri moja na kumwambia ndege tumemkamata pamoja’.

Maelezo haya yanaonyesha moyo suluhu unaompasa binadamu wa kawaida kuwa nao. Kitinda mimba halipizi kisasi kama ambavyo tungetarajia. Wale ndugu sita wamesawiriwa kuonyesha ubaya, tabia na matendo yao hayabadiliki kutokea mwanzo hadi mwisho. Hao wanasimamia wahusika bapa sugu. Wametumiwa kutilia nguvu sifa za kitinda mimba za bidii na upendo. Kwa mfano, wale vijana sita wanapotumwa kuenda kutafuta yule ndege wa ajabu, wanasema kuwa baba yao ni mwendawazimu. Anawaambia wakamtafute ndege ilhali ana mabawa ya kumwezesha kupaa nao hawana mabawa ya kupalia. Ndege anakwenda juu, nao wanakwenda chini, watawezaje kumshika.

Baba wa vijana hawa pia anawakilisha wahusika duara ambao hubadilikabadilika kitabia na matendo. Tunamuona mwanzo akiwa na ubaguzi na upendeleo, vijana wale sita wanapotumiwa kuenda kumtafuta ndege wanapewa farasi mmoja kila mmoja na watumwa mia kila mmoja lakini kitindamimba anaongezewa na pesa juu ya hayo. Pia tunamuona akimkataza kitinda mimba asiende safari hiyo ndefu na ya hatari lakini mwishoni anamkubalia. Pia anawafanyia sherehe kubwa wale vijana sita wanaporudi na ndege aliyemtaka baada ya kuelezewa kuwa kitindamimba hawajui alikoelekea huko mwituni naye anamlaumu kwa kusema ‘potelea mbali, hakushikilia mashauri yangu.’

Ghafla mtoto huyu anapofika nyumbani baada ya kupata fahamu kule mtoni, baba yao anabadilisha nia na kuamua wale vijana sita wafungiwe kwenye mafumba na kutupwa baharini wafie huko.Huko kubadilikabadilika kwake ni njia ya kuonyesha uhalisia wa kijamii. Mhusika kama binti Matlai Shamsi ametumiwa kuonyesha jinsi asasi ya ndoa ilivyo muhimu katika jamii ya Waswahili, na harusi inaweza kufanywa hata mara mbili kuthibitisha furaha na heshima iliyopewa maarusi. Wahusika kama zimwi, sultani na majitu wanatumiwa kujenga hulka ya kitindamimba kwa njia moja au nyingine.Ngano hii ina wahusika wenye sifa ya uchangamano.Sifa hizi ndizo huwakilisha vizuri zaidi uchangamano wa binadamu wa maisha halisi na vilevile uchangamano wa ulimwengu wanamoishi.Msimulizi anafanikiwa katika kuwaumba wahusika kwani ana mhusika bapa kielezo ambaye ni kitinda mimba na wahusika duara ambao ni baba wa vijana saba na zimwi aliyekuwa akimshauri kitinda mimba huko mwituni.Mtunzi amewakuza

wahusika wake hatua kwa hatua huku matukio yakisababishana na kujenga muundo mzima wa ngano hii.Wale ndugu sita wanalipwa kwa maovu yao waliomtendea ndugu yao kwa hivyo wanakufa huku wakijuta kwa yote waliyoyatenda.

### 3.1.2 USIMULIZI KATIKA NGANO YA BINTI MATLAI SHAMSI

Usimulizi kama tulivyokwisha kufafanua katika sura ya pili ni kipengele muhimu cha fani. Ngano ya Binti Matlai Shamsi ina mseto wa kisimulizi. Msimulizi ameanza, masimulizi yake kwa kutumia nafsi ya tatu. Nafsi hii imetumiwa kumrejelea mfalme ambaye pia ni mhusika katika kisa hiki. Nafsi ya tatu umoja huonyeshwa kwa matumizi ya kiwakilishi cha nafsi 'yeye' au kiambishi cha nafsi 'a'. Vivumishi vimilikishi vyenye shina '-ake- 'hutumiwa kuonyesha umiliki katika nafsi ya tatu umoja. Mifano ya vimilikishi na viambishi vya nafsi ya tatu vimetumiwa hivi na mtunzi "aliondokea mtu mmoja mfalme aliyekaa kwa furaha na buraha katika ufalme wake pamoja na watoto wake sita wa mke mmoja na mmoja wa suria wake . Mfalme aliishi na watoto wake saba . Mfalme alikuwa na mazoea ya kuenda kwenye bustani yake kuketi na kubarizi akipunga upepo'.

Nafsi ya tatu humwezesha mtunzi kwa kiwango kikubwa kujitokeza tu kama anayeshuhudia. Hata hivyo, wakati mtunzi mwenyewe anapokuwa ndiye msimulizi pia, huwa hawezi kujitenga na matukio katika masimulizi yake. Mtunzi pia ametumia nafsi ya kwanza umoja katika usimulizi wake. Nafsi ya kwanza umoja huwakilishwa na kiwakiliswa cha nafsi "mimi" pamoja na kiambishi kiwakilishi "ni" katika vitenzi.

Kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja hurejelea mtunzi ambaye pia huchukua nafasi ya msimulizi katika kazi ya fasihi, msimulizi wa aina hii pia huwa mhusika katika kazi husika. Tumeelezewa jinsi kitinda mimba wa mfalme anavyoyasimulia masaibu yake kwa yule zimwi aliyempata mwituni baada ya ndugu zake kumnyang'anya mali yake, watumwa wake pamoja na farasi wake anasema kuwa "mimi sina amri, amri yote ni ya Mungu na mtume wake. Maana Mimi nimetoka kwetu na ndugu zangu sita, mimi wa saba,"

Kitinda mimba ni msimulizi hapa na pia mhusika anajenga uhusiano wa karibu na wasikilizaji wake na kuwafanya waone anachokiona kusikia anachokisikia na kuhisi anachokihisi. Kutokana na masimulizi haya tunapata kuona kuwa kitinda mimba ni mwenye bidii, mwenye mapenzi kwa baba yake na kielezo chema kwa ndugu zake kwa kuwa na moyo wa msamaha kwa ndugu zake.

Nafsi ya pili pia imetumika katika ngano hii kukiwa na viwakilishi vya nafsi “wewe”na “u”, msimulizi anarejelea nafsi ya pili anapoelezea jinsi kitinda mimba wa mfalme anapomwambia Binti Matlai Shamsi kuwa **–** “huku kwetu na wewe usitie hofu, inshallah utarejea kwenu kama ulivyokuwa kwanza “. Maelezo hayo yalitolewa na kitinda mimba kumwondolea hofu ya kuwa hatarini Binti Matlai Shamsi. Hapa anayerejelewa kama nafsi ya pili ni Binti Mtalai, nafsi ya pili pia inatumiwa kama njia ya kuhusisha hadhira katika masimulizi.

## 3.2 KISA CHA CHECHE NA SUNGURA

### 3.2.1 TATHMINI YA MSUKO WA NGANO

Katika ngano hii, msuko unaojitokeza wazi ni msuko sahili ambapo matukio hutiririka kuanzia mwanzo hadi mwisho. Matukio yamefuatana kiwakati na kiusababishi, hakuna urejelezi wa nyuma katika kisa hiki. Ngano hii ina matukio ambayo yameoana vizuri na yanayofuata mkondo madhubuti. Matukio yote muhimu yana wiano na wahusika waliomo kwenye usimulizi.

Msimulizi amefanikiwa katika kujenga mgogoro pale ambapo cheche anamla kanga wote na mayai kisha anamdanganya sungura kuwa labda kanga kateketezwa na moto. Taharuki inajitokeza pale ambapo cheche ana maka baada ya kupata pigo kuwa hangekila kile kitoweo alichoshinda akikitafuta. Wasikilizaji hawajui hatua itakayochukuliwa na sungura. Taharuki pia inajitokeza pale ambapo cheche anafungwa na majani ya mgomba na kupigwa sana. Wasikilizaji hawajui kitakachotendeka baadaye, basi wanakuwa na shauku ya kusikiliza zaidi ili kufikia matokeo hayo. Hii ni mbinu iliyotumiwa vizuri sana na msimulizi. Ngano hii imepata muala unaojitokeza wazi wazi kwa jumla.

Kilele cha usimulizi kinafikia pale cheche anapomualika sungura kwa ngoma nyumbani kwao alasiri ile. Vita vinaanza baada ya wote wawili kukebehiana. Cheche anapandwa na mori baada ya kutambua kuwa aliyemfunga na kumpiga alikuwa ni rafiki yake ambaye ni sungura. Ujumbe unaowasilishwa na msimulizi ni kuwa ubinafsi hujenga uadui na pia ahadi ni deni kama alivyokwisha ahidi Cheche kuwa 'Tunachopata tule sote na siku tusipopata tumshukuru Mungu.' Cheche hakuweza kuweka ahadi hiyo, na ndiyo iliyowaletea vita kati yao. Jambo jingine kuhusu muundo wa masimulizi ya cheche na sungura ambalo ni muhimu kutaja ni kwamba, mwandishi ametumia mbinu ya kuipa ngano mielekeo mipya kwa njia ya ghafla isiyotarajiwa na msomaji. Hivi ni kusema kwamba mara kwa mara matukio fulani yanaanza matukio mengine ambayo yanamshangaza msikilizaji. Kwa mfano, katika zile harakati za cheche kumkebehi sungura akipiga zumari kuwa kanga amemla wote na kusingizia moto, ghafla sungura anachukua ngoma kubwa na kumkebehi cheche pia jinsi alivyomfunga na kumpiga. Haya yote hayakutarajiwa kutendeka kwa wakati mmoja. Matukio ya ghafla kama haya yanaondoa uwezekano wa kumchosha msikilizaji. Iwapo mbinu kama hii haikutumiwa kama ipasavyo msikilizaji hangeweza kutabiri kila tukio na ngano ingekosa uwezo wa kusisimua na kuvutia.

Ngano yenyewe ni fupi ukilinganisha na ile ya Binti Matlai Shamsi iliyotangulia. Kwa hivyo haimchoshi msikilizaji na kumwacha na hamu kuwa ingeendelea. Aidha, imesimuliwa kwa njia ya kusisimua kwa matumizi ya upangaji bora wa msuko, na mbinu kadha wa kadha za kisanaa.

### 3.2.2 USAWIRI WA WAHUSIKA

Msimulizi amewaumba wahusika wake akiwa na lengo la kuonyesha athari za ubinafsi katika jamii. Aidha, tukumbuke ya kuwa aghalabu uumbaji wa wahusika hutegemea maudhui na ujumbe. Vipengele vyote hivi vinaathiriana. Kutokana na maudhui ya ubinafsi msimulizi ana msawiri cheche kama mhusika anayejipenda na kutowajali wenzake. Mwanzo anajifanya kuwa mhusika anayewajibika zaidi anapomkaribisha sungura ili waishi pamoja kwa kuwa wana matatizo yanayofanana. Anamwambia sungura:"….. Mimi sina mke wala sina mama wala mtoto, na wewe kama mimi tu, huna

mke, huna mtoto, afadhali tukae pahali pamoja mimi na wewe, tunapopata tule na siku tusipopata tumshukuru Mungu. Naye sungura akasema; ‘vyema, tayib! Mashauri yako mema. Wakakaa mahali pamoja”.Mambo yalibadilika baadaye na ule wema na huruma aliojitia Cheche uliondolewa na uroho na ubinafsi aliokuwa nao baada ya kitoweo cha kanga kutoa harufu nzuri iliomvutia. Wema ulibadilika na kuwa uovu ulioleta vita baina yao. Urafiki uliisha na uadui kuingia sungura alipogundua kuwa kanga kaliwa na mayai pia na cheche. Cheche ni mhusika duara, anabadilikabadilika, mara ni mzuri na kisha anabadilika na kuwa mbaya ilimradi ajinufaishe. Tabia hii ya Cheche ni kiwakilishi cha tabia ya binadamu wengi katika jamii ambao hujifanya kuwa wema kwa wenzao huku wakiwa na malengo yao ya kibinafsi na mara tu malengo hayo yanapokamilika, huwa hawana shughuli au haja nao tena.

Sungura pia kama mhusika duara amesawiriwa kuonyesha hisi alizonazo binadamu za kulipiza kisasi. Hakuweza kumsamehe Cheche kwa kosa la makusudi la kumla kanga na mayai yake huku akisingizia moto kumteketeza kanga. Sungura anachukua hatua ya kumfunga Cheche kwa majani ya mgomba na kumpiga sawa sawa na kama kipigo hicho hakikutosha, vita viliendelezwa tena ngomani baada ya cheche kumkebehi. Matendo hayo yanaonyesha hali halisi katika jamii wanamoishi binadamu. Tabia za kulipiza kisasi ni mambo ya kawaida. Kwa hivyo katika muundo wa ngano hii, msimulizi anaeleza maudhui zaidi kupitia kwa wahusika hawa. Ametumia mbinu kama uendelezaji wa matokeo kighafla ili kuifanya ngano kusisimua na mbinu zinginezo. Kwa hivyo amefaulu katika kuwaumba wahusika wake. Msimulizi pia alitaka kuwaonyesha wasikilizaji kuwa “ Mjinga akierevuka, mwerevu huwa mashakani”. Kila mara sungura husawiriwa kama mwerevu na mjanja kumbe siku zote si Jumapili.

### 3.2.3 USIMULIZI KATIKA NGANO YA CHECHE NA SUNGURA

Katika ngano hii, msimulizi anatumia mbinu ya usimulizi wa nafsi ya kwanza umoja kama nilivyokwisha kueleza katika masimulizi ya hapo mbeleni, usimulizi wa nafsi ya kwanza umoja huwakilishwa na kiwakilishi “mimi” pamoja na kiambishi “ni”. Msimulizi anatumia mbinu hii kuelezea mazungumzo kati ya Sungura ya Cheche baada ya sungura kumtega kanga na kumleta nyumbani kama kitoweo pamoja na mayai yake.

Sungura anamwambia Cheche, “Mchome kanga huyu na mayai nayo pia yachome. Mimi nimechoka tik! Nitalala kidogo”. Sungura anakuwa msimulizi na wakati huo huo yeye ni mhusika anayewezesha matukio kwenda mbele, Cheche pia anaichukua nafasi hii ya kuwa msimulizi wa nafsi ya kwanza umoja anaposema “vyema na mimi nitakwenda” anajirejelea wakati ambapo sungura amekasirika baada ya kanga kuliwa na Cheche, sungura anapanga njama ya kulipiza kisasi.

Wasimulizi na wahusika hawa wawili wanasimulia tajriba zao ili kujenga uhusiano wa karibu na hadhira yao. Katika hali hii msikilizaji anakuwa katika nafasi nzuri kuelewa tabia, sifa na mitazamo ya wasimulizi. Kwa mfano, kutokana na masimulizi haya tunapata kufahamu kuwa cheche ni mlafi na anajipenda, hajali maslahi ya wenzake, japo mwanzoni anamhadaa sungura kuwa aje waishi pamoja wanachopata wale pamoja na siku wasipopata wanashukuru Mungu. Hii ilikuwa hila tu. Sungura naye anatumia ujanja wake kulipiza kisasi.

### 3.3 KISA CHA SUNGURA NA SIMBA

#### 3.3.1 TATHMINI YA MSUKO WA NGANO

Masimulizi ya ngano yanayoshughulikiwa yanatokana na tukio la sungura kuona mzinga na kuitamani asali yenyewe huku akijua wazi kuwa asali hiyo ni ya simba. Tukio hilo ni kama shina ambamo matukio yote mengine yanatokezea. Hivi ni kusema kwamba hakuna tukio muhimu lisiloweza kuhusishwa, kwa njia moja au nyingine na tukio hilo la kimsingi. Mbinu hii imeipa ngano hii mwelekeo ambapo msikilizaji hatatiziki kuitafuta hadithi na kuioanisha na matukio yake. Hali hii inaleta uwiano na muundo bora wa msuko kama asemavyo Laurence (1959: 142) anasema kuwa:

> *Mwandishi bora hufanya uteuzi, haingizi chochote katika hadithi ambacho hakiendelezi dhamira kuu ya hadithi, lakini hapaswi kuteua tu lazima pia apange. Matukio yanapaswa kupangiliwa kwa njia itakayoleta taathira zaidi.*

Katika ngano iliyooanishwa vizuri, kila tukio linachipuka kutokana na lile ambalo lilitangulia. Kwa maoni yetu, msuko wa ngano ya sungura na simba umetimiza kanuni hizo hapo juu.

Hapa na pale mtunzi ametumia mbinu rejeshi ili kuupa msuko uchangamano na ruwaza nzuri. Kwa upande wa maudhui, tunapata picha ya ukatili, dharau na ukora unavyotumiwa na watu ili kujinufaisha. Sungura anadanganya panya buku kuwa asali ni ya babake, tamaa ya kupenda kula bila kupeleleza kwa undani inamtumbukiza katika hatari ya kuupoteza uhai wake. Kobe anatumia uerevu wake na kujinasua kutoka mkono katili wa simba.Taharuki inajengeka pale ambapo wasomaji wanataka kujua yatakayompata sungura endapo simba atamkamata baada ya kutoroka. Tunapata taswira ya simba alivyo mnyama mkali na jasiri lakini anashindwa na wanyama wadogo kama sungura na kobe. Taswira za mazingira katika ngano zinachangia kuleta uyakinifu na pia kuashiria mazingira ambamo matukio yanazuka. Sifa hizi zinainua kiwango cha utimilifu wa kisanaa katika ngano inayohusika. Maelezo haya hapa chini yanathibitisha tusemayo.

Siku moja aliondoka sungura kuenda kutafuta chakula msituni na kuuona mbuyu mkubwa sana. Alipoyatupa macho yake juu aliuona mzinga mkubwa sana wa asali ya nyuki. ...... walipofika hapo huku wamebeba mienge kama kawaida wakapanda juu. Waliwachoma nyuki, wakakimbia, sungura na kobe wakakaa kitako na kuanza kula asali.

Taswira za mazingira kama hizi hazitoshelezi mahitaji ya kisanaa tu bali pia zina umuhimu mkubwa kimaudhui. Kifungu tulichoelezea hapo juu kinaelezea kilele cha urinaji wa asali na shughuli zote zinatekelezwa wakati wa kurina asali. Tunaelezewa uhondo waliokuwa nao sungura na kobe. “ walikaa kitako”, elewa walikuwa juu ya mbuyu. Kutokana na hayo, tunaweza kusema kuwa mtunzi alifaulu sana kutumia kipengele cha mazingira ili kurutubisha muundo wa ngano.

### 3.3.2 USAWIRI WA WAHUSIKA

Sifa alizopewa sungura katika ngano hii ni ujanja na udanganyifu. Msimulizi anaeleza sifa hizi na zinajitokeza waziwazi anavyowadanganya panya buku na kobe kuwa asali na mzinga ni wa baba yake. Wanapokamatwa na simba, bado sungura anaendelea na udanganyifu pamoja na ujanja na kumwambia simba kuwa nyama yake ni ngumu na hailiki bila ya kutwangwa kwa mchi. Simba anayeaminika kuwa na nguvu na makini anahadaiwa na sungura baada ya kuingia nyumbani kwa sungura na kutaka kumvizia ili amkamate na kumla. Sungura anapoisalimia nyumba yake, jambo lisilo kawaida, simba anasalitika kuitikia salamu. Jambo hilo lilimfanya alikose windo lake.

Kobe naye huwa na mwendo wa polepole uliojaa makini. Anausalimisha uhai wake kwa kumwambia simba alisugue gamba lake kwa mkono ili aifikie nyama yake, badala yake, mkono wa simba unachubuka.Sungura ni mhusika bapa sugu ambaye habadiliki toka mwanzo hadi mwisho.Matendo yake ni yale yale ya udanganyifu na ujanja tangu mwanzo hadi mwisho.Sifa hizi za sungura zinaangazia tabia za watu katika jamii ambao hujipatia riziki zao za kila siku kwa njia za udanganyifu na ujanja kama kufungua afisi za bandia na kusajili watu huku wakiwatoza viwango fulani vya fedha kuwa wangewapatia wafadhili kutoka nchi za ng'ambo.Baada ya muda fulani afisi hizo hufungwa na hakuna awezaye kugundua waliko.

Panya buku naye anasawiriwa kama mhusika asiye na akili ya kuchanganua ni lipi linalofaa kutendwa. Anafanya mambo bila kuyachunguza kwa makini kwanza na wala hajishugulishi kutambua athari zake.Hataki kujua mwenye mzinga wa asali, yeye anaongozwa na tamaa na ulafi.Pia ni mwepesi wa kudanganyika.Sungura anapomwambia amtie ndani ya mwenge na kumwambia simba ajitenge autupe mwenge chini, hashuku kuwa sungura atakimbia na kumwacha katika hatari ya kuliwa na simba na ndivyo ilivyofanyika.Lakini kobe anapoambiwa na sungura maneno yaya haya, anang'amua ujanja wa sungura wa kumwacha mashakani. Kwa hivyo baada ya kumtia sungura kwenye mwenge anamwambia Simba kuwa, "sungura huyo anakuja" simba anamdaka akamkamata mkononi.

Ni vyema kuitambua hatari kabla ya kukufikia ukajitahadharisha mapema au ukapanga jinsi ya kujinusuru.Simba ni mwakilishi wa watu wanaojiona kuwa shupavu na wenye nguvu,lakini wasipoyapanga mambo yao vizuri, huweza kushindwa na mambo madogo madogo wasiyodhania kuwa yangewashinda.Simba anashindwa kuumudu mradi wake wa ufugaji nyuki kwa hivyo wanaofaidika nao ni akina sungura kobe na panya buku. ili kutatua tatizo hili la wizi wa asali, simba angestahili kuajiri walinzi wa mchana na usiku. Mtunzi anawakuza wahusika hivi kwamba kila mhusika ana jukumu lake katika kuwakilisha ujumbe. Kwa maoni yetu, kutokana na matendo ya wahusika hao, hakuna hata mmoja mwenye tabia inayostahili kuigwa.

### 3.3.3 USIMULIZI WA NGANO YA SUNGURA NA SIMBA

Ngano ya sungura na simba ina mseto wa mbinu za kisimulizi. Kuna mchanganyiko wa vitambulishi vya nafsi ya kwanza umoja, nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili umoja na nafsi ya tatu umoja.

Kama nilivyokwisha kueleza hapo mbeleni, kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja ni “mimi” na kiambishi kiwakilishi “ni” katika vitenzi. Msimulizi anatumia viwakilishi hivi katika mazungumzo miongoini mwa sungura, panya buku na kobe kwa wakati tofauti. Simba anapomkamata panya buku baada ya sungura kukimbia anamuuliza, ‘mlikuwa na nani huko juu?’ buku anajibu, ‘mimi na sungura.’ Kwa mara nyingine simba anawapata sungura na kobe wakiwa mtini wakila asali. Sungura anamwaambia kobe, ‘nitwae mimi unitie ndani ya mwenge nami nitakwenda nikungoje chini?’ naye kobe anasema, ‘mimi nitasema umeniambia ni asali yako, kumbe si yako ni ya mwenyewe simba. Katika nafsi hii, wanyama wote hawa ni wasimulizi na pia wahusika katika ngano hii, kutokana na masimulizi haya tunapata kufahamu sifa za sungura za ujanja na udanganyifu kwa wanyama wote hata wale wanaogopwa na wanyama wengine kama simba anayejulikana kama mfalme wa mwitu.

Nafsi ya kwanza wingi pia imetumiwa na msimulizi. Nafsi ya kwanza wingi hujumuisha msimulizi pamoja na watu wengine kama wahusika katika kazi ya kifasihi. Nafsi ya kwanza wingi imetumiwa katika ngano hii pale ambapo sungura anawaita wenzake waje

naye wapate kuila asali hiyo, anawaita panya buku kisha baadaye anamwita kobe pia. Baada ya kuwachoma nyuki kwa mienge ya moto walianza kuila asali iliyokuweko kwenye mzinga. Baada ya simba kumkimbiza sungura na kuchoka, akawaambia watu ‘sungura amenishinda basi simtaki tena’. Pia anaihusisha hadhira pana kwa kuwauliza iliko nyumba ya sungura ili akalipize kisasi.

Nafsi ya kwanza wingi hujumuisha msimulizi pamoja na watu wengine kama wahusika katika kazi ya kifasihi. Matumizi ya nafsi ya kwanza wingi yamempa fursa msimulizi kuwahusisha wengine kama wahusika. Vile vile wahusika hawa wanaweza kuchukuliwa kama hadhira simulizi. Hivyo msimulizi anatumia mbinu hii kuhusisha hadhira yake katika masimulizi.

Nafsi ya pili pia imetumika katika ngano hii. Mfano ni pale simba anapomkamata panya buku baada ya sungura kukimbia na kutoroka. Panya buku anaulizwa na simba, ‘ulikuwa wewe na nani huko juu?’ Panya buku anapojitetea asiliwe na simba anasema, ‘ukinila nyama yangu ngumu, nikamate mkia unizungushe kisha unipige na mchi, basi utanila nyama yangu itakuwa laini na nzuri’

Nafsi ya pili pia inatumika pale simba anaposikia sauti juu ya mti wenye mzinga na kuuliza, ‘nani nyinyi?’ naye kobe akaitikia, ‘sisi hapa!’ sawa na nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili inatumiwa kama njia ya kuhusisha hadhira katika masimulizi. Hali kadhalika nafsi ya tatu imetumika katika masimulizi haya. Tunapata mfano wa nafsi ya tatu umoja ambayo inawakilishwa na ‘a’ na ‘yeye’ Pamoja na vihusishi vimilikishi vyenye shina ‘-

ake-’ pale ambapo kobe anajisemea kimoyomoyo kuwa, ‘huyu ataka kukimbia, kuniacha mimi niliwe na simba ataliwa yeye mbele.’ akamwambia simba, ‘sungura huyo anakuja’ mfano mwingine ni pale sungura alipoziona nyayo za simba zikiingia nyumbani kwake. Msimulizi anasema, ‘akaja yeye na mkewe, akamwambia mke wake rudi wewe, simba anapita hapa ananifuata mimi. Rudi wewe mtoto wa watu. Sungura akaona nyayo za simba zimeingia kwa nyumba yake.’

Matumizi ya nafsi ya tatu inapendelewa sana na watunzi wengi wa kisimulizi kwani karibu ngano hizi zote zina usimulizi wa nafsi ya tatu. Kwa kutumia mtindo huu, wasimulizi wa ngano hii wamefaulu kusawiri sifa mbalimbali za wahusika wake kama ubinafsi, ujanja na ukarimu wa bandia unaoletwa na sungura kwa rafiki zake kama kobe na panya buku.

## 3.4 HITIMISHO

Katika sehemu hii tumeshughulikia utathmini wa msuko wa ngano tatu za kibunifu huku tukiwasawiri wahusika katika ngano hizi. Mbinu za usimulizi na nafsi zilizotumiwa na mtunzi zimeelezwa kwa kina. Pia tumeshughulikia toni iliyotumiwa na msimulizi katika ngano hizi.Vipengele hivi vimevipa ngano hizi mvuto na mshikamano wa kipekee katika miundo yao

# SURA YA NNE

## 4.0 UENDELEZI WA UCHANGANUZI WA NGANO

### 4.1 UTANGULIZI

Katika sura ya tatu tumechanganua ngano tatu za Kiswahili kutoka jamii ya Waswahili. Tumeangalia jinsi vipengele vya fani kama msuko, wahusika na nafsi mbali mbali zinavyohusishwa katika usimulizi ili kuipa ngano mvuto na umbo linalopendeza. Katika sura ya nne tunaendelea na uchanganuzi wa ngano mbili zilizosalia tukiwa na mtazamo ulio sawa na wa sura ya tatu.

### 4.2 KISA CHA NDOVU NA BINADAMU

#### 4.2.1 TATHMINI YA MSUKO WA NGANO

Kwanza inabidi tueleze kuwa hii ni ngano ya kiistiari ambapo wahusika waliotumiwa ni vivuli vya matukio yaliyotendeka kweli.Matukio katika ngano hii yanachangia katika muala na mtiririko wa ploti kwa jumla.Mtunzi anaifikiria na kuipanga kazi yake kwa makini  kama inavyomjuzu mwanasaa bora.

Mtunzi anatumia mbinu ya mgogoro katika sehemu mbili.Kwanza, pale ambapo ndovu anakubaliwa kuingiza mkonga wake tu lakini anajilazimisha kuingiza mwili wake wote na kumfukuzilia binadamu nje ya kibanda chake.Pili, mgogoro unazuka tena wakati kamati inapoundwa ya kutatua matatizo kati ya ndovu na binadamu kisha wanakamati wanaoteuliwa wanakuwa ni wa upande wa ndovu na wanamnyima binadamu nafasi ya kutoa malalamishi yake. Pia wanakata kauli na kumwambia watu wake hawana elimu ya sheria. Tunachunguza zaidi kiwango cha kwanza cha mgogoro kwa sababu ndicho kinachobeba kile cha pili. Katika jamii hii kuna ukandamizaji na unyanyasaji mwingi. Tunamwona binadamu anavyodhulumiwa kwa sababu ya ubaguzi wa kikabila na ulaji rushwa. Ndovu anatengeneza mlo safi ambao unatumika kama hongo kwa wanakamati. Baada ya mlo huo, binadamu hapewi ruhusa ya kujitetea ila kesi inakatwa dhidi yake.

Uchangamano katika msuko na mvuto wa ngano kwa msikilizaji umejengwa kwa matumizi ya mbinu ya taharuki.Tunapata matumizi ya mbinu hii kwa mfano pale ambapo binadamu anapongojea matokeo ya malalamishi ya kutoka kwa kamati iliyoteuliwa na mfalme wa pori (simba). Msikilizaji anaingiwa na shauku ya kutaka kujua kutatokea nini hatimaye. Je, wanakamati watamchukulia hatua gani ndovu kwa kuuingiza mwili wake wote katika kibanda cha binadamu na kumfukuzia nje bila idhini yake? Je, binadamu ataendelea kwenye mvua endapo ndovu atakatalia ndani? Haya ni maswali ambayo yanamhamasisha msikilizaji kuendelea kusikiliza ili apate majibu yake. Matumizi mangine ya taharuki ni pale binadamu anapotumia mafumbo akisema “hakuna mnyama atembeae ardhini asiyeweza kutegwa”. Msikilizaji anabaki akiwa na hamu ya kujua hatua nyingine itakayochukuliwa na binadamu baada ya kujua kuwa hana mtetezi yeyote kwa upande wake.

Kilele cha masimulizi haya yanafikia pale ambapo binadamu anahamia mbali na kukijenga kibanda kikubwa na kizuri kuliko vile vya mwanzo.Kama ilivyokuwa tabia na kawaida ya wanyama hao wanakuja kila mmoja akidhania kuwa ndiye anayekwenda kukiwahi.Mtunzi anatupa taswira ya jinsi wanyama hao walivyopakimbilia anaeleza kuwa, “mara tu bw. Kifaru alipoliona akabumburuka kuelekea huko alikomkuta ndovu tayari anatabaradi,kalala yu burudani kabisa! Bw. Chui alifuatia dirishani, bw. simba ,bw.mbweha na bw. Mbogo wakajitoma mlangoni wakati bwana fisi analialia akisaka nafasi ilhali bw. Ngwena naye alijitandaza paani”. Muda si muda walianza kubishana kuhusu haki za kuwako.Tunaelezwa na msimulizi kuwa katika hali ya mvutano kuwa ndipo mwenye banda hilo alipolitia moto na kuwateketeza wote mle ndani.

Katika muktadha mpana, istiara hii inaweza kupewa fasiri ya mahusiano ya bara la Afrika na nchi za Ulaya ambapo nchi hizi zililigawa bara la Afrika huku kila moja ikijenga himaya yake katika bara hili. Waingereza walizitawala zaidi ya nchi moja, Wajerumani vivyo hivyo na koloni nyinginezo.

Kutokana na ngano tuliyoisimulia ni kuwa, huko pwani ya Afrika Mashariki mfumo wa kijamii-kiuchumi wa kikabaila ulikuwa umefika kiwango cha juu sana hata kabla ya kuwasili kwa Wareno.

Mulokozi (1983:40) anasema kuwa: Tabaka na harakati za kitabaka zilikuwako kitambo hata kabla ya kuwasili kwa Wareno na ushahidi wa jambo hili unapatikana katika maandishi ya karne ya kumi hadi ya kumi na nne ya Waraabu. Aidha,

> ‘Utenzi wa Liyongo ambao unasemekana kuwa ulitungwa katika karne ya kumi na mbili ni ushahidi kuwa hata wakati huo matabaka yalianza kuibuka katika jamii ya Waswahili.Tabaka la mabwanyenye ndilo lililodhibiti utamaduni na uwezo wa kisiasa huko pwani hadi karne ya kumi na tisa’.

Kila kunapokuwa na tabaka vilevile sawia kunakuweko na harakati za kitabaka.Harakati za kitabaka pia hudhihirika katika fasihi kwani fasihi kama njia ya kuwasilisha itikadi ya tabaka fulani ni silaha ya kuwaunga mkono wanaonyonywa ama kuwaunga wanyonyaji.Kwa maneno mengine tunaweza kusema kwamba, katika jamii ya mfumo wa kikabila,makabila huwa na fasihi yao wenyewe yenye lengo la kuimarisha na kudumisha ukabila.Haya yanathibitishwa na kumnyanyasa binadamu anayewakilisha watawaliwa watwana ambao walitawaliwa kwa ujeuri na bila huruma na mabwanyenye kuwanyang’anya ardhi yao na hoteli kubwa kubwa zikajengwa humo na mashamba yao kunyakuliwa huku wakifanywa kuwa maskuota katika ardhi yao ya jadi.

Kwa upande wao, mabwanyenye hawa na fasihi yao ya kupinga ukabila na kuwasilisha itikadi ya kupambana dhidi ya makabila wanaofurahia maisha kutoka kwa jasho la wanyonge. Hivi ndivyo ilivyokuwa katika pwani ya Afrika Mashariki. Waafrika walijua kuwa ‘Amani haipatikani ila kwa ncha ya upanga,’ ndipo msimulizi anamalizia kwa kusema: ‘Amani ni ghali, lakini inahalisi kugharamikiwa.’

### 4.2.2 USAWIRI WA WAHUSIKA

Katika uainishaji wa wahusika tumekwisha elezea kuwa huwa katika makundi mawili-yaani wema na wabaya.Tunaweza kusema kuwa wahusika katika ngano hii wameainishwa kitabaka. Kuna tabaka la mabwanyenye na tabaka la mafukara. Tabaka la mabwanyenye linawakilishwa na simba (mfalme wa pori), ndovu mmoja wa mawaziri katika dola ya simba, bw. Mbogo, bw. Chui, bw. Fisi, bw. Ngwena, bw. Mbweha, bw. Kifaru na wanyama wengine wa pori.Tabaka la mafukara liliwakilishwa na binadamu.

Tunamwona binadamu akiwa karimu na kumwonea huruma ndovu akinyeshewa na mvua na tufani kali huko nje. Anapokubaliwa kuuingiza mkonga wake anamtimua binadamu na kumwacha anyeshewe na mvua. Badala ya ndovu kumlipa kwa wema aliyomtendea, anaamua kumlipa kwa maovu. Maisha na hali anayoishi binadamu katika kibanda kidogo kilichobomoka inadhihirisha hali yake ya ufukara.Na kama hilo halikutosha mabwanyenye wanaendelea kung'ang'ania vibanda vyake kila anapojenga upya. Mulokozi (khj:30) anasema:

> *'Katika hali ya kitabaka, tabaka lililokuwa likitawala liliandika mashairi ya wosia ambayo yalikuwa na lengo la kushawishi na kushauri tabaka lililokuwa likitawaliwa kukubali hali ya serikali ya ukabila wa kiislamu. Kwa upande mwingine tabaka la watwana lilitoa maoni yao kupitia fasihi simulizi'.*

Mifano ya mashairi hayo ni kama utendi wa Mwanakupona na utenzi wa Inkishafi. Ukabila unatumia dini kama chombo cha kuwafanya wanyonge wakubali hali yao na wavumilie kuendelea kutumikia makabila. Haya yanathibitishwa na simba katika ngano hii anapomjulisha binadamu kuwa wale wanakamati walikuwa wameteuliwa na Mungu kuzilinda haki za makabila na jamii zote zisizokuwa na meno makali wala makucha marefu. 'Meno makali na makucha marefu' yametumiwa kimafumbo kuonyesha ukatili wa dhuluma walizokuwa nazo makabila hayo kwa wanyonge. Katika mfumo wa kitabaka dini hutumikia tabaka linalotawala kwa kuhubiri kuwa Mungu ndiye aliyeumba matajiri na maskini na kuwa kila mtu sharti akubali hali yake. Inkishafi ni ushairi wenye maudhui mazito na kwa sababu hii mtunzi (Sayyid Abdallah bin Ali bin Nassir) alifaulu

kutumia maneno kisanaa hata akafanikiwa kuhubiri itikadi hii ya kukatisha tama. Mwisho tumeona kuwa katika jamii ya kitabaka huwa ama inatumikia wanaotoa jasho ama inatumikia wanaokula bila kutoa jasho. Zile kamati zinazoundwa na simba (wakoloni) nia yao sio kumsaidia mwafrika bali ni kuhalalisha matakwa ya mabepari. Mabepari hao hawajali maslahi ya Waafrika (binadamu) katika ngano.

Ule mlo murwa unaoandaliwa na ndovu ni jazanda ya kuwa tume na kamati mbalimbali zinazochaguliwa kushughulikia maswala na kesi humu nchini, hutoa uamuzi kulingana na kiasi cha hongo anachoweza kutoa mdhulumu. Kwa hivyo mdhulumu hupata haki pale asipostahili, ndiposa wahenga walisema ‘mnyonge hana haki mpaka mwenye nguvu apende’. Hatimaye binadamu anafaulu kuwakomboa watu wake toka unyanyasaji hadi uhuru wao. Tukitamatisha sehemu hii ni kwamba tunaweza kulinganisha mifumo hii kijamii, kitaifa na kiulimwengu.

### 4.2.3 USIMULIZI KATIKA NGANO YA NDOVU NA BINADAMU

Kuna mseto wa nafsi uliotumika katika usimulizi wa ngano hii. Kuna nafsi ya kwanza umoja, nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili, nafsi ya pili umoja na nafsi ya tatu umoja na wingi .

Msimulizi ametumia vitambulishi vya nafsi ya kwanza umoja kama nilivyokwisha eleza hapo awali. Katika majadiliano kati ya ndovu na binadamu, ndovu anataka binadamu amruhusu kuuingiza mwili wake wote ndani ya kibanda. Ndovu anasema hivi, ‘Rafiki yangu mwema , ngozi yako ni ngumu kuliko yangu, unaweza kuhimili kipigo cha mvua. Mimi naikinga ngozi yangu huku ndani isipigwe na vua hilo kubwa’. Msimulizi hapa japo si mhusika katika ngano hii lakini anajenga uhusiano wa karibu na hadhira yake na kuipa hadhira yake taswira ya yaliyotendeka.

Hali kadhalika nafsi ya kwanza wingi imetumika kwingi katika masimulizi haya. Msimulizi anasimulia kuwa “ndovu aliitikia amri ya mkuu wake kwa kushirikiana na wanyama wengine kuiteua kamati ya uchunguzi” Tunaelezwa kuwa walioteuliwa walikuwa waheshimiwa na waliosifika kwa kutopendelea kwao na kupenda haki.

Walikuwa wameteuliwa na Mungu kuzilinda haki za makabila na jamii zote zisizokuwa na meno makali wala makucha marefu.

Masimulizi ya nafsi ya kwanza wingi yamempa fursa msimulizi kuwahusisha wengine kama wahusika. Vile vile wahusika hawa wanaweza kuchukuliwa kama hadhira simulizi. Hivyo msimulizi anatumia mbinu hii kuhusisha hadhira yake katika masimulizi. Vile vile mbinu hii imemsaidia kuendeleza maudhui ya ukabila, ugandamizaji, upendeleo na ulaji rushwa katika ngano hii. Haya tutayapata kwenye viambatisho.

Nafsi ya pili pia imetumika katika ngano hii. Msimulizi anarejelea nafsi ya pili pale ambapo fisi pamoja na wakuu wengine wa porini wanaalikwa na ile kamati iliyoteuliwa na simba kutatua malumbano yaliyokuwa kati ya ndovu na binadamu. Fisi na wakuu wa pori walimuunga ndovu mkono, huku yule binadamu akikatizwa kauli asiweze kuelezea masaibu yake. Ile kamati iliyoteuliwa na simba ndiyo nafsi ya pili. Nafsi ya pili pia inatumiwa na msimulizi pale ambapo simba anasifu tabia ya binadamu ya kukubali kumsetiri ndovu wakati wa mvua. Simba anamwambia binadamu kuwa "umefanya vizuri kuwa na urafiki na watu wangu hasa ndovu, ambaye ni mmoja wa mawaziri wakuu kwenye dola yangu. "Nafasi hiyo inatwaliwa ili kukufaidi wewe, madhali mwenyewe hujafikia kiwango cha kuweza kuitumia ipasavyo. Sawa na nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili inatumiwa kama njia ya kuhusisha hadhira katika masimulizi.

Nafsi ya tatu pia imetumiwa na msimulizi. Msimulizi anajitokeza hapa kama anayeshuhudia matukio bila ya yeye kuwa mhusika katika usimulizi huu. Hata hivyo mtunzi mwenyewe anapokuwa msimulizi vile vile, huwa hawezi kujitenga na matukio katika masimulizi yake.

Msimulizi anatupa mfano wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika usimulizi wake. Tunaelezewa kuwa ili simba aweze kuituliza ile hofu aliyokuwa nayo binadamu ya kunyang'anywa kibanda na pia watu wake kutoteuliwa katika ile kamati ya utatuzi, simba alimwahidi uamuzi wa haki.

Yule jamaa alifurahia ghaya baada ya kuyasikia maneno haya matamu ya mfalme wa pori. Aliamua kusubiri kwa hamu kuu nafasi hiyo, aliamini kuwa kile kibanda kitarudishwa kwenye umiliki wake .

Nafsi ya tatu wingi imetumika kuelezea walioisikia sauti ya malalamishi kutoka kwa binadamu, " wanyama waliokuwa kwenye msitu uliokuwa hapo karibu walisikia sauti yake ya kulalamika. Wote walitua na kukaa tutwe kuyasikiliza mazungumzo ya mvutano yaliyokuwako kati ya jamaa na rafiki yake ndovu. Kwa ujumla mbinu hii husaidia katika kuwasilisha maudhui ya aina mbalimabli.

## 4.3 MIGANI YA FUMO LIYONGO

### 4.3.1 TATHMINI YA MSUKO WA NGANO

Kuhusiana na msuko wa ngano hii ni kwamba matukio yote ya kimsingi kama yalivyopangwa katika sehemu iliyotangulia, yana sababu maalum – yanachangia katika muala na mtiririko wa msuko na ngano kwa jumla.Msanii ameipanga kazi yake kwa makini kama inavyomjuzu mwanasanaa bora.

Mbinu ya mgogoro imetumiwa na msanii katika viwango viwili. Kwanza nafsi ya nguli yaani Fumo Liyongo yuko katika mgongano na kaida fulani za kijamii kwamba mtoto wa suria hana haki ya kirithi ufalme licha ya umri wake. Pili, Fumo Liyongo yuko katika mgogoro na ndugu yake Daudi Mringwari ambaye anamwonea wivu Fumo Liyongo kwa sababu alikuwa na nguvu nyingi, alipendwa na wengi na kwa hivyo angeipindua serikali yake. Tunachunguza zaidi kiwango cha kwanza cha mgogoro kwa sababu ndicho kinachobeba kile cha pili.Jamii alimoishi Fumo Liyongo haikuwathamini watoto wa masuria.

Tunaelezewa kuwa:

> *"…Fumo Liyongo alikuwa mtoto wa mfalme lakini mamake alikuwa suria kwa hivyo Fumo Liyongo hakuhesabiwa kama mtoto halisi wa mfalme. Mfalme alipoaga dunia, Fumo Liyongo hakumrithi licha ya umri wake."*

Tunaelezewa pia kuwa kulizuka mvutano mkubwa kati ya Fumo Liyongo na ndugu yake anayejulikana kama Daudi Mringwari. Mvutano huu ulileta na mambo ya urithi na wivu.

Maelezo hayo yanatupa picha ya jamii ya Waswahili jinsi ambavyo watoto wa masuria walivyoteseka.Hali hii ya jamii kuwatweza watoto hawa ndiyo Fumo Liyongo anaipinga tangu mwanzo hadi mwisho wa masimulizi. Kuthibitisha hili ni kwamba hata msichana aliyeozwa na Wagalla alikuwa na mtoto wa kiume aliyempata kutokana na ndoa yake ya mbeleni lakini Liyongo alimpenda na kumtunza kijana huyu kama mwanawe wa kumzaa. Tunaona hapo kwamba msanii ametumia mbinu ya kumpa nguli sifa za utu-hasa kutojali mila na utamaduni mbaya wa kutowathamini watoto wa masuria kama Waswahili walivyofanya, ili apinge kaida mbovu katika jamii. Hivyo basi mgogoro baina ya Fumo Liyongo na jamii yake unastawisha maudhui na kuendeleza masimulizi.

Mvutano uliokuwako kati ya Liyongo na Daudi Mringwari unaufanya msuko wa hadithi kuwa changamano na wenye mvuto kwa matumizi mengi ya mbinu ya taharuki. Tunapata matumizi ya mbinu hizi pale ambapo Liyongo anatoroka Pate na kuhamia bara alikoishi na Wasanye. Na si hayo tu kila mara mfalme anapanga njama za kumuua Liyongo akatumia watu mbalimbali na hatimaye anafanikiwa kumuua akimtumia kijana wa Fumo Liyongo anayefanikiwa kumuua babake kutumia sindano ya shaba. Hiki ndicho kilele cha masimulizi haya. Taharuki ya mwisho ni kuwa je, huyu kijana ataozwa binti mfalme na kupewa ufalme kama alivyoahidiwa na Mringwari? Msikilizaji anashikwa na shauku ya kujua kutatokea nini hatimaye. Mbinu ya taharuki imetumiwa vizuri na kuoana na mtiririko wa matukio.Mbinu rejeshi pia imetumiwa na msanii kutueleza maisha ya Liyongo ya utotoni na kuzaliwa kwake pamoja na jamii iliyomkuza.

Msanii ametumia maelezo kutupa picha ya jinsi Liyongo alivyotoka gerezani na kuikata ile minyororo na zile pingu. Alitoka nje kwa kishindo kikubwa na kuvigonganisha vile vichwa vya maaskari.Kisha anapodungwa kitovu kwa sindano ya shaba pia Liyongo 'aliamka kwa kishindo kikubwa,alitoa ukelele mzito wa uchungu…..' katika vishindo hivi viwili, cha kwanza ni cha ushindi au mafanikio ya kuwa huru kutoka katika utumwa na cha pili ni cha kushindwa au kuangushwa kwa shujaa. Hapo msanii ametumia mealezo ili kuupa msuko uchangamano na ruwaza nzuri inayompatia msikilizaji picha ya matukio haya.Mbinu ya taswira ya mazingira pia imetumiwa na msanii kwa mfano pale Wasanye wanapokwenda na Liyongo mwituni kutunda makoma, Wasanye wanauchagua mkoma ulio mrefu kushinda yote, wanasema: "huu hapa tumeupata!" Liyongo alipoangalia aliona ni mrefu mno akaijua nia yao. Mbinu hii pia inapatikana pale Liyongo anapodungwa sindano kitovuni, tunaelezewa hivi:

> *Fumo Liyongo aliamka kwa kishindo kikubwa, alitoa*
> *ukelele mzito wa uchungu ambao ulisikika Shaka nzima*
> *na inadaiwa kuwa hata leo mwangwi wa sauti ya kilio*
> *hicho husikika usiku hasa majira ya mvua kuu.*
> *Fumo Liyongo alitimua mbio kuelekea palipokuwa*
> *na kisima cha maji cha mjini na kupiga magoti huku*
> *ametia mshale wake kwenye uta wake. Watu*
> *walishindwa kwenda kwa kuogopa kuwa alikuwa*
> *amekasirika, alipoguswa na mamake alianguka mfu.*

Kifungu kilichonukliwa hapa kinaashiria kilele cha maisha ya shujaa huyu kwa jamii yake. Mshale na uta na kupiga magoti kama anayefuma ni ishara ya ulinzi na mapambano dhidi ya mila na imani zilizopitwa na wakati katika jamii. Fumo Liyongo alikuwa mtetezi wa haki ya wanaogandamizwa.

Msanii anamalizia kwa masimulizi ya kitanzia ya kifo cha Liyongo na cha kijana wake anayeingiwa na uchungu kwa kusalitika na kumuua babake kisha naye anatorokea msituni na kufia huko. Msanii anaafikiwa katika kuujenga muundo wa ngano kwa

kutumia mbinu mbalimbali zikiwemo mafumbo, nyimbo na mashairi katika kuwasilisha ujumbe.

### 4.3.2 USAWIRI WA WAHUSIKA

Wahusika waliotumika katika migani hii wana tabia changamano. Wanaweza kuainishwa katika makundi mawili wema na wabaya. Wale ambao ni wema huwa ni vielelezo ambavyo vinafaa kuigwa na wanadamu.

Mhusika mkuu katika mighani hii ni Fumo Liyongo. Mhusika huyu anaainishwa katika kundi la wahusika wema.Wahusika hawa pia tunaweza kuwaainisha kitabaka. Tabaka la watawala na tabaka la watawaliwa. Fumo Liyongo ndiye mhusika aliyekuzwa kikamilifu na matukio yote yaliyo muhimu. Tunamwona Liyongo tangu utotoni hadi anapofikia kifo chake. Msimulizi anamkuza mhusika huyo hatua kwa hatua, akieleza kila kipindi cha maisha yake. Tangu mwanzo tunaona maisha ya Liyongo yana dosari ambayo inaweza kuangaliwa kama taashira ya dhiki zinazomkumba maishani. Dosari hii ni kwamba yeye ni mtoto wa suria. Dhiki zinazomkumba Liyongo ambazo zinaelezwa katika sehemu ya msuko zinamfanya mwakilishi wa tabaka la wanyonge katika jamii ya kitabaka. Msanii amemsawiri Liyongo akiwa na lengo la kuonyesha namna ambayo mazingira ya kijamii ambapo hakuna usawa wa kiutawala na katika uongozi, yanaweza kumdunisha mwanadamu na kumwangamiza utu wake. Mfano wa taathira za mazingira hayo kwa Liyongo, ni pale ambapo baba yao ameaga dunia naye Liyongo akijua ya kuwa ndiye atakayekuwa mrithi wa ufalme ule kwa sababu ya umri wake. Nakuwa mfalme alikuwa baba yake mzazi. Anabaguliwa kuwa yeye ni mtoto wa suria. Kitendo hiki kinaleta mvutano kati yake na nduguye. Mringwari. Kwa hivyo Liyongo ananyimwa haki ya urithi na Daudi Mringwari ambaye alikuwa mdogo kwa umri.

Tunamwona Daudi Mringwari akitumia mamlaka yake ya uongozi vibaya kwa kumfuatilia Liyongo hatua kwa hatua ili kumteketeza. Anawatumia Wagala na Wasanye kumnasa na kumuangamiza Liyongo kwa kutumia hila mbalimbali. Yeye (Daudi Mringwari) anawakilisha mhusika bapa sugu kama anavyoelezea sifa za mhusika huyu Wamitila (2003). Mhusika huyu habadiliki tangu mwanzo hadi mwisho. Matendo yake

ni yaleyale. Mringwari hana msamaha kwa ndugu yake hata Liyongo anapotoroka na kuenda mbali naye, bado huwatuma wajumbe wake kumfuata akiwa huko ili kumwangamiza. Hatimaye anatimiza dhamira yake ya kumzimisha Liyongo kwa kumtumia mtoto wa Liyongo kumdunga babake kwa sindano ya shaba kitovuni. Tabia ya Daudi Mringwari ni taashira ya unyanyasaji kwa wanyonge unaotumiwa na baadhi ya viongozi ili kuwazimisha wapinzani wao. Kwa ujumla, Liyongo ni mhusika aliyetiwa uchangano mwingi na ni mhusika ambaye anawakilisha mwanadamu katika jamii ambaye anajaribu kuitetea haki yake lakini haipati kwani wahenga husema "mwenye nguvu mpishe". Kwa hakika Liyongo ni mhusika duara.

Mamake Liyongo ni mhusika bapa-kielezo ana tabia nzuri ya huruma na mapenzi kwa mwanaye. Ni mvumilivu na mwenye bidii. Hachoki kuioka mikate ya kumpelekea mwanawe anapokuwa gerezani. Kila Saada anapoipeleka gerezani inachukuliwa na kuliwa na wale walinzi lakini mama mtu hachoki. Mapenzi hayo ya mama kwa mwanae pia yanadhihirika pale Liyongo anapokufa huku amepiga magoti kando ya kisima. Mamake anatafutwa ili aende akaongee naye, 'mamake Liyongo alimwendea huku akimwimbia tumbuizo nzuri za kuliwaza'. Alipomgusa na akaanguka ndipo walipogundua kuwa alikuwa amekufa. Tunaelezwa kuwa huzuni kubwa iliwashika watu wote. Haya yanaonyesha mapenzi waliyokuwa nayo Waswahili kwa Fumo Liyongo. Alikuwa 'mtu wa watu'.

Kijakazi Saada pia ni kielelezo kizuri kwa watumishi wa nyumbani. Fumo Liyongo anapomtuma kwa mamake kwa njia ya mafumbo kwa kutumia shairi:

> 'Wee kijakazi nakutuma utumike kamwambie mama sijaerevuka
> afanye mkate, katikati aweka tupa nikate pingu na minyororo
> ikifunguka niingie njiani, niteleze kama nyoka nipande madari
> na kuta nikitazama huko na huku'.

Saada anatii na kuufikisha ujumbe ule kwa mamake Liyongo kisha yaliyobidi yanatendwa, na Liyongo anafanikiwa kutoroka kutoka gerezani.

Wale askari wanaonyesha ulafi na ukatili walionao walinzi wa magereza yetu. Hawana utu wala huruma kwa wafungwa. Matendo kama hayo ya kuwanyang'anya wafungwa vyakula walivyoletewa havikuwepo wakati ule wa Liyongo tu, bali vingali vinaendelea hata leo. Katika kumalizia sehemu hii ni muhimu tusisitize kwamba migani hii ina muundo thabiti unaounda pamoja vipengele vyote.

### 4.3.3 USIMULIZI KATIKA MIGHANI YA FUMO LIYONGO

Msimulizi wa mighani hii si mmoja wa wahusika katika usimulizi. Yeye anaelezea matukio bila ya kujihusisa nayo. Yeye anachukua nafsi ya mtunzi. Nafsi ya pili imetumika katika usimulizi huu pale ambapo mfalme Mringwari anapowatumia wagalla kwenda kumhadaa Fumo Liyongo.

Nafsi ya kwanza wingi imetumika pale ambapo Liyongo anakubali kushirikiana na Wasanye katika kikoa cha kutunda na kula makoma. Fumo Liyongo aliwaambia wauchague makoma, Wasanye walimwambia Liyongo, "huu hapa tumeupata mkoma mrefu"

Nafsi ya tatu imetumika kwingi katika mighani hii kuwarejelea Fumo Liyongo na mfalme Mringwari kama wahusika wakuu lakini kwa kutoa maelezo yao kwa wakati tofauti. Katika hali ya kukumbusha tu ni kuwa, nafsi ya tatu umoja huonyeshwa kwa matumizi ya kiwakilishi cha nafsi "yeye" au kiambishi cha nafsi "a" pamoja na vivumishi vimilikishi vyenye shina "-ake-" hutumiwa kuonyesha umiliki katika nafsi ya tatu umoja kama anavyosema Wamitila (2008) mtindo huu wa kutumia vimilikishi umetumiwa kuonyesha sifa zinazosimuliwa na mtunzi. Vimilikishi hivi ni kama anavyojaribu kuonyesha tofauti iliyokuwa kati ya Wagalla na Fumo Liyongo kimaumbile Anasema hivi, 'licha ya urefu wao huo waliweza kumfika Fumo Liyongo kwenye magoti ya miguu yake ya ajabu'

Pia tunaelezewa mbinu alizotumia kutungua makoma. 'badala ya kuupanda ule mkoma, alitia mishale yake kwenye uta wake na kutungua ngaa nzima ya makoma wakala wakashiba'

Nafsi ya tatu wingi pia imetumiwa na msimulizi. Msimulizi anatuelezea uamuzi waliokuwa nao Wasanye baada ya kushindwa na werevu wa Fumo Liyongo. Mtunzi anatueleza kuwa, 'Wasanye walishindwa na la kufanya. Walimwendea mfalme na kumweleza kuwa haikuwa rahisi kupambana na Fumo Liyongo.

Kimsingi nafsi ya tatu humwezesha mtunzi kwa kiwango kikubwa kujitokeza tu kama anayeshuhudia. Hata hivyo msimulizi huyu pia anajitokeza kama mtafiti msimulizi kutokana na maelezo yake juu ya madai ya watu wengine kuhusu miaka aliyoishi hadi kifo chake na mahali alikozaliwa 'baadhi ya maelezo yanaeleza kuwa Fumo Liyongo alizaliwa Siu ilhali mengine yanasema kuwa alizaliwa sehemu inayojulikana kama Shaka.' Kwa kutumia mtindo huu msimulizi wa mighani amefaulu kusawiri sifa mbalimbali za kimaumbile za Fumo Liyongo.

Mbinu hii ni muhimu kwani inawasawiri wahusika, ambacho ni kipengele cha fani. Mbinu hii pia imemsaidia mtunzi kuwasilisha maudhui ya mapenzi ya maana kwa mwanaye, usaliti kati ya ndugu na wivu miongoni mwa ndugu, utiifu kama aliyodhihirisha kijakazi Saada miongoni mwa mengine.

## 4.4 HITIMISHO

Katika sura hii tumechunguza msuko, wahusika na usimulizi katika ngano ya kisitiari na ya kihistoria kutoka kwa jamii ya Waswahili. Tumebainisha kuwa watunzi wamefaulu katika kutumia vipengele hivi vya fani ili kuzipa ngano hizi mvuto unaostahili katika kazi yoyote ya kifasihi. Kutokana na uchambuzi wetu, tunafikia uamuzi kwamba msanii anatumia vizuri vipengele hivyo na kufanikiwa katika kuunda muundo wa kazi hizo. Kwa kutumia msuko/ploti iliyochangamano na sahili, masimulizi ya kusisimua, taswira thabiti za mazingira na uumbaji wa wahusika wa aina mbalimbali msanii anafaulu kutunga kazi iliyo na muundo mzuri kwa kutumia vipengele mbalimbali vya fani.

# SURA YA TANO

# UKIUSHI WA KISEMANTIKI KATIKA NGANO TANO ZA KISWAHILI

## 5.0 UTANGULIZI

Semantiki ni tawi la isimu ambalo hujishughulisha na uchambuzi wa lugha katika kiwango cha maana. Sura hii inashughulikia namna mtunzi amekiuka matumizi ya lugha ya kawaida ili kuleta maana mbalimbali katika kazi yake. Tunajadili matumizi ya semi, tamathali za usemi kama tashihisi, chuku, na mbinu zingine za lugha kama usimulizi, viliwazo na taswira. Mbinu hizi za lugha zinahusiana na semantiki kwa sababu zinabeba maana mbalimbali katika muktadha zinamotumiwa na pia zinajenga muundo wa kazi hiyo.

## 5.1 SEMI

Misemo ni matumizi ya maneno ya kawaida kinjozi kwa njia isiyokuwa ya kawaida. Misemo huhitaji mtu kufikiria kwanza ndiposa afichue maana ya maneno husika. Misemo mingi hubuniwa na jamii. Misemo katika jamii moja hutofautiana na jamii nyingine. Hii ni kwa sababu baadhi ya misemo hutungwa kutokana na mazingira pamoja na itikadi za jamii. Misemo hutumika kwa lengo la kusitiri maana na pia kumfanya msomaji kutafakari ujumbe uliopo.

Wamitila K. (2003) anakubaliana na kauli kwa kueleza kuwa semi ni neno lenye upana ambalo hutumiwa kuelezea matamko fulani yanayoelezea ukweli fulani. Aidha, semi ni kauli za maneno kadha yenye maana iliyofichika.

Katika ngano zilizokusanywa na kuhaririwa na Wamitila kutoka jamii ya Waswahili watunzi wametumia semi mbalimbali katika ngano hizo kuelezea hali fulani zinazowakumba wahusika. Kwa mfano katika ngano ya 'Binti Matlai Shamsi' wametumia usemi 'Kubarizi akipunga upepo'. Msemo huu unaonyesha hali ya starehe aliyokuwa nayo mfalme wa nchi ile. Kila jioni tunaelezewa alivyozoea kuingia bustanini mwake na kuketi humo. Pia tunaelezewa kuwa 'alikaa kwa furaha na buraha,'

katika ufalme wake. Alikuwa na watoto wa kiume sita wa mke mmoja na mmoja wa suria wake. Hali hii inaonyesha kuwa mfalme huyu alikuwa na starehe nyingi na mali mengi ambayo alikwisha tengeneza, kwa hivyo lililobaki ilikuwa ni kustarehe na kula. Msemo mwingine uliotumiwa katika kisa kiki hiki ni ‘alipotupa macho.’ Hapa ni pale kitinda mimba wa suria alipokwisha nusurika kifo kutoka kwa ndugu zake, baada ya kutembea msitu na nyika kwa muda wa usiku nzima, alichoka na alipokuwa akipumzika chini ya mti na kupatwa na usingizi alisikia kishindo kikubwa kwenye sehemu ya mwitu na alipoangalia kando akaona zimwi kubwa sana likija.

Katika ngano ya <u>cheche na sungura</u> mtunzi ametumia semi ‘usiahi mkali sana’ kumaanisha kelele kubwa. Msemo huu unadhihirisha kilio cha uchungu aliokuwa nacho Cheche kutokana na kipigo hicho kama lipizo la kisasi baada ya yeye (Cheche) kumla kanga wote na mayai yake.

Katika ngano ya <u>sungura na simba</u>.kuna matumizi ya msemo baba ‘ameaga dunia.’ Msemo huu unarejelea kifo cha babake sungura ambaye anadai kuwa alimuachia mzinga wa asali uliokuwa juu ya mbuyu. Anawaalika panya buku na kobe ili waende wakaile ile asali ambayo kwa hakika haikuwa ya sungura bali ilikuwa ya simba. Sungura na kobe wanapopanda mbuyuni ‘wanakaa kitako’ kumaanisha kuwa walikuwa wamekaa chini kwa starehe bila ya wasi wasi wowote.

Simba anasema “amenitenda leo, sungura aliyeyaanzisha haya.” Msemo huu unaonyesha uchungu aliokuwa nao simba baada ya kuusugua mgongo wa kobe kwa mkono wake mpaka ukatoa damu baada ya kuchubuka. Kobe alimdanganya kuwa kama angelisugua gamba lake angekuwa laini na simba angeweza kumla kwa urahisi. Hili liliposhindikana simba ‘akashika njia’ kwenda kumtafuta sungura aliyesababisha shida hiyo ya simba. Msemo huu unaonyesha kuwa aliondoka na kwenda zake.

Katika ngano ya <u>ndovu na binadamu</u> mtunzi anaelezea namna binadamu alivyofurahi baada ya simba mfalme wa porini alivyomuahidi usalama na uamuzi wa haki kutoka kwa ile kamati iliyoteuliwa. Anasema kuwa ‘yule jamaa alifurahi ghaya’ baada ya

kuyasikia maneno hayo matamu. Hali hiyo inaonyesha furaha isiyokuwa na kifani, haielezeki kwa maneno ya kawaida. Msemo alikuja kwa ‘mbwembwe na kiburi’ umetumiwa na mtunzi kuonyesha maringo na majivuno aliyokuwa nayo ndovu ili kuleta suluhu kati yake na binadamu. Majivuno hayo  na kiburi kile yalionyeshwa na ndovu kwa sababu alijua kuwa yeye ndiye atakayeshinda kesi kwani ile kamati ilikuwa na upendeleo pia alikwisha wapa hongo ya chakula kizuri.

Binadamu anapoitwa na ile kamati ili ajitetee, anaharakishwa na kuambiwa, ‘jamaa, tafadhali usituvungevunge hapa yaeleze yaliyo muhimu tu!’ Msemo huu unamaanisha kuwa asidanganye au asiseme maneno yasiyo ya kweli. Anakatiwa kauli kabla ya kutoa maelezo yake yote. Hali hii inaonyesha upendeleo kwa wenye uwezo kimali na unyanyasaji kwa wanyonge wasio na watetezi wao.

## 5.2 TAMATHALI ZA USEMI

Tamathali za usemi hujulikana pia kama lugha ya kitamathali. Tamathali za usemi ni mojawapo wa dhana kongwe zaidi katika fasihi za ulimwengu. Dhana hii imetumika katika uhakiki wa fasihi tangu enzi za nadharia ya balagha ya zamani. Dhana hii imeelezwa na kuainishwa na wataalamu mbalimbali wa fasihi katika makamusi na pia vitabu vya kinadharia. Japo wataalamu wengi wa fasihi ya Kiswahili wameishughulikia dhana hii, uainishaji wake ambao ni wa wazi zaidi umefanywa na Kuhenga (1977), Wamitila (2008), Mbatiah (2001), Holman na Harmon (1986). Wataalamu hawa wanakubaliana kuwa tamathali za usemi ni dhana ya kifasihi ambayo hutumiwa kuelezea aina ya ukiushi wa kimaksudi katika matumizi ya lugha ya kawaida au iliyozoeleka.

Wanaelezea kuwa ukiushi huu unaweza kuwa katika viwango vya maana (semantiki) na mpangilio wa maneno (sintaksia) ili kuleta maana mpya au msisitizo. Kwa hivyo, tamathali ya usemi ni fungu la maneno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine.

Tamathali ya usemi huwa ni mbinu ya kupimia usemi wa mtunzi. Ubunifu lazima ujitokeze katika matumizi ya tamathali mbalimbali za usemi. Pia tamathali za usemi huvutia wasikilizaji na kuwapa hamu ya kutaka kusoma zaidi. Huwafanya wasikilizaji kutafakari kuhusu wanayoyasikia na kulinganisha na mazingira na mandhari yao. Ni vyema tufahamu ya kwamba, tamathali za usemi nyingi huwa na mpaka mdogo sana kati yazo. Msikilizaji anastahili kuwa na uelewa wa kina ili aweze kupata ujumbe ulionuiwa na mtunzi.

Tamathali za usemi ni nyingi mno. Zile zinazochukua nafasi muhimu katika kazi za kifasihi na hasa ngano ni pamoja na sitiari, tashbihi, kinaya, chuku, tafsida, tabaini, maswali ya balagha, nidaa, usambamba, tashihisi na taashira. Kwa kuwa tamathali hizi ni nyingi, hututaweza kuzijadili zote. Tumejadili tu zile ambazo zimetufaa katika utafiti huu.

### 5.2.1 TASHBIHI

Tashbihi ni mbinu ya mlinganisho wa vitu viwili au zaidi vyenye hulka tofauti kama vile sitiari. Hata hivyo tofauti na sitiari, tashbihi hutumia viungo vya ulinganishaji.

Msokile M (1992) anafafanua kuwa aina hii ya tamathali hutumia ulinganisho wa mambo ama vitu kwa kutumia viunganishi ‘ja’, ‘mithili ya’, ‘mfano wa’, ‘sawa na’ na ‘kama’. Mtunzi hutumia ulinganishi huu kusisitiza sifa fulani na pia kujenga picha ya aina fulani akilini ambayo athari yake ni ya kudumu zaidi.

Katika ngano ya ‘Binti Mtlai Shamsi’ yule kijana kitindamimba alipokutana na zimwi kule mwituni, alipewa masharti ya kuwa asipompa yule zimwi chakula masufuria arobaini ataliwa yeye. Ndiposa yule zimwi anamwambia yule kijana kuwa:

> *Damu yako itakuwa kama maji ya kusukutua kinywa changu.*

Hapa mwandishi anatuchorea picha ya uchache wa damu ya yule kijana ukilinganishwa na umbo kubwa la lile zimwi, kwa hivyo damu ya yule kijana haingeweza kuivunja kiu ya zimwi ila tu kusukutulia na kuishia kinywani bila hata kufika tumboni mwake.

Katika kisa hicho hicho tunaelezewa jinsi zimwi lile lilivyomwambia yule kijana achukue mti na kuuchonga kama upanga na kumpelekea Sultani badala ya kumpelekea upanga wa radi ili apewe yule ndege wa ajabu. Inaonekana kuwa upanga huu baada ya kupakwa rangi, tofauti haingeonekana kati yake na ule wa asilia- upanga wa radi uliokuwa na thamani kwa Sultani.

Katika mighani ya 'Fumo Liyongo', Liyongo anamtuma Kijakazi Saada kwa mamake kwa njia ya fumbo katika shairi akisema:

> *Ningie ondoni ninyepee ja mwana nyoka*
> *Ningie mwituni ningurume ja simba buka.*

Mtunzi anafananisha kutambaa kwa Fumo Liyongo kutoka gerezani kama nyoka atumiavyo tumbo lake bila miguu na kulinganisha ile sauti atakayoitoa Fumo Liyongo afikapo mwituni na mgurumo wa simba. Mtunzi anatupa picha ya wanyama hao wawili nyoka na simba. Pia ni katika hali ya kusisitiza uzito wa sauti aliyonayo simba na nguvu alizonazo Fumo Liyongo.

### 5.2.2 CHUKU

Chuku pia hujulikana kama udamisi. Ni mbinu inayotumika kueleza hali ya kukipa kitu, mtu au hali sifa kupita kiasi. Matumizi ya mbinu hii hudhamiriwa kusisitiza sifa hiyo ya ukubwa au udogo. Kauli zinazotumika katika mbinu hii huwa ni za kutiliwa chumvi ili kusisitiza na pia kuchekesha. Kwa kutumia chuku, sifa za kawaida za kitu kinachohusika hukiukwa. Kitu hicho huweza kudunishwa au kukuzwa. Katika Kiswahili chuku hujulikana kama kutia chumvi.

Katika migani ya 'Fumo Liyongo' mbinu hii imekolezwa sana, tunaelezwa kuhusu umbo la Fumo Liyongo hivi.

> *Wagalla walikuwa warefu sana, lakini walishangaa kutokana na ukubwa wa Fumo Liyongo. Licha ya urefu wao huo waliweza kumfika Fumo Liyongo kwenye magoti ya miguu yake ya ajabu.*

Katika dondoo hili, mtunzi anapigia chuku umbile la Fumo Liyongo.

Anapoalikwa na Wasanye kwenye kikoa cha kutunda makoma, badala ya kuupanda ule mkoma alitia mishale yake kwenye uta wake na kutungua ngaa nzima ya makoma wote wakala wakashiba. Hali hii imetiliwa chuku zaidi kuonyesha Liyongo alivyokuwa mlenga shabaha makini.

Katika migani hiyo hiyo tunaelezwa, kuwa alipodungwa sindano ya shaba kitovuni na mtoto wake, Liyongo aliamka kwa kishindo kikubwa. Alitoa ukelele mzito wa uchungu ambao ulisikika shaka nzima na inadaiwa hata leo mwangwi wa sauti ya kilio hicho husikika usiku hasa majira ya mvua. Chuku imetiliwa kitendo cha kutoa "ukulele mzito uliosikika shaka nzima". Hiyo inaonyesha nguvu nyingi alizokuwa nazo shujaa huyo.

Katika kisa cha Binti Matlai Shamsi, tunaelezwa jinsi zimwi alikula vyakula masufuria arubaini. Si jambo la kawaida, kwa hivyo mbinu ya chuku imetumiwa kuelezea maajabu hayo.

**5.2.3 TASHIHISI**

Wales (2001:349) anafasili tashihisi kuwa; 'Ni tamathali ya usemi ambapo kitu kisicho na uhai, mnyama, kisicho binadamu au chenye sifa za kidhahania kinapewa sifa za binadamu.'

Tamathali hii hutumiwa kuleta mvuto wa kisanaa na athari fulani za kihisia. Katika ngano ya 'Binti Matlai', tunaelezewa kuhusu mshituko alioupata mfalme baada ya kudanganywa na yule kijana kitinda mimba kuwa alikuwa mganga na alienda kumfanyia madawa binti Matlai akiwa baharini. Mfalme alipotoka nje na kupata kuwa ile merikebu ya mganga haikuwepo, alikata shauri hivi;

> *Akaziambia merikebu zake zote ziende dunia nzima kumtafuta binti huyo. Merikebu zikaondoka zikaenda zikatafuta hata zikachoka zikarudi bila ya kumwona*

Merikebu zimepewa sifa za binadamu. Tunafahamu fika kuwa merikebu haina miguu wala macho kuonea kitu. Ikiwa merikebu imetembea na kumtafuta binti huyo dunia nzima, basi zinapewa sifa za binadamu. Katika ngano tulizoteua, kwingi wanyama wametumiwa kama wahusika na kwa hivyo wamehuishwa kwa njia mbalimbali kama katika masimulizi na matendo yao.

### 5.2.4 DHIHAKA/KINAYA

Wamitila (2003) kuihusu tamathali hii, anasema kwamba msemaji au mwandishi hutumia usemi unaoficha hisia zake kumhusu mtu au kuihusu hali fulani. Kimsingi, pana kinaya fulani katika maneno yaliyotumiwa. Sababu kuu ya kutumia dhihaka ni kumcheka na kumkera mtu.

Mfano mzuri wa dhihaka unapatikana katika kisa "Cheche na Sungura". Cheche baada ya kumla kanga na mayai yake anamwalika sungura kwao kwa ngoma ili kumkasirisha sungura anachukua zumari na kuipiga 'kanga pia singizia moto, ti! ti! ti!' kumaanisha kanga nilimla wote. Sungura alipokerwa na maneno hayo, naye akachukua ngoma kubwa na kuipiga 'nikamtwa nikamfungafunga na majani ya mgomba nikampiga pu! pu! pu!' Hii inaonyesha dhihaka waliokuwa nayo kati yao.

### 5.2.5 TAKRIRI

Takriri ni mojawapo wa tamathali za usemi ambayo inahusu urudiaji katika lugha. Ingawa urudiaji ni wa aina nyingi sana, baadhi ya urudiaji umepewa majina mengine kama vile usambamba.

Msokile (1992:61) anaeleza kuwa; "Takriri ni urudiaji wa silabi, maneno, mistari au vifungu vinavyolingana katika kazi ya sanaa". Lengo kuu la msimulizi kurudiarudia maneno au vipengele hivyo ni kulitilia mkazo jambo linaloelezwa. Kwa mfano katika kisa cha 'Binti Matlai', kitindamimba akiielezea hali yake kwa mfalme (baba yao) anapokatazwa asiende hiyo safari ya hatari. Lakini anamwambia babake kuwa, "hali yangu ni kama ya wenzangu, niki<u>pata</u> sawa, nisipo<u>pata</u> basi". Kuna urudiaji wa neno pata. Hii ni takriri ya neno.

Tunaelezwa kuwa Binti Matlai alipoona kuwa yule kitinda mimba ameuawa na wale ndugu zake, tunaambiwa kuwa;

--- *Akakataa kula, kunywa wala kusema.*

Katika dondoo hilo kuna takriri silabi ‘ku’ ya kurejelea hali ya binti huyo. Lengo la msimulizi hapa ni kusisitiza kitendo cha kukataa kutenda.

Katika ngano ya ‘Binti Matlai Shamsi’, yule kijana aliyenyang’anywa mali na watumwa na nduguze alishika njia msitu na nyika, msitu na nyika kwa mwendo wa siku mbili kwa miguu.

Hii ni takriri kifungu. Katika ngano ya ‘Sungura na Simba’ sungura anasalimu nyumba yake akisema;

*Salaamu nyumba! Salaamu nyumba! salaamu nyumba!*

Hii ni takriri kifungu kusisitiza majibu aliyoyatarajia sungura kutoka kwa simba ili ajiandae kutoroka zaidi endapo simba alikuwa ndani.

Kwenye migani ya ‘Fumo Liyongo’ kuna urudiaji katika lile shairi alilomkaririа kijakazi saada lina vina vinavyoishia hivi;

Kijakazi saada nakutuma tumwa tumika
Kamwambie mama ni muinga hayalimuka
Afanye mkate pale kati tupa kaweka
Nikereze pingu na minyoo ikinemuka
Niparage kuta na madari kuyakiuka

Na katika ngoma za gungu aliimba nyimbo zilizokuwa na vina vya mwisho vya

-- - Liyongo
-- - Mwengo
-- - ringo
-- - zifungo
--- - shingo

Hii ni takriri vina. Urudiaji huu huwa njia ya kudumisha ridhimu na kuonyesha umahiri wa mtunzi katika usanifu wake. Takriri vina ni mojawapo ya kaida muhimu za mashairi ya kimapokeo.

### 5.2.6 USAMBAMBA

Usambamba ni aina maalum ya urudiaji katika matumizi ya lugha ambapo hupatikana katika kiwango cha kirai, kishazi au sentensi. Kuna aina mbalimbali za usambamba. Miongoni mwa aina hizi ni usambamba wa kimuundo na usambamba wa kisintaksia. Usambamba wa kimuundo ni aina ya urudiaji ambao hujengeka katika urudiaji wa muundo ulio sawa. Urudiaji wa aina hii hupatikana sana katika nyimbo za ngano na katika ushairi wa Kiswahili ambapo muundo sawa wa baadhi ya mishororo hurudiwa katika beti mbalimbali.

Kwa upande mwingine usambamba wa kisintaksia ni aina ya urudiaji katika matumizi ya lugha ambao unahusu uruduaji wa vipengele au vipashio vya kisintaksia katika mfuatano. Vipengee virudiwavyo viwe virai au vishazi, hupatikana katika sehemu ile ile ya sentensi vikiwa vimeandamana. Mifano mingi tumeitoa katika sehemu ya takriri. Mfano mmoja zaidi ni katika kisa cha ‘sungura na cheche’. Sungura anapokasirika na kuondoka akihisi njaa kali baada ya kitoweo chote cha kanga na mayai kuliwa na cheche. Akiondoka na kwenda zake anasema;

*Twende kwetu, twende kwetu tukatafute chakula.*

Hii ni takriri ya kifungu – maneno yanayofuatana ili kusisitiza kuonyesha hisia za hasira alizokuwa nazo sungura baada ya kukikosa chakula.

### 5.2.7 TANAKALI ZA SAUTI

Tanakali ni neno ambalo huiga sauti fulani, jinsi kitu kiangukavyo au kilivyo. Msingi mkuu wa matumizi ya mbinu hii ni kumwezesha msomaji kupata taswira kamili na hisia za mlio wa kitu kinachozungumziwa.

Wamitila (2003) anathibitisha kauli hii kwa kusema kuwa tanakali sauti hutumiwa kurejelea sauti ambayo inaigiza jinsi kitu fulani kiangukavyo, kiliavyo, kilivyo n.k.
Katika uhakiki, wataalamu wanatofautisha kati ya tanakali sauti inayotuletea hisia za mlio wa kitu fulani na tanakali sauti inayotukumbusha maneno yanayohusiana na neno fulani maalum.

Mbinu hii imetumiwa katika kisa cha 'sungura na cheche' kutuelezea hisia za sungura za uchovu anapomweleza cheche kuwa;

> *'Mchome kanga huyu na mayai hayo pia yachome mimi nimechoka tik!'*

Katika kisa hicho hicho, cheche anachukua zumari na kuipiga ili kumkebehi sungura, cheche anasema,

> *Kanga pia singizia moto, ti! ti! ti! ti! ti!* --- *maana yake – kanga nimemla wote.*

Sungura naye alipoyasikia maneno ya Cheche katika zumari akachukua ngoma kubwa akapiga akisema,

> *Nikamtwaa nikamfungafunga na majani ya mgomba nikampiga pu! pu! pu! pu!*.

Aidha, katika kisa cha 'ndovu na binadamu' mtunzi anatuelezea kuwa baada ya ndovu kukaribishwa na mwenyeji wake ili auingize mkonga wake tu yeye aliuingiza mwili wake wote na kumsukumia mwenyeji wake nje apambane na mvua. Anasema;

> --- *Sasa ndovu alitulia tuli!, burudani kabisa!*.

## 5.3 MBINU NYINGINE ZA LUGHA

### 5.3.1 NIDAA

Hii ni mbinu ambayo hutumika kuonyesha hisia fulani kama vile mshangao, furaha, hasira au kukataa jambo fulani. Alama ya mshangao hutumiwa kuleta hisia iliyokusudiwa. Kwa mfano katika ngano ya Sungura na Simba, Sungura alipogundua kuwa simba alikuwa akimtafuta, alitafuta mbinu ya kuelewa kama simba alikuwemo nyumbani mwake.

Aliisalimia nyumba yake akisema, 'Salamu nyumba! Salaamu nyumba! salaamu nyumba! Yule simba alipodanganyika na kuitikia salaamu sungura akasema;

> *'Loo! simba umo ndani, wataka kunila mimi mwanao, ukasikia wapi nyumba kusema?' 'Simba akamwambia, 'uningojee basi,'*

Cheche alipomla kanga na kusingizia kateketezwa na moto alipatwa na usingizi jambo ambalo halikuwa kweli. Sungura alimwangalia akasema,

> *Basi!* --- *Sungura alijua tu kuwa cheche kamla kanga walakini kasingizia moto*

Sungura hakukubaliana na maelezo ya cheche kuhusu kutoweka kwa kanga, aliamini kanga kaliwa na cheche.

**5.3.2 TASWIRA**

Taswira ni picha ambazo humjia msikilizaji akilini anapoisoma kazi fulani ya kifasihi. Picha hizi hujengwa kwa maelezo fulani. Aidha hujengwa kwa matumizi ya tamathali za usemi kama tashibiha na sitiari. Sababu moja ya kutumia taswira ni kumfanya msomaji aelewe vile mtu au kitu kinavyoonekana na pia kutoa msisitizo fulani.

Kuna taswira kadhaa ambazo zimetumiwa na msanii katika ngano tulizoziteua kwa mfano, katika kisa cha "binti Matlai Shamsi," anatupatia picha ya mfalme aliyekuwa akibarizi akipunga upepo bustanini mwake kwa njia ya maelezo. Anaeleza kumhusu yule ndege wa ajabu hivi.

> --- *Alipokuwa bustanini alimtokezea ndege mmoja aliyekuwa mfano wa sana Alikuwa na mbawa za dhahabu na miguu ya rangi ya lulu; si mirefu si mifupi, si minene si mwembamba.*

Maelezo haya yote kumhusu huyu ndege yanajenga picha ya sura na uzuri wa yule ndege. Pia mtunzi ametumia taswira ya kimaelezo katika kisa cha 'binti Matlai Shamsi' anapotuelezea jinsi yule kitinda mimba wa suria alivyompokea kijakazi wa binti wa

mfalme na kumpamba. Anasema kuwa ‘akampamba nguo nzuri nzuri, akamvika na fedha na dhahabu akawa mzuri kupindukia.’

Hapa tunapewa picha ya uzuri na urembo aliokuwa nao kijakazi huyo baada ya kupambwa na kupambika ili isionekane tofauti iliyoko kati yake na binti wa mfalme isije ikagunduliwa na majitu kisha wakanyimwa yule ndege wa dhahabu.

Katika ngano ya ‘Sungura na Simba’ tunapewa maelezo ya jinsi Sungura alivyomhadaa Kobe, “Kobe akakubali, wakaondoka kuelekea ulipokuwa ule mzinga. Walipofika huku wamebeba mienge kama kawaida wakapanda juu. Waliwachoma nyuki, wakakimbia. Sungura na kobe wakakaa kitako na kuanza kula asali.”

Maelezo haya yanatupa picha ya kwamba ili mtu aweze kuila asali iliyo mzingani ni lazima aweze kuwafukuza nyuki mwanzo na ndivyo Sungura na Kobe walivyofanya kwa kutumia mienge waliyoibeba.

Hizi ni taswira ambazo hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi au lugha anayoitumia msimulizi. Hata hivyo hazina maana ya ziada au iliyofichika inayohitaji kufumbuliwa. Msimulizi ametumia lugha ambayo ina uwezo wa kujenga picha fulani katika akili ya msomaji au msikilizaji wake.

### 5.3.3 VILIWAZO

Wamitila (2003) anasema kiliwazo ni sehemu ya hadithi ambayo huwa imekusudiwa kuituliza hadhira kidogo hasa kwenye hadithi zinazozungumzia masuala ya kusikitisha au ya kitanzia.

Kiliwazo kinaweza kuwa kifungu kilichojaa ucheshi kilichokusudiwa kuiondoa kwa muda ile hali ya kusikitisha. Nyimbo hutumiwa kama viliwazo. Kwa mfano, katika migani ya ‘Fumo Liyongo’, mtunzi anatueleza kuwa Liyongo alipokuwa gerezani aliomba iandaliwe sherehe ya gungu kabla ya kuuliwa kwake. ‘Watu walikusanyika nje ya gereza alikofungwa Fumo Liyongo kwa ajili ya gungu hiyo.

Huko ndani Fumo Liyongo alikuwa akiimba nyimbo nzuri za kuwatumbuiza waliokuwa huko nje. Wakati anaimba alikuwa akizikata zile pingu na minyororo. Wimbo tutaupata kwenye kiambatisho.

**5.3.4 USIMULIZI**

Katika ngano ya 'cheche na sungura', sungura anasema: 'Mimi sina mke wala sina mama wala mtoto, afadhali tukae pahali pamoja mimi na wewe. Sungura akamwambia cheche 'Mchome kanga huyu na mayai nayo yachome. Mimi nimechoka tik, nitalala kidogo.

Usimulizi wa nafsi ya pili huhusisha viwakilishi vya nafsi ya pili "wewe" na "u" kulingana na Wamitila (2003) ni kuwa aina hii ya usimulizi ni nadra sana kupatikana. Kwa mfano; katika kisa cha 'ndovu na binadamu' ndovu anamwambia simba "….kama uonavyo nimo ndani, umefanya vizuri kuwa na urafiki na watu wangu hasa ndovu ambaye ni mmoja wa mawaziri wakuu kwenye dola yangu."

Usimulizi wa nafsi ya tatu huwa na matumizi ya 'a' na 'yeye' katika viwakilishi vya nafsi. Ni mtindo ambao hupendelewa sana na wasomii. Hadithi huelezea matukio yanayohusu mtu mwingine. Msimulizi huwa nje ya hadithi akisimulia juu ya mhusika fulani.

Wellek na Warren (1949) wanasema kuwa katika tenzi, mtunzi husimulia kisa kama msimulizi wa nafsi ya tatu. Wakati mwingine huwapa nafasi wahusika wake kuzungumza moja kwa moja. Kuna waandishi ambao huchagua kusimulia kisa pasipo kushiriki moja kwa moja, huwaacha wahusika peke yao na kumruhusu msomaji kuwahakiki bila kumwelewa msimulizi. Usimulizi mwingine humruhusu msikilizaji kumwelewa msimulizi na mitazamo yake kuhusu mambo yanayoikabili jamii.

Usimulizi wa matukio huweza kuwa wa nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu. Katika ngano usimulizi ni muhimu sana kwani huwasilisha ufafanuzi zaidi wa sifa za mandhari, wahusika wake, majukumu yao na matukio yakiwa katika mbinu ya mfululizo au

kukatizwa kwa visa. Pia kipengele cha toni hudhihirika katika usimulizi msanii atakaowasilisha. Katika ngano teule za Kiswahili tulizohakiki mtunzi ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu na amefaulu sana katika matumizi ya mbinu hii.

## 5.4 HITIMISHO

Katika sura hii tunaelezea matumizi ya lugha katika kiwango cha kisemantiki. Tumeangazia matumizi ya semi mbali mbali na kutoa mifano anuwai kutoka ngano mbalimbali ili kuthibitisha hoja zetu.

Aidha, tumeangalia namna tamathali za semi zimetumiwa ili kutoa mvuto wa kisanaa, kuonyesha ukomavu wake wa lugha na zimechangia pakubwa katika muundo wa maumbo ya ngano tulizoteua. Baadhi ya tamathali za usemi ambazo tumezigusia ni pamoja na tashbihi, tashhisi, chuku, kinaya nidaa, takriri miongoni mwa nyingine. Tamathali hizi zina majukumu kadhaa. Zimetumiwa kufafanua maana, kuibua hisia, kuhuisha, kuchekesha au kurembesha. Muhimu zaidi ni kwamba zina jukumu la kuongeza ujumi katika hadithi zinamotumika.Mbali na hayo,tumejadili kuhusu mbinu nyingine za lugha ambazo msimulizi amezitumia. Mbinu hizo ni; takriri, tanakali za sauti, nidaa, taswira na viliwazo. Tunaelezea pia kuhusu usambamba na toni. Matumizi ya mbinu hizi katika ngano hizi zimeifanya kuwa na mvuto wa kiujumi, kuburudisha msikilizaji na kumwondolea ukinaifu wa lugha chapwa.

# SURA YA SITA

## 6.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tunawasilisha hitimisho la utafiti wetu. Sura hii ina sehemu zinazoshughulikia matokeo ya utafiti, utathmini wa nadharia tete, umuhimu wa utafiti na mapendekezo ya utafiti zaidi juu ya ngano za Kiswahili.

## 6.1 MUHTASARI WA MATOKEO

Tumeona kuwa ploti ya ngano hizi ni sahili.. Ploti zenyewe zinatiririka kimfuatano. Hakuna urejelezi nyuma isipokuwa katika migani ya Fumo Liyongo. Mengi ya masimulizi ni ya moja kwa moja. Katika sura ya tatu na ya nne tumebaini sifa mbalimbali za wahusika na mbinu mbalimbali za usimulizi zinavyojitokeza katika ngano tano za Kiswahili tulizoteua. Tumeangazia usimulizi katika nafsi anuwai kama usimulizi nafsi ya kwanza, ya pili na nafsi ya tatu. Tumeona jinsi mbinu hii inapotumiwa vizuri na mtunzi huleta mvuto na kuifanya hadhira ishiriki kikamilifu katika usimulizi.

Katika sura ya tano tumehakiki vipengele zaidi vya fani. Hapa tumehakiki matumizi ya lugha. Tumechanganua matumizi ya tamathali za usemi, tumeona kwamba katika kiwango cha semantiki kuna ukiushi wa kimaana kwa kutumia semi za tamathali za usemi ili kuzua maana mbalimbali. Licha ya hayo tumegundua kwamba semi na tamathali za usemi zimechangia thamani ya kiujumi katika hadithi tulizohakiki. Tumebainisha kuwa tamathali za usemi zina umuhimu mkubwa kwa vile zimetumiwa kufafanua maana, kutoa mifano mwafaka, kuibua hisia, kuzua ucheshi mbalimbali na kuongeza ujumi wa kisanaa. Watunzi wa ngano hizi wameifinyanga lugha kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kubuni tamathali za usemi na ukiushi wa kaida za kisarufi.

Tamathali tulizoziangalia ni pamoja na tashbihi, chuku, usambamba, takriri, tashhisi, kinaya, taswira miongoni mwa nyingine. Madhumuni yetu ya pili yalikuwa kutathmini mchango wa vipengele vya fani katika kuwasilisha maana katika ngano zilizoteuliwa. Tumebaini kuwa vipengele vya fani vina mchango mkubwa sana katika kuwasilisha

maana na maudhui yanayobainika kutokana na fani mbalimbali. Hali kadhalika vipashio vya fani vimesaidia kuleta picha kamili ya hali ya mambo katika ngano hizi. Bila ya vipengele hivi vya fani, maana na taswira katika simulizi hizi hazingejitokeza kwa uwazi. Hivyo basi, fani ina mchango mkubwa katika utunzi na usimulizi wa ngano za Kiswahili.

Katika lengo letu la tatu tulikusudia kutathmini kufana au kutofana kwa watunzi wa ngano za Kiswahili tulizoteua. Tumefanikiwa katika kulithibitisha lengo hili kwenye sura ya tatu , nne na tano, pale ambapo fani zilizotumiwa na watunzi wa ngano hizi wamefaulu katika utunzi wao. Wasanii hawa wameweza kuzipa ngano miundo iliyoshikamana kutokana na vitushi vizuri vya fani vilivyoingiliana na kutegemeana. Tumeona ya kuwa katika kila ngano kuna dhamira inayojitokeza ambayo mtunzi anatarajia hadhira yake kuipokea.

**6.2 KUHUSU NADHARIA TETE**

Nadharia tete yetu ya kwanza ilisema kuwa vipengele vya fani katika ngano za Kiswahili vimeingiliana na kuhusiana katika ujenzi wa umbo au muundo wa ngano zenyewe. Nadharia hii tumeithibitisha kuwa kweli kwa kuwa misuko na masimulizi pamoja na uumbaji wa wahusika vimeingiliana vizuri na kushikamana kiasi kwamba huwezi kuondoa moja kisha muundo wa ngano ile ikabakia na uwezo wa kuwa na umbo lililokusudiwa. Tumeona ya kuwa kuelezea msuko wa ngano hizi ni sawa na kuelezea usimulizi wake na pia kuelezea msuko wenyewe ni sawa na kuelezea sifa za mhusika, kama tulivyoona katika sura ya tatu na sura ya nne.

Nadharia tete ya pili ya utafiti ulisema kuwa, vipengele mbalimbali vya fani katika ngano teule za Kiswahili zimechangia pakubwa katika kuwasilisha maana za ngano zenyewe. Tumedhihirisha nadharia tete hii kuwa ya kweli. Kutokana na matumizi ya lugha, msimulizi ameweza kuwasilisha maana ya sifa katika ngano hizi. Tamathali za usemi zimetupa taswira na sifa mbalimbali za wahusika. Wahusika wanyama katika ngano hizi wametumiwa kisitiari kuwakilisha tabia za binadamu halisi katika jamii.

Wahusika hawa ni wa viwango viwili tu, aidha wabaya au wazuri. Mhusika mwenye tabia mbaya hastahili kuigwa.

Nadharia tete ya tatu ilisema kuwa, watunzi wa ngano za Kiswahili tulizoteua wamefaulu katika usanifu wa muundo. Tumeona kuwa nadharia tete hii ni kweli. Watunzi wa ngano hizi wamewaumba wahusika wao vizuri. Pia wametumia misuko sahili ambayo inasaidia kueleweka kwa ngano hizi kwa njia rahisi. Fani katika ngano hizi imeingiliana vizuri na vipengele vyake haviwezi kutenganishwa.

## 6.3 MAPENDEKEZO YA UTAFITI

Tumehakiki fani katika ngano za Kiswahili kwa kutumia nadharia ya umuundo. Hata hivyo vipengele kama vile uchambuzi wa lugha katika kiwango cha msamiati. Lahaja za mwambao wa pwani sikuzichambua kwa sababu ya uhaba wa wakati. Tumependekeza kuwa watafiti wa baadaye watakaofanya utafiti katika ngano za Waswahili washughulikie swala hili. Fani katika ngano pia huweza kuhakikiwa kwa kutumia nadharia tofauti na ya umuundo na kuleta ufaafu unaostahili.

## MAREJELEO


African, Corporation. (1977) *Encyclopedia Americana Volume* II. New York. American Corporation.

Akiranga, S. /Odanga, B. (1982). *Oral Literature, A School Certificate Course,* Nairobi Ibadan London. Heinemann Educational Books.

Culler, J. (1975*). Structuralist Poetics*, London. Routledge and Kenya Paul.

Farsi, S. (1958) *Swahili Sayings from Zanzibar*. Heinemann Educational Books.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa,* London. Oxford University.

____________(1992). *Oral Traditions and Verbal Arts, Guide To Research,* London: Routledge.

Forster, E.M (1927) *Aspects of the Novel*, London. Arnold and Company.

Fuertes, C. (1971). *Class Codes and Control*, London Routledge And Kagan Paul.

Gitaru, J. (1989). "Uhakiki wa Muala Katika Ngano za Waswahili*"*. Tasnifu ya Uzamili chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Healey, J. (2006). *Towards An African Narrative*, Nairobi: Paulines Publication Africa.

Holman, C. Na Harmon, K. (1986). *Faces of Islam in Africa Literature*. London: Heinemann Portsmouth.

Kezilahabi, E. (1997). *"Creative Writing in Swahili*",Makala ya Kongamano la Uandishi wa Kibunifu Katika Lugha za Kiafrika,uk 28-34

Kigwe, S. (1993). *Hekaya za Miujiza Uarabuni*. Hadithi za Kumbukumbu. Nairobi Macmillan Publishers.

Kirumbi, P. (1975) *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi, Shungwaya Publishers Ltd.

Kuhenga, C. (1977) *Tamathali za Usemi*. Dar es Salaam,East African Literature Bureau.

Kombo, D./ Tromp, L. (2006) *Proposal and Thesis Writing*: Paulins Publishers.

Lawrence, P. (1959) *Story and Structure*. New York, Hart Court, Brace and World. Inc.

Marx, K./ Angels, F. (1967) *The Communist Manifesto*. Middle- Sex, Penguin Books.

Matteru, L.M (1979 )"Utafiti, Mbinu na Ukusanyaji wa Fasihi Simulizi na Hatima Yake".Lugha Yetu uk.34-36.

Mbatia, M. (2001) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks, Graphics and Publishing.

Mbele, J. (1982) *Oral Literature and the Written Tradition*. Heinemann Educational Books.

Mghanga, J. (1984) *Fasihi Simulizi Katika Jamii, Uhakiki wa Ngano wa Kidawida.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Mlamali, M.(1980) *Inkishafi:* Nairobi. Longman Publishers

M'ngaruthi, T. (2008) *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Msokile, M. (1992) *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dare es Salaam University Press.

Mulokozi, M. (1983) “Utafiti wa Fasihi Simulizi, Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili”. uk 42-50

Nandwa, J. /Bukenya, A. (1983) *African Oral Literature for Schools*. Nairobi. Longman.

Ngara, E. (1985) *Art and Ideology in the African Novel*, London. Heinemann.

Ngole, S./ Henero, N. (2006) *Fasihi Simulizi ya Mtanzania*. *Methali Kitabu Cha Pili*,Dar es Salaam, TUKI.

Ngure, A. (2007) *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Njogu, K./ Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji Wa Fasihi*, *Nadharia na Mbinu*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Rubanza, Y. (1984) *Fasihi Simulizi: Majigambo*. Dar es Salaam. TUKI.

Steere, E. (1970) *Swahili Tales as Told By Natives of Zanzibar*. London: Harverd College Library.

Timammy, R. (1990) “Uhakiki wa Ngano Za Kiswahili”. *Tasnifu na Uzamili*, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

TUKI (2004*) Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam, TUKI.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wales, K. (2001) *A Dictionary of Stylistics* (2nd Edition) England: Pearson Education Ltd .

Wamitila, K. (1999) *Kamusi ya Misemo na Nahau*. Nairobi. Longhorn Publishers.

__________ (2002), *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi. Phoenix Publishers Ltd.

___________ (2003 A) *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*, Nairobi: Focus Books.

___________ (2003 B) *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.

___________ (2008) *Kanzi ya Fasihi, Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi. Vide- Muwa Publishers Ltd.

Wamutiso, K. (2005) "Hurafa ya Uyakinifu Katika Hamziyyah". Tasnifu ya Uzamili chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Wellek, R./Warren, A. (1949) *Theory of Literature New York*, Penguin Books.

## VIAMBATISHO

Ngano hizi tano tumeziteuwa kutoka *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi* wamitila (2003). ngano hizi zimekusanywa na kuhaririwa na Wamitila K.

### KISA CHA BINTI MATLAI SHAMSI

Aliondokea mtu mmoja mfalme aliyekaa kwa furaha na buraha katika ufalme wake pamoja na watoto wake sita wa mke mmoja na mmoja wa suria wake. Huyu ndiye aliyekuwa kitinda mimba wa suria huyo. Basi kwa hivyo mfalme huyo aliishi na watoto wake saba. Kama kawaida yake, mfalme alikuwa na mazoea ya kwenda kwenye bustani yake kuketi na kubarizi akipunga upepo. Basi siku moja alipokuwa bustanini alimtokezea ndege mmoja sana aliyekuwa na mbawa za dhahabu na miguu ya rangi ya lulu;si mrefu si mfupi si mwembamba.

Yule ndege alikuja na kutua karibu na mti alipokuwa mfalme akibarizi na kuifurahia bustani yake nzuri.Baada ya yule ndege kuondoka, mfalme aliwaita wanawe na kuwaambia: tafadhalini wanangu yule anipendaye lazima aniletee yule ndege. Wale watoto wa mke wake wakasema: tutakuletea ndege yule baba; naye akajibu: vyema. Yule mtoto wa suria hakusema neno lolote . Baada ya muda wote waliondoka na kuandamana kuelekea nyumbani.

Walipokuwa huko walifanya mashauri ya kuanza na kila mmoja akipewa farasi mmoja na watumwa mia. Yule kitinda mimba akamwambia baba yake: Na mimi baba nitasafiri pamoja na ndugu zangu kwenda kumtafuta ndege huyo. Baba yake akamwambia: Wewe mwanangu bado kijana hutaweza kwenda katika safari ya aina hii. Mtoto naye akajibu: hali yangu ni kama hali ya wenzangu, nikipata sawa, nisipopata basi. Baada ya maneno hayo, baba yake alimtayarishia safari naye akapewa farasi na watumwa mia pamoja na fedha kwa sababu alipendwa sana na babake. Basi wale watoto, wote saba kwa jumla, waliondoka kwenda kumtafuta yule ndege wa ajabu. Walienda mwendo wa karibu siku tano kwenye bara kubwa hadi walipofika karibu na sehemu iliyokuwa na msitu na wale ndugu sita wakaamua kumuua ndugu yao.

Walimwambia, “tupe mali yako na farasi wako pamoja na watumwa wako na kama hutaki tutakuua”. Naye akasema, “hapana haja ya kuniua.Mkiniua mimi nitapoteza roho yangu na mtaipata mali,afadhali muichukue mali na mniachie roho yangu. Basi wakamnyang’anya mali yote wakamwacha tu na nguo zake za mwilini na kitabu alichokuwa nacho. Baada ya kufanya haya, wale watoto sita wakasema, “baba yetu ana wazimu: ametwambia twende kumtafuta ndege, na ndege ana mbawa anaweza kuruka juu na sisi tunakwenda chini, tutawezaje kumshika? Sisi tufanye maskani hapa, tupafanye mji, maana kila mmoja ana watumwa mia moja pamoja na wale tuliomnyang’anya yule. Hawa wanatosha kutufanyia kazi; tukae hapa kwa kipindi kilichobaki cha uhai wetu katika dunia hii.”

Yule kijana aliyenyang’anywa mali na watumwa wake, alishika njia msitu na nyika, msitu na nyika, msitu na nyika kwa mwendo wa siku mbili kwa miguu mpaka akatokea mahali palipokuwa na jangwa kubwa. Katikati ya jangwa hilo palikuwa na mti mkubwa sana alipoamua kupumzika kwa muda. Alipokuwa hapo alisikia kishindo kikubwa kwenye sehemu ya mwitu na alipotupa macho akaona zimwi kubwa sana likija. Lile zimwi lilimsogelea na kumwuliza, “mtoto wee unatoka wapi na unakwenda wapi?” Yule kijana akajibu, “sijui nitokako wala niendako”. Lile zimwi likamwangalia na kusema, “wewe hata hunitoshi chakula changu hata kwa saa moja.” Yule kijana akajibu, “ni kweli sitoshi.” Lile zimwi likasema, “damu yako itakuwa tu kama maji ya kusukutua kinywa, mifupa yako nayo kama mswaki wa meno yangu na nyama yako kama kifungua kinywa halafu niingie mwituni nitafute tembo wawili maana hunitoshi wewe.”

Yule kijana akaliambia lile zimwi, “ni kama atakavyoamuru Mungu nifanye, maana mimi sina amri, amri yote ni ya Mungu na mtume wake .Maana mimi nimeondoka kwetu na ndugu zangu sita mimi wa saba. Baba yetu amemwona ndege na kutamani sisi tukamtafutie ndege huyo. Tulipofika mwituni walinikamata wenzangu ili kutaka kuniua na kuninyang’anya mali yangu. Basi nikawaambia hivi: msininyang’anye roho yangu afadhali twaeni haya mali mniachie roho yangu nikafie mbele. Basi wakaninyang’anya mali yote nami nikaondoka peke yangu na kufika hapa hata ukaniona wewe leo.”

Basi lile zimwi likamwambia, “kama unaitaka roho yako wewe nifanyie chakula unipe nile.” Yule kijana akasema, “mimi peke yangu sina chakula nitapata wapi chakula cha kukupa wewe katika mwitu huu?” Akamwambia, “nitakuua kama hutanipa chakula. Akamwambia, “nimekupa muda wa saa mbili.” Yule kijana akatwaa kitabu chake akasoma akaomba Mungu, “mara akaona masufuria arobaini ya vyakula. Lile zimwi likafurahi sana kwa kupata chakula. Likayainamia yale masufuria na kula chakula chote kilichokuwa mle kwenye masufuria yenye uzito wa ratili mia mbili. Yule kijana alistaajabu sana alipoliona lile zimwi limekula masufuria arobaini. Lilipomaliza lile zimwi lilimwambia yule kijana, “sasa tuulizane hali maana nimeshiba na akili yangu imetulia kichwani. Lile zimwi likamwambia yule kijana, “nipe habari yako sasa; nieleze ni nini unachotafuta.” Yule kijana akamwambia, “natafuta ndege mwenye umbo la dhahabu na lulu. Lile zimwi likasema: Ninajua anakokaa yule ndege, ni mbali lakini haidhuru twende.”

Yule kijana na zimwi wakaondoka kwa mwendo wa siku tatu hadi wakafika karibu na majumba fulani. Lile zimwi likamwonyesha yale majumba na kusema, “nenda penye nyumba zile unazoziona, utawakuta watu wengi waliolala; utamwona yule ndege unayemtaka na wengine katika tundu moja. Ukisikia watu wanazungumza wamelala, ukisikia wamenyamaza ujue wa macho hawakulala.” Yule kijana akaondoka akaenda mpaka akafika sehemu alikoelekezwa na alipofika huko akasikia vishindo vingi vya mazimwi, akasikia makelele mengi na kujua kuwa wamelala kama alivyoambiwa. Akasogea na kumwona yule ndege aliyemtaka lakini kabla ya kulifikia lile tundu lake, yale mazimwi yakazindukana. Yale mazimwi yalimkamata na kumpigia kelele yakisema: tumle, wengine wakisema: tusimle tumpeleke kwa sultani. Basi akaja yule mkubwa wao akasema: tusimle, tumpeleke kwa Sultani. Basi yule kijana akapelekwa kwa Sultani. Sultani akamwuliza: jambo gani lililokuleta huku? Yule kijana akamwambia kuwa nilichotaka ni ndege tu. Sultani akamwambia, “na kama unataka ndege, nenda ukanitafutia upanga wa radi, ukiniletea nitakupa ndege; na sio mmoja bali wote.”

Yule kijana akaondoka na kurejea alipokuwa rafiki yake lile zimwi. Lile zimwi likamwuliza, “mbona hukumpata yule ndege?” Yule kijana akasema: Sikupata: nimeambiwa nikatafute upanga wa radi, nikiupata nitapata ndege, na sio mmoja bali wote.”

Lile zimwi likamwambia: vyema rafiki yangu walakini nipe chakula kwanza nile tupate kufanya safari ya kwenda kutafuta upanga wa radi. Basi yule kijana akasoma kitabu chake halafu yakaja masufuria arobaini kama mara ya kwanza. Lile zimwi likala na kijana naye akala kidogo kisha wakaondoka wakaenda kwa mwendo wa siku mbili. Walifika mahali palipokuwa na majumba na lile zimwi likasema kuwa majumba hayo ndiyo yaliyokuwa na upanga wa radi. Lilimwambia yule kijana: basi nenda pale unapoyaona yale majumba. Yule kijana akashika njia mpaka akafika pale na kuona kama alivyoona huko nyuma: upanga ulikuwa pamoja na panga nyingine; jumla tatu. Aliponyoosha mkono wake kuuchukua ule upanga, yakaja mazimwi yakamshika.

Mengine wakasema: tumle, mengine wakasema : tumpeleke kwa sultani. Akaja mkubwa wao na kusema tumpeleke kwa sultani; wakamchukua na kumpeleka huko. Sultani akamwuliza alipofika; unatafuta nini huku? Yule kijana akajibu: Mimi natafuta upanga wa radi. Yule sultani akasema: Kama unataka upanga wa radi nenda ukanitafutie binti Matlai Shamsi; ukienda ukinileteа binti Matlai Shamsi nitakupa panga zote tatu. Yule kijana akaondoka na kurudi alipokuwa yule rafiki yake zimwi.

Lile zimwi likamwuliza: Je mbona hukuleta upanga wa radi? Yule kijana akamwambia; nimeambiwa niende nikamlete binti Matlai Shamsi, nikishamleta binti Matali Shamsi nitapewa panga zote tatu. Basi wakaondoka wakafanya mashauri ya kwenda kumtafuta binti Matlai Shamsi kama alivyotaka sultani. Walienda mpaka wakafika mahali karibu na pwani; wakang’oa miti na kuunda merikebu nzuri wakaitosa katika bahari wakaingia hadi wakafika mji alikokaa binti Matlai Shamsi ambao mfalme wake alikuwa baba yake binti huyo.

Walipofika yule kijana akaliuliza zimwi, “sasa tumekwisha fika tutafanya nini mpaka tumpate binti Matlai Shamsi?” Lile zimwi likamwambia, “utapata wala usifanye shaka, lakini inataka hila kubwa ili kumpata.” Yule kijana akauliza, “ni hila gani hiyo usemayo?” Zimwi likasema, “jigeuze mganga anayejua dawa na hirizi ambazo mtu akizifanya dawa hizo hafi.” Yule kijana akajibu, “hivyo ni vyema.” Lile zimwi likamwambia ; kesho shuka uende kwa mfalme umwambie kuwa unajua dawa na hirizi ambayo mtu akifanya hafi; walakini akikwambia fanya dawa ya binti yangu mwambie; dawa ya mtoto haifanyiwi penye nchi ila katika bahari, na akija huku binti yake tutamchukua.”

Yule kijana akaitikia maneno ya rafiki yake akamwambia; kesho nitakwenda nikijaliwa. Akalala hadi asubuhi kulipokucha akaondoka yule kijana akaenda hadi kwa sultani akataka ruhusa ya kuonana na sultani. Akamwambia sultani baada ya kumwamkia; mimi nimekuja kwako Seyidina na mimi najua dawa kadha, mtu akifanya hafi.

Sultani akamjibu; mimi nataka unifanyie mimi na wanangu, wake zangu na masuria wangu na jamaa zangu. Yule kijana akamjibu; hewala Seyidina, nitafanya. Yule kijana akaenda merikebuni akachukua ‘dawa’ zake akaja nazo hata kwa Sultani akafanya dawa ya watu wote isipokuwa yule binti. Akamwambia sultani; dawa ya binti haifai kufanyiwa katika mji au nchi; dawa ya binti lazima ifanyiwe baharini. Basi baba yake yule binti akasema; vyema, kesho atakuja. Yule kijana akasema; Inshaallah, walakini asije na watu wengi sababu dawa inataka siri. Baba yake akasema; vyema. Yule kijana akaondoka akaenda zake na kumwambia rafiki yake zimwi; yule binti Matlai Shamsi anakuja kesho. Na yule rafiki yake akasema; Inshaallah, na mimi niko tayari kufanya safari yetu.

Basi na huku nyuma kwa sultani akamwambia binti yake; kesho fanya safari ya kwenda merikebuni kwa yule mganga wala usiende na watu wengi; nenda wewe na mjakazi mmoja basi. Yule binti Matlai Shamsi akasema; hewalla baba. Akalala na asubuhi akafanya safari na mjakazi wake wakaenda mpaka merikebuni. Walipofika merekebuni

akatokeza yule kijana na kumkaribisha yule binti Matlai Shamsi chumba cha chini akimwonyesha madawa ya uwongo uwongo. Kumbe huku nyuma lile zimwi limekwisha kuifungua merikebu inakwenda na yule binti hana habari. Walipotoka huko chini merikebu ilikuwa imekwenda safari ya kutwa. Binti akauliza; huku wapi? Yule kijana akamwambia; huku kwetu na wewe usitie hofu, Inshaallah utarejea kwenu kama ulivyokuwa kwanza. Basi na huko nyuma walikotoka baba yake alipoona ile merikebu haiko bandarani akafanya wazimu akili yake ikampotea kwa jinsi alivyompenda binti yake; akaziambia merikebu zake zote ziende dunia nzima kumtafuta binti huyo. Merikebu zikaondoka zikaenda zikamtafuta hata zikachoka zikarudi bila ya kumwona. Yule sultani akalia na kusikitika sana.

Yule kijana aliyemchukua binti Matlai Shamsi akaenda hadi akafika karibu na mahali palipokuwa na upanga wa radi. Akamwita rafiki yake zimwi akamwambia; ee rafiki yangu nipe mashauri yako, Binti Matlai Shamsi tunaye na tunataka upanga tufanye shauri gani hata tupate upanga? Yule rafiki yake akamwambia; Shauri hapana ila mwombe kijakazi wake binti Matlai Shamsi; ukimpeleka useme; Huyu ndiye binti Matlai Shamsi. Yule kijana akamwambia vyema. Akaenda kwa binti Matlai Shamsi; tafadhali nipe kijakazi wako nikambadili na upanga wa radi. Binti Matlai Shamsi akaridhia. Yule kijana akampokea yule kijakazi akampamba nguo nzuri nzuri akamvika na fedha na dhahabu akawa mzuri kupindukia. Yule kijana akamchukua yule kijakazi akaenda naye hata akafika kwa sultani wa mji ule.

Yule kijana akaingia mjini akaenda hata kwa Sultani wa mji ule na kumwambia; huyu binti Matlai Shamsi uliyemtaka, nipe upanga wa radi, Sulatni akamwambia hizi hapa chukua zote tatu Yule kijana akamwambia, “la mimi sitaki isipokuwa upanga mmoja basi.” Sultani akamwambia; hiari na shauri yako, akanyanyua mkono akachukua upanga mmoja. Yule kijana akaenda na upanga wake hadi alipokuwa rafiki yake akamwambia; huu upanga wa radi nimekuja nao. Yule rafiki yake akamwambia; haya twende zetu sasa. Waliondoka wakaenda zao hata wakakaribia karibu na alipokuwa ndege. Yule kijana akamwambia rafiki yake; sasa tumekwisha fika panapo ndege tufanye shauri gani hata tumpate ndege? Rafiki yake akamwambia shauri kubwa na dogo najua mimi.

Walipokaribia wakakaa kitako katika hema, wakatoa vyakula vyao na kula. walipokwisha kula, lile zimwi likasema kata mti tuufanye upanga. Yule kijana akaukata mti akampa rafiki yake zimwi ambaye aliuchonga kama upanga na kuupaka dawa ukageuka chuma. Lilimwambia kijana; uchukue upanga huu uende nao hata kunako ndege upeleke umwambie Sultani kuwa upanga wa radi unaotaka huu nimekuletea; nipe huyu ndege nimchukue.

Kijana akaupokea upanga akauchukua akaenda nao mpaka akafika kwa sultani mwenye ndege. Alipofika kule akaenda hata kwa sultani akampa ule upanga akamwambia huu ndio upanga wa radi unaoutaka. Yule sultani akafurahi sana akamwambia; chukua ndege wote watatu wala sio mmoja tu. Yule kijana akasema; La. Mimi ninamtaka ndege mmoja tu, basi, akamwambia sultani vile upendavyo. Basi yule kijana akamchukua ndege mmoja na tundu lake. Akarudi naye hadi alipokuwa rafiki yake zimwi. Wakaondoka wakaenda zao hata karibu na walipokuwa wale ndugu zake. Lile zimwi likamwambia; Eeh rafiki yangu nikupeleke kwa baba yako au utakwenda kwa ndugu zako hapo walipokaa? Yule kijana akasema la rafiki yangu, nitakwenda kwa ndugu zangu, nipate kwenda nao pamoja kwa baba.

Yule rafiki yake akamwambia: haya nenda, walakini nitakupa akiba unyoya wangu ufutike. Endapo utakumbana na tatizo lolote katika dunia hii, uchukue unyoya na kuuchoma moto halafu utaniona mimi mbele yako nimekutokea.

Yule kijana akaupokea unyoya akaufutika mahali na kuagana na rafiki yake akaenda zake pamoja na binti Matlai Shamsi, ule upanga wa radi na yule ndege. Aliwakuta ndugu zake wamefanya mashamba wanalima akaingia yule kijana akawaamkia na kuwaambia habari yote. Wale ndugu wakamwuliza; ndugu yetu mwanamke gani huyu, na jina lake ni nani? Yule kijana hakuwaambia lolote isipokuwa mwanamke huyu nimemwokota njiani na jina lake silijui na huu upanga nimeukuta naye na ndege huyu ndiye anayemtamani baba. Basi twendeni sote kwa baba kwa shauri moja na kumwambia kuwa ndege tumemkamata pamoja. Wakalala hata usiku wakamkamata

ndugu yao wakamkaba roho hata akazimia wakamchukua wakaenda wakamtupa katika mto na yule binti Matlai Shamsi alipoona vile akakataa kula, kunywa wala kusema.

Wakaondoka wale ndugu zake wakaenda zao wakamchukua binti Matlai Shamsi na upanga ule na yule ndege hata wakafika kwa baba yao. Baba yao alipoona watoto wake akafurahi na akampokea yule ndege na kuzidi kufurahi. Akawauliza watoto wake; Ndugu yenu kitinda mimba yuko wapi? Wote wakasema hatujui, amekwenda na njia zake. Baba yao akasema na apotelee mbali sababu hakushika mashauri niliyompa. Mamake yule kijana akatolewa katika nyumba ya sultani, akafukuzwa, akapewa nyumba ya nje ndogo akakaa. Wale ndugu zake kijana wakaulizwa na baba yao mwanamke huyu jina lake nani? Wasema; hatumjui, tumemuokota njiani na upanga wake. Baba akauliza kwa nini mwanamke huyu hali wala hasemi wala kunywa? Wale vijana wakasema; labda mwanamke huyu anawaza kwao, alikopotea basi. Yule mkubwa akasema; nitamwoa mimi mwanamke huyu. Wakafanya mashauri ya kuoa.

Na yule kijana mtoni alikotupwa akalala hata asubuhi ukampiga upepo wa alfajiri akapata fahamu ya dunia akafufuka; akaondoka akakoleza moto akatoa unyoya wa rafiki yake. Mara akamwona rafiki yake mbele yake; Akamwambia; ee rafiki yangu, una nini? Akamwambia; kuja hapa jana kwa ndugu zangu yamenipata mambo kadha wa kadha; akamweleza kila kitu kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Akamwambia haidhuru twende zetu nikupeleke hata kwa baba yako. Akamchukua akampa nguo nzuri yule kijana akavaa akaenda naye akampandisha juu ya farasi akamchukua hadi kwa babake barazani. Watu walikuwa wamejaa baraza tele; mawaziri na makadhi na wale ndugu zake wamekaa na baba yake. Yule kijana akaanguka mbele ya baba yake akasema habari zote kuhusu yote yaliyomfika. Hata mwisho alilitaja jina la binti Matlai Shamsi pamoja na ule upanga wa radi. Lile zimwi lilikuwa pale pale tu.

Ndugu zake walikuwa palepale. Alikuja binti Matlai Shamsi akajinadi akasema watu wote wakastaajabu kwa kusikia mwanamke yule anasema. Mara baba aliamrisha watu akawaambia; wachukueni watoto hawa sita mkawaue wote. Wakachukuliwa wakatiwa katika mafumba wakaenda wakatoswa katika bahari. Yule kijana akapata heshima

kubwa kwa babake na mamake akapata heshima sana kuliko ilivyokuwa mwanzoni. Yule kijana akafanya harusi akamwoa yule binti Matlai Shamsi. Wakasafiri hata kwa baba yake binti Matlai Shamsi. Yule mzee alipoona kuwa binti yake amerudi akafurahi sana akamwambia kijana; ahsante, umenichukulia binti yangu halafu umeniletea. Akamwoza mara ya pili akafanya harusi kubwa kuliko ile ya kwanza. Wakakaa wakila wali wao na mkate hata wakachoka.

**KISA CHA CHECHE NA SUNGURA (JAMII YA WASWAHILI)**

Aliondokea cheche siku moja akamwambia sungura, “Mimi sina mke wala sina mama wala mtoto, na wewe kama mimi tu, huna mke huna mtoto, afadhali tukae pahali pamoja mimi nawe, tunachopata tule, na siku tusipopata tumshukuru Mungu.”Sungura akasema, “Vyema, taiyib! Mashauri yako mema.’ wakakaa mahali pamoja. Kazi yao ilikuwa kutega ndege wakila. Basi siku moja wakaenda maguguni kutega ndege wakagundua mahali palipokuwa na mayai ya kanga. Sungura akamwambia cheche: ‘Tutege kanga!’ Cheche akasema: Vyema. ‘Sungura akaenda akafanya mtego akatega akanasa kanga. Baadaye walimchukua kanga wakaelekea zao nyumbani.

Sungura akamwambia cheche ‘Mchome kanga huyu na mayai nayo pia yachome. Mimi nimechoka tik, nitalala kidogo. Cheche akasema, “Vyema.” Cheche akamchukua yule kanga akamchoma, akachoma pia na yale mayai. Sungura akaenda zake kulala.

Kanga alipoiva, cheche akasikia harufu nzuri kupindukia. Hamu kubwa ikamwingia kwa hiyo akamla yule kanga na kummaliza. Alichukua yale mayai nayo akayala yote. Alilichukua ganda moja la yai la kanga na kuliweka sawasawa kisha akalificha mahali. Baada ya hayo akachukua manyoya yaliyobakia na miguu ya kanga akatia motoni naye akalala.

Manyoya yalitoa harufu kali ya kunuka yalipokuwa yakiungua motoni. Sungura akazinduka kwa harufu akamwamsha cheche akamwuliza, ‘kanga yuko wapi?’ Cheche akasema; Nimemwacha hapa katika moto usingizi ukanishika nikalala, basi kaungua kanga. Sungura alimwangalia akasema; Basi!

Lakini sungura alijua tu kuwa cheche kamla kanga walakini kasingizia moto. Sungura akasema, “Twende kwetu, twende kwetu kutafuta chakula.” Cheche akasema “Vyema na mimi nitakwenda kwetu sasa hivi.” Sungura akaondoka akaenda zake akajificha mahali. Cheche akashiba sana akalala njiani. Sungura akatafuta majani ya mgomba akanyatia nyatu nyatu mpaka alipokuwa cheche. Akamfunga majani akamfunga vyema, akampiga sana. Halafu sungura akaondoka akaenda zake.

Cheche akapiga usiahi halafu akanyamaza, na mtu aliyempiga hamjui kabisa. Akaja sungura akamsukuma cheche miguu yake akasema; ‘Nini hiki?’ Akamsukuma. Cheche akamwambia, mimi rafiki yako. Akamwuliza : “Una nini?” Cheche akasema kaja mtu akanifunga akanipiga sana. Sungura akauliza, ‘Unamjua mtu huyu?’ Cheche akasema simjui. ‘Sungura akakasirika akamfungua akamwona anataabika mno. Wakakaa kitako.

Basi siku moja pakatokea ngoma ya kiumbizi kwao cheche. Cheche akamwambia sungura; ‘Nakualika kwetu, kuna kiumbizi leo.’ Sungura akasema; ‘Vyema, walakini nitakwenda kwetu kwanza. Nitakuja alasiri.’ Cheche alisema; ‘Vyema basi.’ Sungura akaenda zake.

Cheche akavaa nguo zake akachukua yai la kanga akavaa kichwani akatwaa unyoya wa kanga akachomeka juu ya lile yai akaenda kwao kucheza kiumbizi mpaka alasiri. Alasiri hiyo sungura akafika kwenye kiumbizi kama alivyosema. Cheche alipomwona sungura akamkaribisha naye akakaa kitako.

> Mara cheche akatwaa zumari akapiga
>
> Kanga pia singizia moto ti! ti! ti!
>
> Maana yake; kanga nimela wote
>
> Sungura akasikia maneno yale katika zumari akaruka akashika ngoma kubwa akapiga.
>
> Nikamtwaa nikamfungafunga na majani ya mgomba nikampiga, pu! pu! pu!

Cheche akasikia maneno ya ngoma akakasirika mno akashika fimbo wakapigana sana, hata masikio ya cheche akatwaa sungura na sungura akatwaa cheche. Ndio maana sungura ana masikio marefu. Kwanza alikuwa cheche mwenye masikio marefu, sungura alikuwa na masikio mafupi.

**SUNGURA NA SIMBA (JAMII YA WASWAHILI)**

Siku moja aliondoka sungura kwenda kutafuta chakula msituni na kuuona mbuyu mkubwa sana. Alipoyatupa macho yake juu aliuona mzinga mkubwa sana wa asali ya nyuki. Aliamua kurudi zake nyumbani ili akawaite wenzake waje wapate kuila asali hiyo.

Alipita alikoishi panya buku ambaye alimkaribisha wakakaa kitako. Baada ya mazungumzo, sungura alimwambia, baba ameaga dunia na kuniachia mzinga wa asali, twende tukaile.’ Basi baada ya kusema hivyo, wote wakaondoka kuelekea mwituni.

Walipofika huko, sungura akamwambia mwenzake, ‘Basi panda juu’ Panya buku akafanya hivyo na sungura naye akamfuatia. Walikuwa na mienge ya moto waliyoitumia kuwachoma nyuki waliojazana mzingani. Baada ya kufanya hivyo wakaanza kula asali iliyokuwako.

Mara akatokea simba chini ya ule mbuyu uliokuwa na mzinga wa nyuki. Yule simba aliyatupa macho yake juu na kuona watu wanakula, akawauliza, ‘Ninyi ni nani?’ Sungura akamwambia buku, ‘nyamaza, ana wazimu mzee yule!’ Simba akauliza tena, ‘Nani ninyi, hamsemi?’ Buku akaogopa baada ya kuisikia ile sauti ya juu ya simba akajibu, ‘Sisi hapa!’

Sungura akamwambia buku, ‘Nitwae mimi, unitie ndani ya mwenge, umwambie mzee simba, jitenge nitupe mwenge, nami ninakuja. ‘Buku akafanya kama alivyoshauriwa na sungura. Alipomtaja simba akajitenga na buku akautupa mwenge chini. Ulipoanguka chini, sungura akafyatuka kama mshale, huyooo akakimbia akaenda zake.

Baada ya muda simba akamwambia buku, ‘shuka basi.’ Buku akashuka kwa hofu na wasiwasi mkubwa. Alipofika chini tu, simba akamkamata. Alimwuliza, ‘ulikuwa wewe na nani huko juu?’

Akamwambia, ‘mimi na sungura. Je, hukumwona hapa nilipomtupa?’ Simba akamwambia, sikumwona. Akamshika buku na kumla papo hapo. Baadaye akatoka kwenda kumtafuta sungura, asimwone.

Baada ya siku kadha sungura naye akaenda, akamwita kobe akamwambia, ‘twende tukale asali.’ Kobe akamwangalia sungura kwanza na kumwuliza. ‘Ya nani?’ Sungura naye akajibu mara moja ‘ya baba.’ Kobe akakubali, wakaondoka kuelekea ulipokuwa ule mzinga. Walipofika hapo huku wamebeba mienge kama kawaida wakapanda juu. Waliwachoma nyuki, wakakimbia, sungura na kobe wakakaa kitako na kuanza kula asali.

Mara akatokea simba ambaye kwa kweli ndiye aliyekuwa mwenye mzinga ule wa asali. Simba akauliza, ‘Nani ninyi juu?’ Sungura akamwambia kobe, nyamaza.’ Simba akatulia na baada ya muda akauliza tena. Kobe akaingiwa na hofu akamwambia sungura, mimi nitasema, umeniambia asali hii yako, kumbe si yako, ya mwenyewe simba?’ Simba akauliza tena,’Nani ninyi?’ Kobe akamwambia,’sisi hapa!’ Simba naye ambaye amemtafuta sungura kwa siku nyingi akasema,’leo nitampata sungura’

Sungura akamwambia kobe,’nitwae mimi unitie ndani ya mwenge, umwambie simba, jitenge nitupe mwenge nami nitakwenda,nikungoje chini.’ Kobe akasema,’vyema.’ Moyoni mwake akasema, “huyu ataka kukimbia, kuniacha mimi niliwe na simba, ataliwa yeye mbele.’ Akamtwaa sungura na kumtia ndani ya mwenge kama alivyosema. Baada ya hayo akamwambia simba, sungura huyu anakuja.’

Simba akamdaka, akamkamata mkononi, akamwambia,’nikufanyeje leo?’ Sungura akaona hali imekuwa ngumu. Akawaza na kumwambia,’ukinila nyama yangu ngumu.’Simba akamwuliza,’nikufanyeje basi?’ Sungura akasema, nikamate mkia

unizungushe, kisha unipige na mchi, basi utanila, nyama yangu itakuwa laini na nzuri. ‘Simba akamkosa sungura.

Basi akamwambia kobe,’shuka na wewe.’ Akashuka, Akamwuliza, ‘nikufanyeje nawe?’ Kobe naye akmwambia simba,’nitie na tope, unisugue hivi hata nibanduke maganda. Simba akafanya kama alivyoambiwa, akamsugua mikono hata ikachubuka. Akaangalia mikono yake inatoka damu, akanena ‘amenitenda leo sungura aliyeyaanzisha haya.’ Basi akashika njia kwenda kumtafuta.

Kila aliyekutana naye anamwuliza, “nyumba ya sungura iwapi?’ Aliowauliza wakamwambia, “hatuijui.” Kumbe sungura amekwisha kumwambia mkewe, ‘tuhame nyumba hii.’ Wakahama. Simba akaenda kuuliza, wakamwambia watu,’nyumba yake ile pale juu ya mlima.’ Akaenda simba, hata akafika lakini hakuwako sungura. Simba akasema, ‘nitajificha ndani ya nyumba,hata sungura akija na mkewe, nitawala wote wawili.’

Sungura akaja, yeye na mkewe, hana habari lakini njiani akaona nyayo za simba, akamwambia mkewe,’rudi weye,simba amepita hapa ananitafuta mimi.’ Akamwambia,’sirudi,nitakutafuata mume wangu.’ Sungura akamwambia,’wewe mtoto wa watu, rudi.’ Akarudi. Sungura akaenda, akafuata nyayo za miguu, akaona zimeingia ndani ya nyumba yake. Akasema, ‘Loo! Simba yumo ndani. ‘Basi akarudi taratibu, akaenda akasimama mbali, akatoa salaamu, akasema, ‘Salaamu nyumba! Salaamu nyumba! Salaamu nyumba!’ Akasikia kimya. Akanena sungura,’jinsi gani kila siku nikipita hapa, nikitoa salaamu, nyumba hunijibu, labda leo mna mtu humo ndani.’ Yule simba akadanganyika, akaitikia ‘salaamu!’

Akamwambia, ‘Loo! Simba umo ndani, wataka kunila mimi mwanao, ukasikia wapi nyumba kusema?’ Simba akamwambia, ‘uningoje basi.’ Sungura akakimbia, wakafukuzana hata simba akachoka. Aawambia watu. ‘sungura amenishinda basi, simtaki tena.’ Akarudi zake.

**NDOVU NA BINADAMU**

Hapo zamani za kale ndovu alifanya urafiki na binadamu. Siku moja palitokea radi na mvua kubwa. Ndovu alimwendea rafiki yake aliyekuwa na kibanda kidogo kidogo kando mwa msitu na kumwambia: 'rafiki yangu mzuri, je utaniruhusu kuuweka mkonga wangu kwenye kibanda chako ili kuunusuru na mvua kubwa iliyoko?' Yule jamaa alimwangalia kabla ya kusema, "rafiki yangu ndovu, kibanda changu ni kidogo sana lakini kina nafasi ya kutosha kwa mkonga wako nami tu. Basi uweke mkonga wako huo taratibu sana." Ndovu alimshukuru rafiki yake kwa kusema,'umenitendea fadhila kubwa sana; siku moja ntapata fursa ya kuonyesha shukrani zangu.' Lakini ni nini kilichotokea? Mara tu ndovu alipouingiza mkonga wake, alianza kukisogeza ndani kichwa chake, mwili wake mpaka akaishia kumsukumiza mwenyeji wake nje apambane na mvua hiyo. Sasa ndovu alitulia tuli, burudani kabisa, kwenye kibanda cha mwenyewe akimwambia rafiki yake: 'rafiki yangu mwema, ngozi yako ni ngumu kuliko yangu, unaweza kuhimili kipigo cha mvua mimi naikinga ngozi yangu huku ndani isipigwe na vua hilo kubwa.'

Yule jamaa alipoona vile rafiki yake alivyomfanyia, alianza kulalamika. Wanyama waliokuwa kwenye msitu uliokuwa hapo karibu walisikia sauti yake ya kulalamika. Wote walitua na kukaa tutwe kusikiliza mazungumzo ya mvutano yaliyokuwa kati ya jamaa na rafiki yake ndovu. Katika vurugu hilo, simba alitokeza akinguruma na kutoa sauti nzito. "hivi nyinyi hamjui mimi ndiye mfalme wa porini!mnathubutuje kuiharibu amani yangu?" Baada ya kuyasikia hayo, ndovu ambaye alikuwa na cheo kikubwa katika ufalme wa porini alisema kwa sauti laini na ya upole: 'bwana mkubwa, hamna vurugu katika ufalme wako. Nimekuwa na mazungumzo mafupi tu na rafiki yangu hapa kuhusu umiliki wa kibanda hiki ambacho kama unavyoona nimo ndani.' Simba ambaye alitaka utulivu na uvumilivu kuweko kwenye ufalme wake, aliteua kamati ya kulichunguza suala hilo na kumpa taarifa kamili. Alimgeukia Yule jamaa na kumwambia: "umefanya vizuri kuwa na urafiki na watu wangu, hasa ndovu, ambaye ni mmoja wa mawaziri wakuu kwenye dola langu. Usilalamike sana, kibanda chako hakijapotea. Subiri mpaka wakati wa kikao cha kamati yangu na utapewa fursa ya kutosha ya kutoa malalamiko yako. Nina hakika matokeo ya kamati niliyoteua yatakuridhisha. Yule jamaa alifurahi ghaya baada ya kuyasikia maneno hayo matamu ya

mfalme wa pori. Aliamua kusubiri kwa hamu kuu nafasi hiyo; aliamini kuwa kile kibanda kitarudishwa kwenye umiliki wake.

Ndovu alitii amri ya mkuu wake kwa kushirikiana na wanyama wengine kuiteua kamati ya uchaguzi. Wajumbe wafuatao waliteuliwa kushiriki kwenye kamati hiyo: 1. Bw. Kifaru 2. Bw. Mbogo 3. Bw. Ngwena 4. Muadhamu Mbeha kama mwenyekiti, na 5. Bw.Chui kama katibu wa kamati hiyo.

Yule jamaa alipotambua walioteuliwa alilalamika sana na kuuliza kwa nini hakuhusishwa jamaa wa upande wake. Lakini alijulishwa kuwa hilo halikuwezekana kwa sababu hamna jamaa yake aliyetaalamika vya kutosha kuhusiana na sheria za porini. Fauka ya hayo, alijuzwa hapakuwa na sababu ya kuwa na hofu kwa sababu walioteuliwa walikuwa waheshimiwa waliosifika kwa kutopendelea kwao na kupenda haki. Alijulishwa kuwa walikuwa wameteuliwa na Mungu kuzilinda haki za makabila na jamii zote zisizokuwa na meno makali wala makucha marefu. Alikumbushwa kuwa watachunguza suala hilo kwa makini na kutoa ripoti isiyokuwa na mapendeleo.

Ile kamati ilianze kazi yake ya kukusanya taarifa zilizotakikana. Mheshimiwa Ndovu aliitwa kwanza kuhojiwa. Alikuja kwa mbwembwe na kiburi kikubwa na kusema kwa sauti ya ukuu: “Waheshimiwa wa porini, hakuna haja yangu kuwapotezea wakati wenu kwa kuwasimulia kisa ambacho mnakijua kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Tangu zamani umekuwa wajibu wangu kuhakikisha kuwa haki za marafiki zangu zimelindwa; na yaelekea hili limenizulia baa kwa mwenzangu hapa. Alinialika kumsaidia na kumnusuru ili kibanda chake kisibomolewe na tufani. Tufani hiyo ilikuwa imeanza kushika kutokana na mwanya uliokuwako kibandani. Basi niliamua kuchukua hatua ya kukaa kwenye sehemu hiyo wazi na kuitumia; uamuzi ambao nina haki mngeuchukua katika mazingira kama hayo.”

Baada ya kuyasikiliza maelezo ya ndovu, ile kamati ilimwita Bw. Fisi pamoja na wakuu wengine wa porini ambao kwa kauli moja walimuunga mkono ndovu. Mwishowe walimwita yule jamaa ambaye alianza kueleza msingi wa ule ugomvi lakini ile kamati

ilimkata kauli; ‘Jamaa, tafadhali usituvungevunge hapa; yaeleze yaliyo muhimu tu. Tumekwisha kusikiliza maneno mengi kutoka kwa watu wasiokuwa na upendeleo; tunachotaka kujua kwa sasa ni kama hiyo sehemu iliyokuwa wazi katika chumba chako ilitwaliwa na mtu mwingine kabla ya ndovu.’ Yule jamaa alianza kusema, “La, lakini…” lakini ile kamati ilidai kuwa ilikuwa imeyasikiliza maelezo ya kutosha kwa hiyo walitaka kukaa kwa tuo kukata kauli.

Baada ya kutua na kula mlo safi uliogharimiwa na ndovu, walifikia uamuzi wao, wakamwita yule mtu na kusema, “Kwa maoni yetu, mgogoro huu umetokana na kutoelewana na mawazo yako yaliyopitwa na wakati. Tuna imani kuwa Bw. Ndovu ametekeleza jukumu lake teule la kuzilinda haki zako. Nafasi hiyo inatwaliwa ili kukufaidi wewe, madhali mwenyewe hujafikia kiwango cha kuitumia nafasi ipasavyo. Tunaamini pana umuhimu wa kuyafikia mapatano fulani yanayowafaidi wote wanaohusika. Bw. Ndovu ataendelea kuishi kwenye kibanda chako, lakini tunakupa ruhusa ya kusaka pahali pengine na kujenga kibanda kingine ambacho kitakidhi mahitaji yako; nasi tutahakikisha kuwa umelindwa ipasavyo.

Yule jamaa kwa kutokuwa na jingine na kwa kuogopa huenda akashambuliwa kwa meno na makucha ya wanakamati, alifanya kama alivyoshauriwa. Lakini mara tu alipoanza kujenga kibanda kingine, Bw. Kifaru alijitoma ndani kwa kipusa chake na kumfurusha nje. Kamati nyingine iliteuliwa na kufikia uamuzi kama ule ule wa mwanzo. Hali hii iliendelea mpaka Bw. Mbogo, Bw. Chui, Bw. Fisi na wengineo wote wakapata makazi mapya. Sasa yule jamaa aliamua kutumia mbinu nyingine kwa kuwa zile kamati hazikuelekea kumjali kabisa. Alikaa kitako na kusema; “hakuna (mnyama) atembeaye ardhini asiyeweza kutegwa,” au kwa maneno mengine, “ unaweza kumpumbaza mtu kwa muda lakini huwezi kumhadaa milele.”

Siku moja asubuhi, wakati vile vibanda vya zamani vilipokuwa vimeanza kupukutika kidogo kutokana na uzee, aliamua kujenga banda kubwa na zuri huko mbali. Mara tu Bw, Kifaru alipoliona akabumburuka na kuelekea huko alikomkuta ndovu tayari anatabaradi, kulala yu burudani kabisa! Bw. Chui alifuatia dirishani, Bw. Simba, Bw.

Mbweha na Bw. Mbogo wakajitoma milangoni wakati Bw. Fisi analilia akisaka nafasi ilhali Bw. Ngwena naye alijitandaza paani. Muda si muda walianza kubishana kuhusu haki za kuwako. Mabishano hayo yalizaa ugomvi na vita vikali. Wakati wanapapurizana, yule jamaa alilichoma lile banda na kuliteketeza kabisa, wote walikuwemo. Baadaye aliondoka kuelekea nyumbani akijiambia; ‘Amani ni ghali, lakini inahalisi kugharamika,’ Tangu siku hiyo aliishi raha mstarehe.”

**MIGANI YA FUMO LIYONGO**

Fumo Liyongo ni shujaa anayesifika sana katika jamii ya Waswahili na Wapokomo katika pwani ya Kenya. Kipindi alichoishi shujaa huyu hakijulikani kwa usahihi ingawa kuna madai kuwa aliishi baina ya 1160-1204 hata hivyo wachunguzi wengine wanasema Fumo Liyongo aliaga dunia takriban mwaka wa 1580. Hadithi ya Fumo Liyongo inaanzia anapokuwa mtu mzima. Hata hivyo, katika fasihi simulizi ya Waswahili kuna maelezo yanaeleza kuwa Fumo Liyongo alizaliwa Siu ilhali mengine yanasema kuwa alizaliwa sehemu inayojulikana kama Shaka karibu na ulipo mji wa Kipini kwenye Pwani ya Kenya. Maelezo mengine yanadai kuwa Fumo Liyongo alikuwa mtoto wa mfalme lakini mamake alikuwa suria kwa hivyo Fumo Liyongo hakuhesabiwa kama mtoto halisi wa mfalme. Mfalme alipoaga dunia, Fumo Liyongo hakumrithi licha ya umri wake. Ulizuka mvutano mkubwa kati ya Fumo na ndugu yake anayetajwa kama Daudi Mringwari. Mvutano huu uliishia kusababisha Fumo Liyongo atoroke Pate na kuhamia bara alikoishi na Wasanye.

Liyongo alipata sifa nyingi miongoni mwa watu alioishi nao. Wakati huu wote mfalme alitaka kufanya hila ya kumshika na kumfunga Fumo Liyongo. Alimwona kama tishio kwa ufalme wake. Wakati mmoja mfalme alipomwagiza kwenda Pate ili aonekane na Wagalla, Fumo Liyongo alitii. Alipofika huko Wagalla, waliokuwa watu warefu sana, walishangaa kutokana na ukubwa wake. Licha ya urefu wao huo waliweza kumfikia Fumo Liyongo kwenye magoti ya miguu yake ya ajabu. waliamua kufanya mpango naye ili amwoe msichana wa Kigalla, Liyongo alikubali. Lakini Fumo Liyongo alipokuwa huko alituhumu kuwa mfalme alikuwa na nia mbaya naye akatorekea bara tena. Mfalme aliamua kufanya njama na Wasanye ili wamkamate au hata kumwua Fumo Liyongo.

Wasanye walijaribu kila njia lakini wakashindwa. Fumo Liyongo alikuwa na uwezo mkubwa sana.

Siku moja waliamua kumshirikisha kwenye kikoa – kikundi cha kula pamoja. Walipanga kuwa kila mmoja wao atakuwa akipanda mkoma na kuyatunda makoma ili wale wengine wafaidi. Walifanya hivi kwa zamu. Liyongo alishirikiana nao. Ilipofika zamu yake, Fumo Liyongo aliwaambia Wasanye wautafute mkoma waliotaka. Waliutafuta ule mrefu na kumwambia Liyongo, "huu hapa tumeupata!" Liyongo alipouangalia aliona ni mrefu mno, akaijua nia yao. Badala ya kuupanda ule mkoma, alitia mishale yake kwenye uta wake na kutungua ngaa nzima ya makoma wakala wakashiba.

Wasanye walishindwa na la kufanya. Walimwendea mfalme na kumweleza kuwa haikuwa rahisi kupambana na Fumo Liyongo. Mfalme aliposikia hivyo aliwashauri wakamweleze Fumo Liyongo kuwa kulikuwa na mchezo wa gungu (aina ya ngoma) mjini na kwamba hapakuwa na hatari yoyote ile. Kwa kuwa Fumo Liyongo alikuwa mpenzi mkubwa wa gungu na mwao, aliamua kujiunga nao. Mfalme aliposikia hayo, alifanya mpango mzuri na baada ya Liyongo kuwasili mjini tu, akashikwa na jeshi kubwa la askari na kutiwa kizuizini. (baadhi ya wasimulizi wa kisa hiki wanadai kuwa Fumo Liyongo alishambuliwa na Wasanye alipokuwa amekwenda haja kwa mishale na kuumizwa kisha wakamshika na kumpeleka Pate kwa mfalme).

Huko kifungoni alikokuwa, Fumo Liyongo alifungwa kwa pingu na minyororo na askari wakatiwa mlangoni kumzuia asitoroke. Kila siku mamake alikuwa anatayarisha chakula na kumpa kijakazi wao, Saada, kumpelekea. Kila wale askari walipokiona kile chakula kizuri walikichukua na kukila. "Basi siku moja Fumo Liyongo aliamua kumtuma kijakazi Saada kwamamake kwa ujumbe uliojaa mafumbo ya kila aina. Ulikuwa ujumbe wa kishairi, Mkate wa wishwa na kutia tupa ndani. Alitaka aitumie tupa hiyo kuikata minyororo iliyomfunga pamoja na pingu zake na kuondoka gerezani.

Utungo huo ulikwenda hivi:

Kijakazi Saada nakutuma tumwa tumika

Kamwambie mama ni miunga hayalimuka
Afanye mkate pale kati tupa kaweka
Nikereze pingu na minyoo ikinemuka
Niparage kuta na madari kiyakiuka
Niuwe rijali pindi wakiwana nami hateka
Ningie ondoni ninyepee ja mwana nyoka
Niingie mwituni ningurumie ja simba buka
Nali mtu pweke nimeziye katika nyika
Si nduu si mbasi nimeziye katika nyika
Nduu ali mama awasiwe kinda....

Mamake Liyongo alifanya kama alivyotaka Fumo Liyongo. Alitayarisha mikate kadha mizuri na mmoja mkubwa wa wishwa. wale askari walipoiona ile mikate mizuri waliichukua na kuila na kumwambia Kijakazi Saada aingie ndani na kumpelekea ule mkate mbaya wa wishwa. Saada alifanya hivyo alivyoagizwa. Fumo Liyongo alipouana ule mkate alifurahi sana.

Mfalme na wasaidizi wake walikuwa wameamua tayari kuwa watamwua Fumo Liyongo.naye aliomba iandaliwe sherehe ya gungu kabla ya kuuliwa kwake.Watu walikusanyika nje ya gereza alikofungwa Fumo Liyongo kwa ajili ya gungu hiyo. Huku ndani Fumo Liyongo alikuwa akiimba nyimbo nzuri za kuwatumbuiza waliokuwa huko nje.Wakati anaimba alikuwa akizikata zile pingu zilizomfunga pamoja na minyororo yake. Fumo Liyongo aliimba nyimbo za kila aina.huu hapa ni mfano wake.

mringwari taikha fuwanye njooni hwitwa na Fumo Liyongo
Hwitwa na Liyongo Fumo na nduguye shaha Mwengo
Mukaketi yuu ya ulilíye wakusanye watenzi wa ringo
Wakusanye watenzi hiari wajuao kutunga zifungo
Wajuo kufuasa zina na kucheza kwa kumia shingo
Hwitwa hima inukani mwende watukufu wana wa zitengo
Pindi sizo watu wasijakaa ukumbini kikawa kisongo.

Baada ya kipindi kifupi, Fumo Liyongo alifanikiwa kuzikata zile pingu. Alitoka nje kwa kishindo kikubwa huku akiwaua wale askari waliokuwa mlangoni kwa kuvigonganisha vichwa vyao pamoja. Fumo Liyongo alitorokea bara akaenda kuishi karibu na mto Ozi sio mbali na Shaka alikozaliwa. Aliishi huko na mkewe wa ki-Galla aliyejulikana kama Kundazi. Mwanamke huyu alikuwa na mtoto wa kiume aliyempata kutokana na ndoa yake ya mbeleni. Lakini Fumo Liyongo alimpenda na kumtunza kijana huyo kama mwanawe wa kumzaa.

Mfalme naye alikuwa bado na nia ya kumwua Fumo Liyongo. Aliagiza mwanawe Fumo Liyongo ili amtumie kujua siri ya mauti ya babake. (Masimulizi mengine yanadai kuwa mfalme alishirikiana na Wagalla kumshawishi mwanawe Liyongo kwa sababu hawakutaka kuona sifa zake zikienea kwa kasi kama ilivyokuwa). Yule “Mwana wa kigalla” alifanikiwa kuijua siri ya Fumo Liyongo. Fumo Liyongo alitambua kuwa kijana huyo alikuwa amezainiwa au kushawishiwa vibaya na maadui zake lakini alimwelezea siri yenyewe.

Alisema kuwa asingeweza kufa ila kwa sindano ya shaba ikidungwa kwenye kitovu chake. Mfalme aliposikia habari hizo alifurahi sana. Alimwahidi mwanawe Liyongo kuwa atamwoza binti yake ikiwa atafanikiwa kulitekeleza alilotaka. Basi mfalme aliwatafuta wahunzi wazuri wakatengeza sindano ya shaba (baadhi ya masimulizi yanasema kuwa haikuwa sindano ya shaba bali kilomata, aina ya kisu cha shaba kinachotumiwa kutayarisha kili au majani ya mkoma ya kusukia). Yule mwanawe Liyongo alipewa ile sindano ya shaba aende kumwua babake.Siku moja Fumo Liyongo alipokuwa amelala, yule mwanawe alimwendea na kumchoma kwa nguvu zake zote kitovuni. Fumo Liyongo aliamka kwa kishindo kikubwa; alitoa ukelele mzito wa uchungu ambao ulisikika Shaka nzima (inadaiwa kuwa hata leo mwangwi wa sauti ya kilio hicho husikika usiku hasa majira ya mvua kuu). Fumo Liyongo alitimua mbio kuelekea palipokuwa kisima cha maji cha mjini na kupiga magoti huku ametia mshale wake kwenye uta wake. watu walishindwa kumwendea kwa kuogopa kuwa alikuwa amekasirika. Maji yalipoisha mjini walitaabika sana mpaka hatimaye wakashauriana kumtafuta mamake Liyongo.

Mamake Liyongo alimwendea huku akimwimbia tumbuizo nzuri za kumliwaza. Lakini Fumo Liyongo alibaki katika hali ile ile. Alimsogelea pole pole hadi alimfikia na kumgusa naye akaanguka mfu. Huzuni kubwa iliwashika watu wote. Walimchukua Fumo Liyongo na kwenda kumzika. Yule mwanawe Liyongo hakupata ule ufalme aliokuwa ameahidiwa. Watu walimchukia sana naye kwa masikitiko makubwa akatorokea msituni alikofia.